ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13.Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
22. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
23. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
24. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
25. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
26. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
27. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
28. Mhe.Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
29. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe

30. Mhe. Ali Salum Haji - Jimbo la Kwahani
31. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) - Jimbo la Kijitoupele
32. Mhe. Ame Haji Ali - Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk - Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asha Abdalla Mussa - Jimbo la Kiwengwa
35. Mhe. Bahati Khamis Kombo - Jimbo la Chambani
36. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Jimbo la Wawi
38. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Nafasi za Wanawake
39. Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Shaurimoyo
40. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Jimbo la Welezo
41. Mhe. Hidaya Ali Makame - Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) - Jimbo la Mtoni
43. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Paje
44. Mhe. Khadija Omar Kibano - Jimbo la Mtambwe
45. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini
46. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo
47. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani
48. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando
49 Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu
50. Mhe. Mihayo Juma N'hunga - Jimbo la Mwera
51. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni
52. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile
53. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae
54. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
55. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
56. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
57. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
58. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
59. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
61. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
62. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
63. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
64. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
65. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

66. Mhe. Rashid Makame Shamsi	-	Jimbo la Magomeni
67. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa	-	Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Said Omar Said	-	Jimbo la Wingwi
69. Mhe. Said Hassan Said	-	Mwanasheria Mkuu
70. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma	-	Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
72. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
74. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Jimbo la Micheweni
75. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
77. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
78. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
79. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
80. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
83. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika (Mgeni Hassan Juma) alisoma dua

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 – Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Mhe. Naibu Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa asubuhi hii na pia nakupongeza wewe kwa kuniona leo mtu wa mwanzo kabisa kuchangia hotuba hii.

Mhe. Naibu Spika, nampongeza Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, Mhe. Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Afisa Mdhamin wa Pemba pamoja na Wakurugenzi wote na wafanyakazi wote wa wizara hii kwa juhidi zao za kuhakikisha kwamba hali ya nchi yetu inapata mawasiliano mazuri juu ya uendeshaji wa harakati za wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, mimi katika kuchangia kwangu nitachangia sana kwenye mambo mawili au matatu kwa ufupi kabisa. Kwanza niishukuru serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuhakikisha inaondoa kero mbali mbali za usafiri wa nchi kavu, baharini pamoja na anga. Lakini pia niwashukuru watendaji kwa juhudi hizo kuhakikisha pale panapohitajika wanatekeleza haraka kazi zao kwa ufanisi ili maendeleo yapatikane.

Mhe. Naibu Spika, barabara ya Mwanakwerekwe/Fuoni, mimi naishukuru serikali kwa dhati kabisa na azma ya serikali ni kwamba barabara hii lazima ijengwe ili kuondoa adha ya msongamano na usalama wa wananchi wetu. Lakini kwa bahati mbaya Mhe. Naibu Spika pamoja na awamu ya kwanza kumalizika bado naiomba serikali kwa nia njema kabisa hiki kipande kilichobakia cha awamu ya pili kifanywe haraka kwa sababu wananchi wetu kutoka Kwerekwe mpaka Fuoni bado wanapata shida kutokana na vumbi ambalo tunaamini wengi wao afya zao zimeharibika hivi sasa.

Tegemeo langu ni kwamba katika Baraza hili lilijibiwa suala kwenye maswali na majibu Mhe. Naibu Waziri alisema kwamba tunategemea mpaka Disemba ikifika barabara hii iwe imeshakamilika. Najua ni muda mrefu lakini nachukulia kwamba serikali yetu moja ina mambo mengi, mimi naiomba serikali pamoja na jitihada hizo ijitahidi angalau ikifika hiyo Disemba iwe kweli imekamilika barabara hii na kuondoa adha kwa wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia nipongeze sehemu mbali mbali barabara ya Kwerekwe mpaka Fuoni tulipata shida ya maji na mpaka leo bado kuna shida sehemu ya Melinne, Melinne Uzi, Kwarara, Kijitoupele na baadhi ya maeneo ya Fuoni na Pangawe. Kwa hivyo, niiombe serikali sasa hivi utandikaji wa mabomba naona unakwenda vizuri, lakini ningeiomba mamlaka inayohusika ya maji kwa kushirikiana na usafirishaji na ujenzi ifanye kazi hiyo haraka ili wananchi wetu wapate maji waondokane na adha ya muda mrefu ambayo imewakabili.

Mhe. Naibu Spika, jengine nitalolizungumza katika bajeti yetu hii nimeoma maeneo mengi ya barabara zilizotiwa kifusi, lakini bahati mbaya naweza kusema tu kwamba maendeleo mheshimiwa yanapatikana kila sehemu au wananchi wanahitaji katika maeneo yao. Bahati mbaya kutoka Kwarara Melitano Msikitini mpaka kufika huko Kwarara kwa Madina mheshimiwa bado wananchi wa maeneo hayo wana shida kubwa sana. Shida yao waliyokuwa nayo, kero yao na matatizo yao ni daladala hazifiki, watoto wadogo wanasoma kutoka huko Madina wanakuja Kijitoupele Mashine ya Maji, hayo ni masafa marefu lakini pia mama mjamzito anapata shida. Kwa bahati nzuri mheshimiwa mimi Kamati yangu ya Maendeleo ya Wanawake, Watoto, Wazee, Vijana na kina mama nategemea kwamba kina mama wanahitaji mawasiliano ya haraka pindi wanapokutwa na matatizo yao.

Mhe. Naibu Spika, mama utamkuta ana mtoto anampeleka kliniki anataka gari, mjamzito anataka gari. Kwa hivyo, naiomba wizara kwa sasa hivi niseme tu kwamba bahati nzuri naishukuru wizara tukishirikiana mimi na mbunge tumeifanyia kazi barabara hii inapitika. Kwa hiyo, naiomba njia hii ifike huko Madina, hilo nitalisimamia kama mwakilishi kwa wananchi wangu wa Jimbo la Kijitoupele nihakikishe hiyo inatekelezeka na wananchi wanapata manufaa.

Mhe. Naibu Spika, jengine kuna barabara ya Mshelishelini mpaka sehemu inaitwa kwa Walevi, hii naomba radhi wananchi wangu hawanielewi vibaya, ukisema jina jengine utapata tabu, mimi Shihata ukinitafuta jina jengine utapata tabu. Kwa hivyo, huko kwa Walevi sio kama wanalewa watu lakini ni jina la masihara tu mpaka unafika Magirisi na barabara hii naomba ipatiwe kifusi, ili

wananchi wake wapate huduma ya usafiri katika maeneo yao. Hizi barabara zote ukijumlisha kilomita hazizidi tatu, hivyo naiomba serikali kupitia wizara yetu tuhakikishe barabara hizi tunawapatia kifusi, ili wananchi wapite na gari zao kusaidia jamii yetu kwenye maendeleo yao.

Mhe. Naibu Spika, jengine ni kuhusu Shirika la Bandari. Mhe. Naibu Spika, katika nchi yetu tuna sehemu mbili ambazo ndio muhimu kwa uchumi wa nchi yetu; Uwanja wa Ndege na Bandari na tukichukulia asilimia kubwa ya bandari ni chanzo ambacho kinawasaidia wananchi kwa kupata bidhaa mbali mbali na meli kutoka Dubai zinakuja hapa kufanya kazi zao. Lakini kwa masikitiko mheshimiwa mimi nimepata malalamiko na malalamiko haya si ya utani ni ya kweli kweli; wafanyabiashara wengi wenye meli zao wanatukimbia sasa hivi wanakwenda Tanzania Bara. Wanakwenda huko kuteremsha bidhaa zao kwa sababu wanasema wanapata usumbufu katika bandari ya Zanzibar, bora wakakae Bara usumbufu ule hawaupati.

Kwanza kwa kuwa meli zinafunga nje ya bandari kwa muda ambapo muda ule umesababishwa na bandari kukosa nyenzo za kupakulia mizigo haraka na kuondoka. Kwa hivyo, malipo wanayolipishwa kule nje yanaleta usumbufu katika biashara zao na muda ule unakuwa sio wao ni wa Shirika la Bandari wenyewe waliosababisha hivyo. Kwa hiyo, naiomba serikali na namuomba sana Mhe. Waziri awe mkali sana kufuatilia suala hili, kwa sababu roho ya uchumi wa nchi yetu unapitia bandarini na uwanja wa ndege.

Mhe. Naibu Spika, pia jengine ninalolizungumza hapa bandarini kuna utaratibu wa kuteremsha mizigo kwa chombo cha bandari chenyewe, lakini pia inasemekana kuna chombo…

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa umebakiza dakika tano.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Eeh! Haya mheshimiwa.

Mhe. Naibu Spika, kuna chombo kimekodiwa kutoka Tanzania Bara, chombo hiki kwa siku mheshimiwa kinatumia milioni moja. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri anisikilizie chombo chetu kimeharibika, lakini kifaa kilichoharibika hakijatengenezwa mpaka leo. Namuomba sana Mhe. Waziri kwa mwezi tunatumia milioni 30,000,000 kwa mwaka itakuwa milioni mia ngapi? Kwa hiyo, namuomba sana Mhe. Waziri hili tuliangalie kwa usalama na pato la nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, jengine kwa kuwa muda umenipita niseme tu kwamba nimeomba kifusi katika maeneo yangu, na kifusi hiki kitawasaidia wananchi wangu. Lakini pia naiomba tena serikali kuhakikisha kwamba barabara yetu kuu ya kutoka Mwanakwerekwe/Fuoni kama kuna barabara nyengine zimetengewa fedha, basi ni bora kuifanyia hii kwanza, kwa sababu najua yote yanahitaji fedha, lakini tunatizama yenye adha zaidi kwa wananchi wetu. Wananchi wanaotoka Kwerekwe mpaka Fuoni wanaathirika afya zao kutokana na vumbi. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru tena na naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Sina pingamizi nayo, lakini namuomba Mhe. Waziri niliyoyaomba yatekelezwe kwa manufaa ya jamii yetu. Ahsante mheshimiwa.

Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali: Mhe. Naibu Spika, wa Baraza la Wawakilishi kwanza hatuna budi sote kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutupa pumzi hizi kufikia hapa tulipofika, *Alhamdulillah*.

Mhe. Naibu Spika, niipongeze Wizara hii ya Mawasiliano kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa Mhe. Waziri, na niipongeze Kamati ya Mawasiliano ambayo inaongozwa na *Comrade* Mhe. Hamza Hassan Juma pamoja na wajumbe wenzangu na mimi nikiwa mjumbe wa kamati hii.

Mhe. Naibu Spika, nichukue nafasi hii kuzipongeza taasisi zote zilizokuwepo chini ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, kama vile *Airport*, barabara, bandari sehemu zote zilizokuwa chini ya uongozi wa wizara hii niwapongeze watendaji wake, na viongozi kuanzia Waziri mpaka Naibu Waziri, Katibu Mkuu.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli natoa pongezi hizi nikiwa kama mjumbe wa Kamati hii kwa kazi nzuri na uzalendo wa kuipenda nchi yao.

Mhe. Naibu Spika, hawa wenzetu watendaji wa *airport*, bandari, barabara hizi akina Amini hawa wote, hawa ni wazalendo Mhe. Naibu Spika. Kubwa letu tulilokuwa tunakabiliana nalo katika serikali yetu mheshimiwa ni nyenzo, yaani fedha kile tunachokipata ndio tunachokitumia.

Mhe. Naibu Spika, suala la bandari halina tatizo na watendaji wote pamoja na bandari yenyewe. Eneo la bandari mheshimiwa ni dogo halikidhi mahitaji na meli zinazokuja hata tukiwa na *crane* za kutosha ziwe 200, bandari yetu ni ndogo. Mheshimiwa kama kwenye *godown* lako unaweka kontena 100 unataka kuweka kontena 300, *it is impossible* mheshimiwa. Kwa hiyo, njia tuliyokuwa nayo *we have a problem, we have to find the solution and say what is next.* Kwa hivyo, bandari yetu imekuwa ndogo, Mwenyezi Mungu ametuletea neema

wanaita *hadha-min-fadhly-rabiy*, meli zimekuwa nyingi lakini bandari imekuwa ndogo. Kwa hivyo, hata ule uteremshaji wa kontena na uwekaji wa kontena hautoshelezi na meli zetu tulizokuwa nazo.

Mhe. Naibu Spika, sasa tukubaliane kwamba ule uwanja wa Bwawani pale ulikuwa unakidhi angalau kuipa pumzi ile bandari kwa kuweza kupeleka kontena pale. Lakini kama hatutapata *solution* ya ile bandari kwa muda huu ambao Mwenyezi Mungu ametuletea baraka na *revenue* yetu hatuwezi kwenda na jambo jengine lolote. Hata awe Mkurugenzi atoke Marekani aje Mzungu tatizo lile… uzalendo wanaofanya watu wa pale Mhe. Naibu Spika, *Subhanallah* tuiombee nchi uzalendo wanaofanya watu wa bandari na sehemu za barabara hizo za ndani, Mhe. Naibu Spika hawa viongozi watendaji wana uwezo wa kuifanyia mageuzi Zanzibar bila ya kutegemea kampuni ya nje, katika mambo ya barabara na lami.

Kwa hivyo, natoa wito Mhe. Naibu Spika nilikuwa niwaombe wawakilishi wenzangu kwa kuwa mimi ni mfanyabiashara ndugu yangu Abdalla yupo, Jaku tuwaelezeni umma kwamba hili suala ni kubwa na tutafute solution ya jambo hili.

Mhe. Naibu Spika, kitu kilichonisikitisha kwenye ripoti yangu ya kamati *page 18-19*, katika ripoti hii ya kamati. Mhe. Naibu Spika, Marehemu Mzee Abeid Amani Karume Mwenyezi Mungu amlaze mahala pema. Amiin. Ni kwamba alianzisha ile Benki ya Watu wa Zanzibar (*PBZ*). Leo Mhe. Naibu Spika, katika ripoti hii bandari ina *revenue* kubwa, leo Benki hii ya Watu wa Zanzibar ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, leo bandari wanataka fedha za kuendesha vifaa vyake. *People's Bank of Zanzibar* ni mali ya serikali si mali ya binafsi, si mali ya watu waliokuwa wawili au watatu. Kwa kweli nasema ni jambo la kusikitisha nataka serikali ifanye uchunguzi wa kina, lazima humu ndani kuna vitu vinafanyika kwa baadhi ya watendaji wa Bodi na watendaji wengine si kila anayepepesuka ni mlevi, nasema kuna baadhi ya Wajumbe wa Bodi wanataka kuhujumu uchumi wa nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, mimi nasema niko tayari nikiwa Mzanzibari ninayeipenda nchi yangu taasisi zote zinazokabiliwa na fedha za kukopa, basi niko tayari kuwasimamia kutoka Benki ya *KCB*, *Exim Bank* na benki zote zilizokuwa ndani na nje ili Zanzibar tupate kusonga mbele. Mhe. Naibu Spika, hatuwezi kwenda hivi tukitaka kumchinja nyani usimtazame uso wake. *PBZ* hiyo mheshimiwa kwa hali ilivyo na hali ya ripoti hii tuliyopewa, mimi hapa niko kwenye ripoti imekuwa na watu binafsi umimi, umimi. Pia kuna watendaji wengine ndani ya Bodi katika *regulator* ya *BoT* wamekataliwa, yaani kutokana

na uwezo wao hawana uwezo tena. Mhe. Naibu Spika, baadhi ya Wajumbe wa Bodi nasema sio wote wamekataliwa na Benki Kuu. Sasa mheshimiwa lazima tuwe wakweli. Mhe. Naibu Spika, katika mazingira tuliyokuwa nayo sisi tegemeo letu kubwa kwa wananchi ni Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, nije katika suala la barabara. Mhe. Naibu Spika, mimi niombe serikali hii yetu sana. Mhe. Naibu Spika, Marehemu Mzee Abeid Amani Karume tulipofanya Mapinduzi ya Zanzibar lengo la Mapinduzi ya Zanzibar ni kuwaletea wananchi maendeleo bila ya kujali rangi, kabila wala dini. Kwa hivyo, mheshimiwa Mapinduzi yalifanyika kwa kuwaletea watu huduma bora kama vile maji, umeme, barabara, skuli na mambo mengine.

Mhe. Naibu Spika, tulipofanya Mapinduzi 1964 mpaka 1979 kwa bahati nzuri Mzee Jumbe; Rais Mstaafu mwaka 1979 alianzisha rasmi Baraza la Wawakilishi. Mhe. Naibu Spika, humu ndani lengo lilikuwa kwamba wananchi wasikilizwe wanataka nini. Mheshimiwa tumekuja hapa nikiwemo na mimi kuzungumza kwa niaba ya wananchi. Sasa Mzee Jumbe na kwa bahati nzuri leo nchi hii Waziri wa Mawasiliano ni mtoto wa Marehemu Mzee Abeid Amani Karume, Mwenyezi Mungu amlaze mahala pema, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mawasiliano ni mtoto wa Rais Mstaafu Aboud Jumbe. Niwaombe viongozi hawa, wazee wenu wameweka historia, Mzee Jumbe ndiye aliyetufanya sisi tuingie humu leo, tangu 1979 kwa kusikiliza kilio cha wananchi.

Mhe. Naibu Spika, Ahadi nyingi zinatolewa na Rais, ahadi nyingi zinatolewa na Baraza la Wawakilishi, mpaka Makamo wa Pili wa Rais, kwa miaka mitatu hakuna ahadi moja inayotekelezwa, baadhi ya ahadi zinazotolewa na Serikali. Mheshimiwa *it gives me worry*, mimi nimekuja hapa kwa niaba ya wananchi, sikuja hapa kutafuta ajira au posho, sikuja hapa kutafuta mshahara, nina uchungu na nchi. Mapinduzi ya Zanzibar na wananchi ndio walionifanya mimi nifike hapa. Mimi nimesomeshwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, niombe, kuna barabara Jimbo la Uzini, kuanzia Miwani, Manzese, Pagali, Bambi, Uzini nzima. Mhe. Naibu Spika, Uzini hawataki lami, wanataka barabara za ndani na Mhe. Naibu Spika, kuna barabara hizi za Pagali, Ndondongwe, Bambi, nilitakiwa kuchangia milioni ishirini, Mhe. Naibu Spika, kabla ya kuapishwa, nilikwenda Idara ya barabara kupitia Serikali, Idara ya Barabara ni watu waungwana, Serikali Katibu Mkuu wa Mawasiliano nilikabidhi milioni ishirini *cash* kwa kusaidia na Serikali ilisaidia.

Mhe. Naibu Spika, mimi niko tayari kushirikiana na Wizara, wakulima wetu wana matatizo, leo Jimbo la Uzini zima, mama zetu wanapoteza roho, leo ng'ombe hawawezi kupita, wana Uzini hawataki lami mule ndani.

Sasa ninataka kuuliza hili Baraza la Wawakilishi ni nani anaesimamia kuona kwamba ahadi zinazotolewa ndani ya Baraza la Wawakilishi, ahadi zinazotolewa na Rais, ahadi zinazotolewa na Mawaziri, ni nani anayesimamia kutekeleza ahadi hizi. Mimi nafahamu Baraza la Mapinduzi wakati wanapokaa kwenye vikao kunakuwa Sekreteri maalum inayosimamia utekelezaji. Kwenye Baraza la Mapinduzi ulitakiwa ufanye moja mbili tatu, lakini humu ndani Mhe. Naibu Spika, ndio... kwa sababu Mhe. Naibu Spika, hawa wananchi walio wengi ndio waliotufikisha hapa, tumepata ushindi wa kishindo CCM kutokana na wananchi wakulima na wakwezi, sasa usiwache mbachao kwa msaala upitao, zimwi likujualo halikuli likakwisha, usidharau wakunga uzazi ungalipo, tutakuja kuwahitaji hawa wananchi.

Mhe. Naibu Spika, mimi leo alhamdullilahi kupitia Chama cha Mapinduzi, nikiwambia wananchi wa Uzini, jamani tunaitwa na Rais basi wako tayari kuja kwa miguu mpaka huku, lakini mwenzangu akiwaita anakwambia ah! Lete elfu kumi na tano, lete gari, sasa lazima tutizame hilo Mheshimiwa, *these people make somebody stupid, you cannot make always stupidity*, watu wana shida Mheshimiwa.

Mimi niko tayari kwa Jimbo zima la Uzini barabara za ndani kusaidiana na Serikali, Serikali yetu ishafanya mengi Mhe. Naibu Spika, lakini kuna vitu *purposely*, bwana mimi ukitaka kuniwekea vikwazo ninyanganye leseni yangu, lakini unakuja kuwaumiza wananchi Mheshimiwa, wakulima wanalia njia hazipitiki ndani.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo nataka niombe Serikali hii sikivu, nimuombe Mhe. Rais wa Zanzibar haya tunayozungumza humu yatekelezwe, yaelekezwe lakini tutakuja hapa tunaripuana, mtu ukisimamia unaambiwa huyu siye, yale majungu na fitna, tungeliiweka nchi hii katika maendeleo *wallahi.*

Mhe. Naibu Spika, nchi ingelikuwa pepo hii, lakini ukisimama kila mmoja siye huyu, ndiye huyu nani siye nani ndiye mimi sielewi, yaani Wazanzibari tunataka nini, tunakuja hapa mimi kama Razza niko tayari kwa Jimbo langu lote la Uzini kusaidia maji, barabara na uwezo Mwenyezi Mungu kanijaalia ninao; walionifikisha hapa ni wananchi, sasa nisaidieni kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi, leo tumo sote humu. Mimi nimekuja hapa kwa niaba ya Chama cha Mapinduzi, sikuja hapa kama Kampuni ya Hassan and Son's. Kwa

hiyo niombe Mhe. Naibu Spika, kwa heshima zote wananchi wetu wanashida. Ninamuomba Waziri, ahadi zilizotolewa na Rais kwa barabara, maana yake Mheshimiwa tutakuja hapa tupigane buti pu pu *that is not a solution*, kwa miaka mitatu hapa tunapigiana buti, lakini ahadi za Rais, ahadi ya Makamo wa Pili wa Rais ndani ya Baraza hakuna, tena wamekuja na kitabu hiki.

Mhe. Naibu Spika, mimi naamini Wizara ya Mawasiliano na Waziri hapa Mhe. Ali Abeid Amani Karume, nafikiri hii bajeti wamepangiwa, ninaamini ingelikuwa bajeti hii yao kutokana na Muasisi na Mustafa Jumbe siamini kama bajeti hii wangelikubali kuja nayo, lakini kwa sababu uchaguzi tumechelewa, muda umekuwa mdogo, lakini ninasema ninakuombeni Mhe. Waziri wa Mawasiliano, Naibu Waziri wa Mawasiliano, mwenzangu tena kada huyu Naibu Waziri wa Mawasiliano, ni kijana mzuri amepea ni Komredi huyu wa Chama cha Mapinduzi pamoja na Katibu Mkuu na Watendaji wake. Mhe. Naibu Spika, tunaomba sasa hivi barabara zetu na hizo zinazokuja wapewe wazalendo kufanya kazi. Mheshimiwa Umbuji wameokoa bilioni mbili barabara ya lami Umbuji, kwa hiyo tuwapeni zana, tukaeni humu tutatuwe matatizo ya nchi yetu, lakini mtu akisimama huyu ndiye huyu siye, hatuwezi kufika.

Mhe. Naibu Spika, mimi naliomba sana Baraza hili, katika yote Mzee Jumbe kalileta Baraza la Wawakilishi ili wananchi wasikike matatizo yao, Mheshimiwa naomba Jimbo langu la Uzini, Mheshimiwa niko tayari kwa mwezi huu mtukufu wa Ramadhan, hata nije kuongeza nyengine milioni thalathini matatizo yao yaondokane. Niko tayari kushirikiana na Serikali. Ninaomba sana Mheshimiwa ili tuweke jina letu pamoja na Rais wetu katika hali njema.

Mhe. Naibu Spika, nasema Wazanzibari sisi tuliokuwemo ndani uwezo tunao, nia tunayo na sasa tuna-*deliver* kwa wananchi kila ambao wamekuwa wametarajia ndani ya Chama cha Mapinduzi. Mheshimiwa mimi ninaunga mkono, sina kinyongo na jambo hili, lakini tushirikiane, ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Mohammedrazza, mchangiaji anaefuata Mhe.Nadir Abdulatif na baada ya Mhe. Nadir atakuja Mhe. Abdalla Maulid Diwani na atafuata Mhe. Shadya Suleiman.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yusuf Al-Wardy: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia uzima kama kawaida na vile

vile ningeomba dakika tatu za Mhe. Razza unipatie mimi ili niendeleze na zangu nipate nichangie vizuri.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuanza tu ningewapongeza sana Waziri wa Wizara hii, Naibu Waziri pamoja na Watendaji wote kwa ujumla kwa kazi nzuri wanazozifanya na mimi nitakuwa na michango yangu pamoja na maswali yangu kadhaa ili nije nijibiwe hapo baadae.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitaanza na mambo matatu; nitaenda kwenye ujenzi, mawasiliano pamoja na usafirishaji. Lakini nikianza kwenye ujenzi ningependa kuzungumzia sehemu ya barabara. Kwa kweli kwanza ninaipongeza Serikali sana kwa juhudi zake za kujenga barabara Zanzibar nzima sehemu nyingi sana ina barabara nzuri. Mimi ninaipongeza sana, imejitahidi na kila siku inapokaa inatafakari kujenga njia za *shortcut* ambazo zitaweza kusafirisha wananchi kwa njia nyepesi kabisa kuliko zile za kuzunguka.

Mhe. Naibu Spika, vile vile ningezungumzia suala la barabara yangu ya Jimbo la Chaani, kwa sababu kwenye kipaumbele nashangaa kwamba barabara hii haipo wakati barabara ni maarufu, barabara ya zamani, barabara muhimu ambayo ina-*connect* mambo mengi ya mawasiliano hawa kwa wageni wanaokwenda Mahotelini upande wa Kiwengwa, upande wa Pwani Mchangani, upande wa Matemwe na upande wa Nungwi kwa ujumla. Njia hii ni *shortcut* na ni nzuri na inatumika sana, lakini kutokana na hali iliyokuwa nayo sasa hivi ni mtihani kabisa kabisa, haipitiki kabisa ina mashimo kila mita moja.

Ningemuomba sana Mhe. Waziri, hili jambo angelichukulia la dharura kwa barabara hii kuliko hizo nyengine zilizoekwa humu ndani. Zote ni muhimu lakini barabara hii ni muhimu zaidi na vile vile hata wazee wenyewe wa *Afro Shirazi Party* wapo wameniita wakanambia basi angalau lieleze hili suala tukumbukwe na sisi, sio zinakumbukwa barabra nyengine wakati wakati nyengine ziko vizuri kuliko hii, hali iko ngumu sana Jimbo langu la Chaani, barabara nakuombeni sana Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Waziri barabara hii ishughulikieni, imalizeni kwa sababu ina mtihani mkubwa kuliko barabara zote na ningeomba sana mkafanya kuja kutembelea kwa dharura kabisa, ili kuchukuwa hatua zinazostahiki.

Mhe. Naibu Spika, nakwenda kwenye ujenzi. Mimi nampongeza sana Mhe. Marehemu Abeid Amani Karume, miaka hiyo tuangalie mfano mdogo barabara za *round-about* za Michenzani upana wake *round-about* ile inatoka maji, majumba yamepangwa vizuri, lakini sisi tuko awamu ya miaka hamsini

hakuna… mpaka sasa hivi *action* ambayo imechukuliwa tukapata angalau zile akili zake alizokuwa akizitumia yeye, tupo nyuma sana. Mimi nilimwambia mtu jana naamini angelikuwa yuhai mpaka leo mzee wetu basi hii ingekuwa Dubai sasa hivi, kwa sababu miaka hamsini iliyopita iko hali ile, barabara zile zina mita karibu mita ishirini upana wake, majumba mazuri kajenga lakini leo Wizara inawaachilia tu watu wanajenga kiholela kwenye mabarabara, alama inawezekana zinawekwa lakini hawachukuwi *action.* Mimi ningeomba wachukue *action* na wamruhusu mtu angalau mita ishirini na tano kutoka barabarani ili siku za mbele kukitaka kutanuliwa barabara Serikali isipate matatizo ya kulipa nyumba.

Mhe. Naibu Spika, vile vile ningeenda kwenye ujenzi ambao wa barabara vile unavyojengwa. Mimi nafurahi sana wakipata hawa wajengaji wa *local* yaani Watanzania Wazanzibari wenyewe lakini tuangalie na kiwango, tusikae tu tukasema tuwape Wazalendo lakini kazi zao zikawa sio nzuri. Sasa mimi napendekeza kwamba tuangalie vile vile Kampuni za rahisi za nchi za nje ambazo zina uzowefu zaidi na zina-*quality* zaidi, sisemi zilizokuwepo kwamba hazina *quality* lakini tutizame nyengine. Tunaona baadhi ya barabara zinatengenezwa lakini baada ya mwaka mmoja zinaanza mashimo, zinaanza matuta matuta ukitembea na gari kama vile vile gari ya *rally* inapotembea kule msituni. Mimi nitaishia hapa kwenye suala la barabara na nitaingia kwenye vibali, hili hili suala la ujenzi.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri, vibali kwa kweli hasa vibali vya kutengeza vituo vya mafuta vinatoka sijui vinatoka kwa njia gani, kwa sababu vituo viko vingi vinajengwa sasa hivi vipya lakini viko kwenye maeneo na hii ni hatari kwa nini vibali vile wasipewe kwanza mpaka sehemu ikachunguzwa uzuri. Naamini anayejenga tayari keshapitia sheria zote, kashapita kwenye *system* zote mpaka akaweza kujenga lakini inaonekana hivi vibali havijawekewa vikwazo na watu hawaangalii hali halisi nini itakuja kutokezea baadaye. Ningemuomba sana Mhe. Waziri na Naibu Waziri, vibali hivi sheli zinazojengwa ni hatari kwa wananchi, zinajengwa chini ya nyumba. Nyumba ziko tele zimezungumza ndani ya mita hamsini, ile sheli ikija ikaripuka mtihani mtupu, sheli zingepangiwa sehemu maalumu na zile zilizokuwepo katika vijiji vya watu basi zifungiwe wapewe sehemu nyengine wajenge sheli sehemu nzuri.

Zanzibar sasa hivi kila mita mia tatu mjini kuna sheli ya mafuta, huu utakuwa mtihani kweli kweli, ningeomba sana Wizara ikatizama suala hili ili tukaendelea na mambo mengine.

Mhe. Naibu Spika, vile vile vibali vya ujenzi. Vibali vya ujenzi Waheshimiwa Wizara yako inapotoa vibali mimi nashauri sana visimpe mtu tu kibali kama hajui anajenga nini, mtu anaenda kuchukuwa kibali lakini anajenga uchafu mtupu, maana yake kuna kujenga nyumba, kuna kujenga duka, lakini kuna kujenga uchafu. Mji sasa hivi umechafuka kila mmoja anajenga anavyotaka akeshapewa kibali, hajaangaliwa sijui ramani; mimi ningeshauri iangalieni ramani ipasisheni nzuri, ipokeeni sio nzuri mwambie akarekebishe.

Mhe. Naibu Spika, vile vile nitaendelea kwenye suala la vibali hilo hilo. Mheshimiwa mimi nampongeza Mhe. Hamad Rashid kwa hotuba yake ya mara ya mwisho, alizungumzia kwamba kuna meli thamanini na tatu za uvuvi ndani ya Zanzibar zinavuwa *deep sea*, lakini cha ajabu humu ndani kuna meli mbili tu ambazo zimesajiliwa za uvuvi, meli thamanini na moja nzima sijui zimesajiliwa nchi gani. Mimi ningeomba sana nchi zote zinazovua hapa basi Mhe. Hamad Rashid na Mhe. Waziri wa vibali vya meli hakikisha zile meli zinazotaka kuvua Unguja zikate vibali Zanzibar, kama hazitaki basi ziondoke tutafute wengine lakini sio nchi meli thamanini na moja zinavua, lakini humu tuna meli mbili tu ambazo zilizosajiliwa za uvuvi zinazotambulikana na Serikali au na Wizara yake, huu ni mtihani. Mimi ninampongeza sana kwa kauli yake aliyosema kwamba atahakikisha meli zile zinakuja kujisajili Zanzibar, ni wazo zuri sana.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye mada ya pili, suala la mawasiliano. Mheshimiwa sasa hivi Kampuni za Simu tunazo lakini hizi Kampuni zina maajabu. Kampuni saa nyengine unatia kadi elfu tano, elfu kumi inaliwa yote yaani unaibiwa kwenye mazingira ya utatanishi, watu wanalalamika, simu nafikiri *charges* zilizowekwa nafikiri wanachaji *double* au wanazidisha maana yake almuradi mimi naomba sana muchunguze sana hizi Kampuni za Simu, watu wakitia kadi mara unakuta ghafla tu kazungumza dakika moja kakatwa elfu tatu, kajiunga na *Internet* muda sio muda ishakwisha, wanaibiwa kwa njia ya mazingira ya utatanishi. Ningeomba sana hizi Kampuni zichunguzwe na ziangaliwe vipi zina-*charge* na vipi zinaendelezwa, sio Kampuni imeshakuja kufunguwa halafu haiendelezwi au haiangaliwi.

Mhe. Naibu Spika, vile vile twende kwenye suala la mawasiliano ya *internet.* Mhe. Waziri, Mhe. Naibu Spika, hii *internet* kwa kweli imegeuka balaa ndani ya Zanzibar. *Internet* hii hii mimi nawapongeza sana kwanza ndugu zetu usalama wa taifa, ni watu wastaarabu watu watendaji kazi wazuri, watu ambao wanasimamia nchi vizuri pamoja na polisi wa Jamhuri ya Muungano, watu kama hawa wanaoharibu majina ya Serikali, wanaotukana viongozi wa nchi katika *internet* wanatukana na wanatunga picha za ajabu ajabu kwanini swala

hili Mhe. Waziri, usilikemee na usiwafungie hawa watu. Leo *internet* hatumii mtu kwa *personal use* mwenyewe, anatumia kutengeza *website* ana-*create face book special* tu kwa kutukana Serikali, kwa kutukana viongozi wa Serikali na kuzungumzia mambo ya uongo na mengine hata mimi hapa nikizungumza mengine huenda nikatia chumvi *head line* ile ili watu wapate wasome vizuri.

Mhe. Naibu Spika, mimi ningeomba sana hawa wote wanao-*create* hizi *problems* wakamatwe, mimi ningeomba sana usalama wa taifa na mapolisi wote hawa watu wawachukulie hatua. Wanamtukana Rais wetu, wanatukana Serikali, wanatukana kila mtu, sio kazi zao wafanye kazi zao. Mimi ningeomba sana Wizara hii kwa yule yeyote ambae atafanya suala hili akikamatwa afungiwe na akamatwe sio aachiliwe tu anatukana, tusijiwekee tu *freedom of speech*, waache wakae nazo huko huko Ulaya wasituletee sisi, kama hizi za kutukana viongozi na nchi yetu. hapa tukiendelea na mambo ya kukubali *freedom of speech* za hawa wanoleta mambo haya basi hapa kesho kutwa watajikusanya watu waliokuwa wapumbavu waseme wanataka kuoana wenyewe kwa wenyewe na wanawake watakuja kufanya maandamano waseme wanataka kuoana wenyewe kwa wenyewe kwa sababu ya suala la uhuru.

Mhe. Naibu Spika, vile vile nizungumzie suala la mawasiliano kwa waendesha daladala. Kwa kweli waendesha daladala wengi wao wako tayari kuuwa mtu, kuuwa watu ishirini kwa nauli ya shilingi mia tatu, wanaendesha vibaya, wengine wanakunywa mwanzo pombe halafu ndio wanaanza kuendesha gari, hakuna *speed limit* wanaenda mia moja arubaini katika njia ambazo hazistahiki. Mimi ningemshauri sana Mhe. Waziri na Naibu Waziri, kuna vifaa maalum vya kuzuia gari *speed limit* kwanini *engine* zile zisifungwe zikaweka mwisho *speed* thamanini au sabiini na atakapoendesha *speed* zaidi ya hapo kuna kimashine unakitia kwenye usukani wake kinajuulisha wewe Wizarani kwako kama huyu gari fulani inakwenda *speed* Fulani.

Kuna nchi zinatumia kama Dubai, Oman gari za kukodi na gari za abiria wanatumia hii *system*, yaani wewe wala huna haja ya kumfuatilia barabara, unakifunga tu kifaa kwenye usukani wake anapotia ufunguo anapokwenda *engine* inakueleza kama huyu kavuka *speed limit* kwa muda fulani siku fulani na inawezekana kila wiki mukawakusanya wale mkawapiga *fine*. Hivi vifaa vipo lakini nashangaa kwamba hawa waendesha daladala wanauwa watu kila siku, wao ndio vurugu mechi, wanaleta daladala nyengine hazina hata kiwango. Huko Uingereza zinapakiwa Nguruwe, zinapakiwa maiti wanapakia watu kwenye daladala mbovu.

Mhe. Naibu Spika, mimi ningemuomba Mhe, Waziri, aangalie daladala za kuja zile daladala za zamani za asili, daladala nzuri sana na zina usalama zikifungwa *speed* tu basi zitakuwa nzuri. Sasa hivi tunaletewa gari za maajabu ajabu hazielekei, zinaharibu haiba ya nchi na sijui hata zinatoka wapi. Mimi ningependa sana wakadhibitiwa sana hawa na wale wanaokunywa wakati wanaendesha abiria wapimwe, kuweko na maaskari *special* wana mashine za kupima pombe pale pale wanaposimamishwa, wanahatarisha maisha.

Mhe. Naibu Spika, vile vile niendelee kwenye suala la usafirishaji sijamaliza.

Mheshimiwa swala la bandari. Bandari, Wakurugenzi, Viongozi, Wafanyakazi ni watendaji wazuri lakini bandari yetu mtihani mtupu; leo bandari ile mpaka leo nafasi ya kuweka *empty containers* ya kutoka pale kwenye bandari kuwekwa nje hakuna. Hapo mwanzo Mhe. Razza kasema ilikuwa Bwawani lakini sasa hivi kwanini Serikali isichukue hatu mbadala; kuna Kibanda Maiti kwanini ma-*containers* yasipelekwe pale, kuna hapo Maisara viwanja tele vya mpira kwanini kimoja kisizuiliwe kikaekwa ma-*containers* kwa muda. Malindi mimi sishauri kwa sababu iko kwenye Mji Mkongwe lakini kule Maisara mwisho mwisho kwa nini miwanja miwili isizuiliwe ikawekwa haya ma-*containe*rs ile zile meli zisipate usumbufu.

Mhe. Naibu Spika, hata tukiangalia meli zilizokuja mwaka uliopita na mwaka huu ni tafauti, meli karibu 99 zimepunguwa kwa sababu ya haya haya ya matatizo. Mimi ningeomba sana serikali, serikali ina viwanja vingi na ikitaka jambo lake inaamua tu, lakini mpaka leo hatua haichukuliwi meli haziji kwa sababu wanaona mazonge, zinakaa pale wiki mbili, wiki tatu wafanyakazi wengine wa bandari hawajaliwi, mtu anatembea mle ndani kama pia.

Ningeomba sana viongozi hawa wakatafutiwa *golf course car* zile mbili mle ndani ili kazi ziende kwa haraka. Kiongozi huyu kaitwa huku ana kigari chake anakwenda upande wa pili, kaitwa huku ana kigari chake anakwenda upande mwengine mtu ataendeshwa kwa miguu mpaka masaa mangapi wakati wafanyakazi wa bandari sasa hivi wanafanya kazi asubuhi mpaka saa kumi za usiku. Hii hali naomba sana ifikiriwe na Mhe. Waziri aichukulie hatua ya muhimu sana kuhakikisha kwamba makontena yale *empty* yote yanaondoshwa mule bandarini na yanatafutiwa uwanja haraka iwezekanavyo.

Pia nije kwenye mambo ambayo yanacheleweshwa *service* za bandari ndani. Mhe. Naibu Spika, ndani ya bandari jambo dogo tu utaambiwa ukalipe *TRA*, kule ndani kwa nini ofisi ya *TRA* ya malipo na benki isifunguliwe, iwemo mule ndani ya bandari kama ilivyo *ZRB* na maeneo mengine. Leo kitu kidogo

kitamfanya mtu atoke aende *TRA* nje. Kuna watendaji wazuri wa *TRA* ndani ya bandari, watendaji wazuri wa *ZRB* na mambo mengine lakini utakuta pale hakuna lolote.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe umebakiwa na dakika nne.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Vile vile Mheshimiwa kitabu hiki mimi nimekiangalia vizuri kwenye masuala ya anga, kuna ndege nyingi zimekuja lakini kitabu hakielezi ndege hizi ni ngapi za *commercial*, hizi za *private* zimeelezwa, sasa ningependa kujua.

Sasa nakwenda kwenye maswali yangu, nitaomba Mhe. Waziri aje anijibu suala la barabara. Katika barabara ni tani ngapi inajengwa barabara na shilingi ngapi serikali inalipa kwa yule mkandarasi kwa kilomita moja.
Swali langu la pili ni hatua gani ambazo watakuja kuzichukua wakati hawa waendesha daladala wanaofanya vurugu hasa kwenye *speed limit* zaidi ya inayotakiwa.

Swali langu la tatu, watachukuliwa hatua gani hawa wanaotumia *internet* kwa kutukana serikali, viongozi kwa wingi na kwa kutengeneza *website* ambazo hazina maana.

Swali langu la nne ni lini barabara yangu ya Chaani ninahakikishiwa itamalizwa kwa kiwango cha lami.

Swali langu la tano, naomba kujua kwamba ni lini uwanja utatafutwa kuweka makontena nje kuliko kukaa bandarini ili zikija meli mpya ziweke kontena zake. Swali langu la sita ni suala la ndege, nitapenda kujua ndege hizi zinapotua zinalipa shilingi ngapi, ndege kubwa na ndogo (*landing charges*). Vile vile na hizi *private jet* wanalipishwa shilingi ngapi wanaokuja na inapokaa kila siku inalipa shilingi ngapi.

Mhe. Naibu Spika, nimpongeze Mhe. Rais Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kununua meli Meli ya MV. Mapinduzi II kuhakikisha kwamba wananchi wanapata bei nafuu na meli nzuri. Vile vile kama ninavyosema siku zote viongozi wote wasimuangushe Mhe. Rais ili kazi ziende vizuri.

Mimi naiunga mkono hoja kwa asilimia 90 na asilimia 10 nangojea majibu hapo Mhe. Waziri atapokuja kujumuisha bajeti yake. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii kuichangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji. Awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia uzima wa afya kufika katika Baraza lako hili tukufu. Vile vile niwapongeze kwa dhati ya moyo wangu kabisa Mhe. Balozi Ali Karume kupewa kijiti kuongoza wizara hii pamoja na naibu wake na vile vile kaka yangu mpenzi Mustafa Aboud Jumbe kuwa Katibu Mkuu wa wizara hii, nawapa hongera sana. Imani yangu kwamba tutaondoka hapa tulipo kwa utendaji wao ambao umetukuka na imani zetu kwao.

Mhe. Naibu Spika, niende moja kwa moja katika mchango wangu, nazungumzia juu ya suala zima la *UUB* ukurasa wa nne(4). *UUB* ni taasisi nyeti sana kwa Zanzibar inapaswa kupongezwa sana juu ya utendaji wake wa kazi, lakini imefika muda sasa hivi *UUB* iangaliwe kwa jicho la huruma kabisa. Kwa sababu *UUB* sasa hivi hawana vyombo, vyombo vyao vimepitwa na wakati ni vyombo vya muda mrefu sana tunawapa wakati mgumu juu ya utendaji wao wa kazi katika kutengeneza nchi yetu au kuing'arisha kwa barabara nzuri. Pamoja na ujabari wao wa kufanya kazi ni mahodari lakini upande wa vyombo unawaangusha sana.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri namuomba kwa dhati yake kabisa afanye afanyavyo wale watu wawezeshwe ili wawe na vyombo angalau vya kuweza kukimu hizi harakati zote za utengenezaji wa barabara. Kwa mfano, hata huo mtambo wa kupikia lami sasa hivi spana mkononi, hivyo wanapata wakati mgumu sana. Lengo lao zuri kufanya kazi kwa muda, lakini kutokana na uchakavu wa vyombo vile wanashindwa. Kwa hivyo, Mhe. Waziri najua uhodari wake katika hilo halitampa shida sana afanye afanyavyo kiasi ya wale watu nao wajisikie kwamba na wao wanajaliwa juu ya suala zima la vyombo.

Vile vile kuna suala la barabara. Kama tunavyotambua kwamba pamoja na *UUB* kuwa ni wajenzi wa barabara, kuna Mfuko wa Barabara na shughuli nyengine. Nataka kuuliza ile barabara yetu ya Mpendae - Jang'ombe imefikia hatua gani. Kwa sababu ni muda mrefu sasa hivi (mwaka mmoja) na bahati nzuri barabara ile ilisaidiwa na Mhe. Mbunge wa Mpendae kutoa shilingi milioni mia moja, lakini bahati mbaya mpaka dakika hii imetiwa lami nyepesi na imeshaanza kuchimbuka iondoke katika ubora wake. Kwa hiyo, naomba kwa ridhaa yake kabisa Mhe. Waziri atapokuja anambie hatima yake ni nini na lini barabara ile itaweza kuwekwa sawa katika kiwango cha lami kabisa ikiwa ni barabara bora katika jimbo letu lile.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia nitakwenda katika suala jengine la barabara ya Kwa Mabata-Kinuni. Hii ni barabara moja muhimu sana ya kuunganisha watu wetu wa Kinuni kuja katika mji na kwa bahati nzuri viongozi wa majimbo yale wamejitahidi vya kutosha kwa hatua ya kifusi barabara ile, lakini pindi ikinyesha mvua tu ile barabara inakuwa ni jipu, barabara haipitiki inakatika na ishakuwa kero ya muda mrefu sana kila mwaka wanatia kifusi wale watu. Kwa hiyo, ni lini barabara hii itajengwa kwa ngazi ya lami angalau tuone kwamba wale watu na wao wanafaidika na Mapinduzi ya mwaka 1964.

Pamoja na misaada mizuri sana ambayo inatoka kwa waheshimiwa viongozi wa jimbo lile hivi juzi tu, Mfuko wa Barabara ulikwenda kutembelea kule sijui nini hatima yake. Nini wanatwambia juu ya suala zima la ujenzi wa kiwango cha lami barabara ile ya Kinuni kwa sababu ni kiunganishi kizuri sana baina ya watu wa Magharibi na Mjini.

Sasa nitakwenda katika ukurasa wa 21 *ZMA*. *ZMA* ni taasisi nzuri sana na imeanzishwa vizuri kwa sheria za Zanzibar kuhusu masuala ya bahari na usalama wake wanaposajili. Katika kitabu cha Mhe. Waziri amezungumza kwamba *ZMA* imesajili meli tisa (9) za ndani na meli 87 za nje. Lakini sijaona meli hizi zote zimeiingizia Zanzibar kiasi gani. Naomba atapokuja Mhe. Waziri anijibu hilo swali langu halafu tuangalie na mengine.

Mhe. Naibu Spika, lakini vile vile *ZMA* bado hawana mashiko wameshindwa kujenga ofisi Pemba, kwa hiyo wana kilio cha ofisi huko Pemba na ni kilio cha muda mrefu sana. Mhe. Waziri sijui katika hilo atatwambia nini kwamba wale watu tuone nao wanafaidika na idara yao au taasisi yao ya *ZMA* kule Pemba kwa kuwa na ofisi, najua kiwanja kimeshapatikana Mkoani. Sijui lini utaanza ujenzi wa kiwanja kile na kuwa na ofisi Pemba.

Chengine zaidi hawa watu wanalalamika hawana wataalamu wa kutosha; wataalamu katika *ZMA* imekuwa jipu. Kwa hiyo, nafikiri kama taasisi ya mawasiliano ingeangaliwa kwa dhati kabisa kuweza kuwasaidia wataalamu. Kwa sababu kazi wanazozifanya ni kubwa na ni kazi ambazo za kuingizia pato hili katika nchi hii. Naona kwa maelezo hayo Mhe. Waziri kwa uongozi wake nina imani kwamba haya yote yataweza kukamilika na kuwa mambo mazuri.

Mhe. Naibu Spika, nitaingia katika suala zima la bandari. Bandari ni mlango mkuu kwa Zanzibar katika biashara na kila kitu, lakini bandari imekuwa kilio cha muda mrefu sana hata hawa wenzangu wote waliopita wamelalamika ufinyu wa bandari. Bandari yetu ina uwezo wa kuweka kontena zisizopungua 1,500 kwa vizuri kabisa, lakini sasa hivi kwa kukosea mna kontena zaidi ya

2,400 imekuwa tatizo, imekuwa sasa hivi kontena kutoka bandarini Zanzibar kwenda nje zinachukua muda mrefu sana kuliko kontena kutoka Dubai kuja Zanzibar. Kontena Dubai-Zanzibar linakuja *hardly two weeks* lakini kutoa kontena yako pale bandarini Zanzibar mzigo wako kuupeleka kwenye *godown* popote pale ikiwa Magomeni, Kwerekwe unachukua mwezi mzima. Tuangalie Mheshimiwa na hili tatizo limeshazungumzwa na wote waliochangia hapa kwamba nafasi ya kuweka *empty container* hawana.

Mhe. Naibu Spika, walikuwa wanaweka pale Bwawani ilikuwa ni msaada mkubwa sana kwa shirika lile, kazi inafanyika vizuri sana, lakini kwa utashi tu pengine tunataka maendeleo katika nchi yetu tumempa mwekezaji lile eneo na mwekezaji yule kama tunavyosema hajakuwa tayari bado. Sasa kama hajawa tayari basi wizara yake Mheshimiwa aliombe lile eneo ili kuweza kutatua tatizo la bandarini. Bandari sasa hivi imekuwa na mlolongo mkubwa sana wa kontena hivi sasa kuna meli zaidi ya sita nje ya bandari ya Zanzibar zinataka kuja kushusha kontena pale, imekuwa inachukua muda mwingi imepelekea mpaka baadhi ya mashirika ya meli kuongeza *Zanzibar Congestion Port Charges*, *surcharge* zimeongezeka kutokana na mlolongo wa kusubiri muda mrefu sana nje ya bandari ya Zanzibar, hili ni tatizo.

Kwa sababu inapoongezwa *charge* tayari *charge* ile inakwenda kumuumiza mtu wa chini kule. Kwa hiyo, kama watu wetu tunawapenda basi tungeliangalia hili suala *at list* hizi meli zichukue muda mdogo sana kukaa bandarini Zanzibar au ndani ili kuweza kupunguza hizi gharama ambazo si za msingi.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na hayo vile vile Shirika la Bandari kutaka kufanya kazi zake vizuri kupitia Mkurugenzi wake namsifu sana, Mkurugenzi wajina wangu anafanya kazi vizuri sana, lakini imefika hatua kutaka kusaidiwa tatizo hilo kwa nia safi kabisa kukodi chombo kile *reach stacker* kutoka Tanzania Bara. Namuomba Mhe. Waziri atapokuja anambie chombo kile kinalipiwa kiasi gani. Kwa sababu masharti yake moja kile chombo si zaidi ya masaa manane kwa siku, lakini vyombo vya kwetu sisi unaweza kukaa zaidi ya masaa 24. Chombo kile wenzetu wametukodisha lakini wametuwekea masharti kwamba kisiendeshwe zaidi ya masaa manane na kinalipwa kiasi gani kile chombo, tuangalie basi uiyano, ikiwa kama pesa nyingi kwa nini hatukati pua tukaunga wajihi, tukatoa pesa nyingi tukanunua chombo cha kwetu.

Najua tunaambiwa vyombo vinakuja, vinafika, lini vinakuja vyombo vile ni nyimbo ya muda mrefu sana. Tuliambiwa toka Disemba, Januari, sasa hivi tuko Juni vyombo vile vya kufanyia kazi pale bandarini *reach stacker* lini zitafika hapa Zanzibar. Kwa hiyo, nitaomba aje anisaidie katika hayo.

Jengine kuna malalamiko kwa hawa hawa bandari, kuna wafanyakazi ambao wanachukulia mishahara yao katika benki ya *NMB* wanashindwa kupewa mikopo wanaambiwa kwamba lazima wakachukue mikopo katika Benki ya *PBZ* ambayo wao hawana *account.* Hili ni tatizo imekuwaje, kwa sababu kama binadamu ana utashi wake mwenyewe wapi anapotaka kufungua *account* yake na pale ndipo penye haki ya kupewa mkopo. Lakini wale wote ambao wamefungua *account* zao katika Benki ya *NMB* hawapati mikopo kupitia benki ile kwa sababu Shirika la Bandari linaondoa dhamana zao. Naona hawawatendei haki wale watu atapokuja Mhe. Waziri naomba anisaidie hilo kulikoni.

Mhe. Naibu Spika, nitazungumzia suala jengine juu ya Shirika la Meli na Uwakala. Shirika letu hili lipo linafanya kazi vizuri, lakini kuna tozo napata wasi wasi, tozo ambalo linawatoa wafanyabiashara kupitia kontena zao, sijui kwa sheria gani wanatoa tozo lile mpaka sasa hivi umekuwa kila *document* pale inategemea mna kontena moja unatoleshwa shilingi 40,000 kila zikiwa nyingi inapanda ile *rate* mpaka ifike *ratio* ya shilingi 10,000 kontena zaidi ya kumi. Kwa sheria gani inayowapa watoze tozo hilo, kwa sababu wanawafanyia uwakala watu wenye meli sio wale wafanyabiashara wanaokwenda kununua mizigo yao nje ya nchi kuingia ndani kuleta Zanzibar. Nafikiri Mhe. Waziri amenifahamu, kwa sababu kama ni wakala wanawafanyia wakama meli zote zile za nje wanalipwa kuna *charges* wanapata. Je, inakuwaje watu au wafanyabiasha wetu wakalipe tena katika Shirika la Meli, kwa sheria gani iliyokuwepo. Nitamuomba Mhe. Waziri aje anisaidie hii sheria gani inayopelekea watu wa Shirika la Meli kuwa-*charge* wafanyabiashara wetu tozo la *release documentation*. Hilo nafikiri Mheshimiwa atakuja kunisaidia.

Mhe. Naibu Spika, mambo mengine ya Shirika la Meli *Alhamdulillah* kuzuri, mambo yanakwenda vizuri, meli yetu inafanya kazi vizuri naipongeza sana. Nitakwenda katika suala la nyumba.

Mhe. Naibu Spika, kama wenzangu walivyosema kwamba nyumba za maendeleo zimejengwa Michenzani, Kilimani, Kikwajuni kwa lengo safi kabisa, baada ya Mapinduzi ya 1964 tu kwa kuwasaidia Wazanzibari. Lakini toka kuanzishwa Shirika la Nyumba imekuwa maumivu kwa wananchi wetu, kodi ya nyumba imepanda kubwa sana kama alivyozungumza Makamu Mwenyekiti wa Kamati. Kodi imekuwa kubwa sana na vilio vimekuja sana kwa watu wetu kipato chao cha chini lakini kodi ya nyumba wanayotakiwa walipe sasa hivi shilingi 70,000 ni pesa nyingi sana ukilinganisha na kipato cha wazanzibari wanaoishi katika nyumba zile.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa umebakiwa na dakika nne.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Naibu Spika, ahsante. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri atapokuja atufafanulie vizuri juu ya suala zima la kodi ya nyumba za maendeleo za Kikwajuni kufika bei ya shilingi 70,000 ni pesa nyingi sana.

Vile vile nitazungumzia juu ya suala zima la beji**.** Hivi karibuni kuna changamoto ya beji ya waendesha magari na imefika muda sasa hivi wakienda kupasisha magari yao kule hawapasishiwi mpaka wajulikane wana beji za Mamlaka ya Mawasiliano, lakini beji zile zinatolewa na Manispaa. Sasa ni nani mwenye dhamana ya beji zile; ni Manispaa au Wizara ya Mawasiliano. Imekuwa tatizo imefikia mpaka gari hazipasishwi kama huna beji ya mawasiliano, lakini tayari hawa watu wana beji za Manispaa na wamekata kwa sheria hapo nyuma. Sasa kama kuna mabadiliko waelezwe wale watu wetu ili wasipate shida kwamba beji za Manispaa hazitambuliki tena zinatambulika beji za mawasiliano ili kuondosha utata uliopo sasa hivi. Imekuwa kilio hivi karibuni kimeanza juu ya suala zima la hizo beji. Kwa hivyo, nafikiri Mhe. Waziri vile vile atapokuja anisaidie sana katika suala hilo kwa sababu kama anavyojua gari zile zinawahudumia watu wetu wengi sana na wenye kumiliki gari zile ni wanyonge, kwa hiyo wanahangaishwa hawajui wapi wakamate.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na yote hayo nashukuru sana kunipa fursa hii, nathubutu kutamka kwamba naunga mkono hoja kwa asilimia kama 90 nyengine zaidi nitakuja kuunga baada ya kuridhishwa na majibu ya Mhe. Waziri. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe naomba tutambue wageni wetu waliotutembelea leo hapa ni wageni wa Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo; Mwakilishi wa Jimbo la Amani. Ni vijana wahamasishaji Jimbo la Amani, Shehia ya Kwa Wazee. Jumla yao ni wawili wanaongozwa na Ndugu Salmin Mussa Nahoda. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mgeni wetu wa pili ni mgeni wa Mhe. Nassor Salim Ali, Mwakilishi wa Kikwajuni ambaye ni Dkt. Abdalla Juma Mabodi. Karibu sana na vile vile ni Mbunge Mstaafu wa Jimbo la Rahaleo. Dokta Mabodi karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa tunaendelea sasa namwita Mhe. Shadya Mohamed Suleiman.

Mhe. Shadya Mohamed Suleiman: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana nami kwa kuweza kunipatia nafasi hii ya kuweza kuchangia katika Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

Mhe. Naibu Spika, awali ya yote kwanza naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa pumzi zake na uzima na asubuhi hii nikaweza kusimama katika Baraza lako tukufu nikiwa na afya njema.

Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu naomba kwanza mchango wangu niuelekeze katika pongezi. Naomba nichukue nafasi hii kwa dhati kabisa kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein kwa muono wake kwa kuona kwamba iko haja ya kuona na sisi tunapata meli yetu. Kwa hili tunamshukuru sana Mhe. Rais na tunamuombea kheri na mafanikio mema katika kazi zake za kipindi hiki cha miaka mitano.

Mhe. Naibu Spika, meli yetu hii ya MV. Mapinduzi II ni meli ya kileo, ya kisasa unaondoka katika Bandari ya Unguja saa mbili asubuhi Mwenyezi Mungu akipenda saa 6:30 umeshafika katika Bandari ya Mkoani, tunashukuru sana Mhe. Naibu Spika, sisi tunasema hii ni ndege yetu ya Baharini. Lakini Mhe. Naibu Spika, tunasema kwamba hakuna kizuri kilichokosa kasoro, nafikiri kwamba serikali iliamua kununua meli hii baada ya kuona matukio mbali mbali yaliokuwa yakitokea nyuma. Hatuombei hayo Mhe. Naibu Spika, lakini kidogo naiomba wizara iangalie suala hili kuhusiana na suala zima la meli yetu hii.

Mhe. Naibu Spika, meli yetu hii inatatizo la wakati wa kuteremka, msongamano unakuwa ni mkubwa sana kwa sababu ngazi ni moja na watu wote *first class*, wa kawaida wanateremka kwa wakati mmoja na tunamjua abiria akishafika sehemu safari yake akifika pale anataka awahi. Lakini pale sasa pana matatizo abiria wanakuwa wanasongamana vibaya sana. Kwa hiyo, pale panaweza kutokea tatizo jengine ambalo hatulitegemei. Kwa hiyo, naiomba wizara hii iliangalie kwa kina suala hili la mlango huu wa kutokea abiria.

Mhe. Naibu Spika, vile vile niipongeze wizara kwa kuona iko haja ya MV Maendeleo kufanya safari zake za kuelekea Tanga. Nilileta suala langu hapa kutaka kujua wizara ina mpango gani wa MV Maendeleo kuona inaenda Tanga kutokana na kwamba wananchi wengi wa kisiwa cha Pemba ni wafanyabiashara wanaokwenda kule Tanga kuchukuwa bidhaa zao na wengi walikuwa wanapoteza maisha yao na hata mali kutokana na vyombo

walivyokuwa wakitumia kama vile mashua na ngarawa vilikuwa si vyombo salama kwa maisha yao. Lakini niipongeze wizara kwa kuona hili na tunasema tunashukuru sana, ahsanteni sana kwa kuliona hili.

Mhe. Naibu Spika, juzi nilizungumzia suala zima la nyumba lakini nikaambiwa kwamba nyumba haiko kwenye wizara iliyopita juzi ya Mhe. Salama. Lakini kutokana na bajeti yake ile ilikuwa ya mwaka jana liliingizwa suala hili na mimi nikaona pale pale niingize mchango wangu. Lakini nikaambiwa kwamba liko huku. Kwa hiyo, nataka nimuulize Mhe. Waziri nyumba zile za Madungu au tuseme nyumba zote zile za Michenzani yaani Unguja na Pemba lakini mimi nitazungumzia sana kwa upande wa Pemba.

Mzee wetu Mwenyezi Mungu amrehemu huko akhera aliko, alijenga nyumba hizi kwa ajili ya wanyonge. Lakini jambo la kusikitisha hivi sasa nyumba zile zimepandishwa bei. Mimi kwa upande wa Pemba nitasema wanalipa shilingi elfu arubani na tano. Lakini kwa mwananchi wa Pemba ninaemfahamu mimi pesa hizi ni nyingi kwake yeye, ukimuangalia mwananchi huyu ni dhaifu hana ajira, anahangaika mwenyewe kutafuta maisha yake. Mwananchi huyu anatakiwa alipie maji, umeme na ana watoto na hatima yake aje alipie kodi hiyo.

Mimi ningeiomba wizara kama kweli ilikuwa inataka kufanya hivi tuombe basi kwa sababu nyumba zile mwananchi anaekaa katika nyumba ile anahudumia mwenyewe kutengeza ile nyumba na nyumba yenyewe ni mbovu Mhe. Naibu Spika, ukikaa ghorofa ya kwanza ukitwanga ile tangawizi chini madongo yanaanguka, inakuwa mtihani.

Sasa mwananchi yule anajipinda kwa unyonge wake anatengeneza nyumba ile kwa sababu yumo mle iimsitiri pamoja na watoto wake. Sasa leo anapandishiwa bei.

Tuiombe basi serikali ikiwa inataka kuwapandishia wale zile nyumba kwanza zile nyumba wazifanyie ukarabati mkubwa sana maana kama nilivyosema nyumba zile ni mbovu, ni huo unyonge tu watu wanakaa, ukienda kwenye sehemu za vyoo mubovu, sehemu za maji mbovu ilimradi tunasukuma siku uhai unakwenda.

Kwa hiyo, nimuombe Mhe. Waziri atakapokuja hapa anielezwe hawa wananchi wetu wanyonge waliopandishiwa kodi na wengine wamepewa nyumba hizi toka uhai wa Marehemu Mzee Abeid Aman Karume na leo wanaambiwa walipe amewafikiriaje. Namuomba Mhe. Waziri akija anieeleze hili.

Halafu Mhe. Naibu Spika, niende kwenye mchango wangu kwenye kero nzima kila anaekuja hapa Mwakilishi anaetoka Wilaya ya Chake Chake naona atalizungumzia suala hili la *stand*. Mhe. Waziri ukiona jambo hapa kila Mjumbe anaesimama analizungumzia limekuwa kero tena kubwa sana. Wananchi wa Wilaya ya Chake Chake tuna kero kubwa la *stand;* mji wetu umekuwa ovyo sasa hivi, magari yanasimama ovyo haijulikani wizara iko wapi utakuta magari pembeni wamewekwa na sasa hivi *alhamdulillah* wananchi wetu Mwenyezi Mungu amewajaalia kipato kila mtu ana gari yake. Kwa hiyo, hebu Mhe. Waziri nataka atueleze hili suala zima la ujenzi wa *stand* kwa Wilaya ya Chake Chake ni lini itajengwa *stand* hii. Ili mji wetu uwe na nuru uwe na sura nzuri ya kupendaza. Namuomba Mhe. Waziri akija anieleze hili suala la *stand* .

Halafu naomba nimuulize Mhe. Waziri kupitia ile sheria ya usafiri wa barabarani. Sheria ile Mhe. Waziri imefikia wapi kwa sababu sasa hivi ni wakati wake tukiangalia hasa nilivyokwambia tuna ukosefu wa *stand*. Kwa maana ile sheria ikifanyiwa kazi sasa hivi itaiingizia serikali mapato kama tunavyofahamu sasa hivi serikali yetu tuna uhaba wa mapato kutokana na hawa wananchi wajinga, wazembe ambao wakwepa kulipa kodi. Kwa maana hiyo sheria hiyo ikianza kazi sasa hivi itaingizia serikali mapato. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri akija anaieleze sheria ile imekwama wapi au kuna tatizo gani la kuweza kufanyakazi hivi sasa.

Nikitoka hapo naomba niingie kwenye barabara ya Ole- Kengeja. Mhe. Waziri tunaipongeza sana kwanza serikali yetu kwa kuona iko haja ya kutengeza barabra ile ya Ole - Kengeja tukiamini kwamba wananchi wengi asilimia kubwa ya wananchi wa kisiwa cha Pemba ni wakulima na wanasafirisha bidhaa zao kutoka sehemu hizo nilizozitaja kuelekea mjini kwa ajili ya kuweza kupata pesa kwa ajili ya maslahi ya maisha yao. Barabara ile toka ianzwe huu ni zaidi ya mwaka, naomba kujua Mhe. Waziri mwaka huu imefikiriwa barabara hii ya Ole- Kengeja?

Nikitoka hapo Mhe. Naibu Spika, naomba nizungumze suala kuhusu Mgelema. Mhe. Naibu Spika, waswahili wanasema "Mcheza kwao hutunzwa" na sisi tunaamini kwamba zao la karafuu ndio linalotupatia tija na linaloongoza serikali yetu. Japo sasa hivi kumetokea washenzi wachache wanaohujumu mikarafuu hii kwa kuikata ovyo. Nimuombe tu Mhe. Waziri anieleze karafuu nyingi kwa kisiwa cha Pemba zinatokea Mgelema na barabara ile ina muda mrefu sana wananchi wanasumbuka. Hebu atueleze Mhe. Waziri barabara ile ameifikiriaje nayo ili nao wananchi wa Mgelema kule wajisikie waone kwamba nguvu zao zinalipa baada ya kwisha chuma zao hili la karafuu na naamini

kwamba wakulima wale wa karufuu zile zinakwenda moja kwa moja *ZSTC* haziendi pahali pengine. Kwa hiyo, tunaomba Mhe. Waziri utakapokuja hapa pia unielekeze kuhusu Mgelema.

Nikitoka kwenye barabara ya Mgelema Mhe. Naibu Spika, nataka nizungumzie barabara ya Fuoni, ikiwa na mimi ni mmojawapo ninaepita njia ile. Mhe. Waziri njia ya Fuoni imekuwa ni mtihani huu ni mwaka mmoja tokea njia ile ianze kufanyiwa matengenezo, imekuwa ni kero kwa wananchi wetu wanasumbuka maradhi, lile vumvi peke yake Mhe. Waziri ni maradhi kwa wananchi wetu hususan wale wanaokaa nyumba za barabarani na wengine wameshindwa kufanya biashara zao pale na wakati tukiangalia biashara zile wananchi wale ndio zinazowapatia kipato cha kuendeshea maisha yao ya kila siku.

Tunaomba Mhe. Waziri utueleze barabara hii ya Fuoni kwa sababu sasa hivi tunapata habari nyingi kuhusiana na barabara hii kwamba mkandarasi huyu aliyepewa hii barabara tayari ameshakunja na hata lami yake kwa ajili ya kutengeneza barabara hii. Lakini kuna watu wakorofi wachache ambao wametaka iitishwe tenda wawatie watu wao ili wapate chochote na wao. Tunaomba Mhe. Waziri utueleze kwa kina kuhusiana na suala hili la barabara ya Fuoni na kuhusiana na huyu Mkandarasi aliyepewa kazi hii.

Baada ya hayo machache Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana na kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kusini Pemba naunga mkono bajeti hii kwa asilimia 95% na 5 yangu mwenyewe naweka mfukoni kwanza mpaka Mhe. Waziri atakapokuja kuniridhisha na majibu yake. Nakushukuru, ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Simai Mohammed Said: (Mpakabasi): Ahsante Mhe. Naibu Spika, dakika 15 au vipi?

Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi nianze kwa kuwapongeza Mhe. Waziri pamoja na Naibu Waziri na Katibu Mkuu na wote wahusika wa wizara hii kwa kazi nzuri an hotuba nzuri waliyoitayarisha kwa ajili ya kutuletea sisi hapa.

Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Tunguu na ningependa kutoa mawazo yangu lakini pia kuweza kuisadia serikali na pia kuihoji au kuishauri katika maeneo ambayo maoni yataweza kuisaidia.

La kwanza ningependa kuanza katika maeneo tafauti ni suala la Mji Mkongwe. Kwanza hili jengo la *Old Fort* nilitaka kujua kuna mpango gani maana kwa kweli lile jengo linatumika kwa mambo mengi linatumika kwa matamasha

haliko vizuri. Lakini pia nataka nizungumzie kuhusu masuala ya *traffic* ya magari yanayoingia na kutoka maeneo tafauti. Tuna tatizo la magari ambayo yanabeba wanafunzi na daladala ambayo yanakodiwa kipindi cha mchana na asubuhi, lakini daladala hizi tunakuwa hatuzijui kama zinabeba wanafunzi na zinahatarisha maisha ya watu.

Naomba kutoka serikali au waziri husika ni mpango gani amejipanga siku za mbele ili dereva njiani aweze kutambua kwamba wakati wa mchana hii ni daladala natakiwa niiheshimu barabarani. Lakini pia masuala ya *road speed limit* nimejaribu kuipitia sheria ya *road transport Act ya 2003*. Kwanza ningependa kujua *function* katika *section* namba 8....

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa hebu kaa chini kidogo, nna tangazo limekuja mbele yangu hapa.

Waheshimiwa Wajumbe mnatangaziwa kwamba katika kukamilisha mpango wa huduma ya Bima ya Afya kwa Wajumbe, leo tutakuwa na zoezi la ujazaji wa fomu kwa madhumuni hayo. Hivyo, tunaombwa Wajumbe wote; wawili wawili wawe wanakwenda kwenye zoezi hili kwa maafisa wa Bima hiyo ambao wapo juu kwenye chumba cha kamati namba mbili. Naomba sana watoke watu wawili wawili na isiwe kwamba wameondoka wote. Nawashukuru tuendelee Mheshimiwa.

Mhe. Simai Mohammed Said: (Mpakabasi): Ahsante Mhe. Naibu Spika, narudisha muda wangu kidogo nyuma.

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nazungumzia kuhusu *Road Transport Act ya 2003* nilikuwa nataka kujua kuhusu *section 8,* (b) na (d) kwamba:

(b) "To keep motor vehicles and drivers liscence registers in accordance with this Act"

(d) "To monitor drivers' and other road users' compliance with the safety and other regulations under this Act"

Lakini pia kwenye *section* ya 11 halafu nilikuwa nataja kujua pia kuhusu *Road Transport Board* ambayo ipo katika *section* 40 (1) na pia nilitaka kujua kuhusu kwenye *section* namba 82 (1) masuala ya pikipiki na watoto wanaondesha hizi pikipiki ambao ni *under age* na ni hatua gani ambazo wizara imeliona hasa hawa ni wanafunzi wanaoendesha. Pia naomba na *section* namba 83 ambayo

wanatoa leseni kwa ajili ya watu ambao hawajafika umri wa kuendesha chombo.

Pia nilitaka kujua kuhusu *section 119* watu ambao wanaendesha gari kidogo kidogo njiani wakati wanatumia simu ni hatua gani ambazo serikali inajipanga kuangalia, kwa sababu inahatarisha maisha ya watu. Pia *section 114* ambayo inazungumzia *speed limit*, pia na *section* 160.

Nikiendelea Mhe. Naibu Spika, katika *section* 183 kuhusu *sport penalty*, hii kanuni inatumika na hizi pesa zinakwendea wapi.

Sasa nikisonga mbele kidogo nataka nizungumzie suala la *fiber optic*. Mhe. Naibu Spika, serikali ya Mapinduzi Zanzibar imetumia dola milioni 18 kujenga *fiber optic* ambayo huu mkonge umetandikwa katika maeneo tafauti Unguja na Pemba ambao unatoka hapa unakwenda Dar-es-Saalam una *connect* na Mkonge wa Taifa unakwenda zake mpaka Tanga, Tanga unatoka unakwenda zake mpaka Wesha. Mwenye *responsible pass* na kutandika huu ni wizara, kwa sababu *infrastructure* na hii wizara imeingia mkataba na *Zantel* ambayo inaitwa *Zanzibar Terrestrial and Submarine Network* pamoja na *Zantel*.

Sasa hawa *Zantel* wanatumia huu mkonge kuweza kutoa huduma za Mtandao za *internet* katika maeneo tafauti. Lakini pia katika makubaliano baina ya wizara na serikali walikuwa wapeleke kitu kinachoitwa; *Last mile conectivity* katika wizara nafikiri zaidi ya 80 na taasisi na zake. Nataka kujua hadi hivi sasa hizi fedha ambazo *Zantel* anatumia juu ya huu mkonge wote kufaidika pamoja na huu mkataba tulioingia baina ya SMZ na hawa tumefikia wapi na kwa nini pesa hazingii.

Pia katika barabara inayojengwa kutoka Mwanakwerekwe kwenda Fuoni palitandikwa pale ile *fiber optic*. Nataka kufahamu hii wizara wakati inajenga barabara je, ile *fiber optic* bado ipo salama na kama imeharibika nani kaharibu na nani atalipa hizi pesa juu ya gharama ambazo umetengenezwa, hilo ni jambo la msingi. Kama tunajenga jambo basi liwe endelevu.

Nataka nizungumze kidogo suala la Shirika la Nyumba. Mhe. Naibu Spika, Shirika la Nyumba linachangamoto tumeona, ahsante Marehemu Mzee Abeid Aman Karume, ahsante Mzee Aboud Mjumbe na wengine wengi waliofuata. Lakini tunataka tuone ahsante ya Dkt. Ali Mohammed Shein Rais wetu. Mimi nashauri kwa upande mmoja kwenye Shirika la Nyumba, mbali na zile nyumba ambazo asilimia 35 ambazo serikali wanaziona katika Mji Mkongwe watafute njia mbadala ya kujenga nyumba, kwa mfano kwa nini wasitafute njia kuingia

mkataba na *ZSFF* au wakenda wakakopa pesa *ZSFF*, ili zile fedha wakazitumia kujenga hata katika Mji mpya katika maeneo ya Jimboni kwangu Tunguu na maeneo mengine sio tunakuja kutupiwa taka tu. Jimboni kwangu nataka nyumba mpya za bei nafuu zije kujengwa na inawezekana mkafanya hivyo. Lakini pia katika kubuni lazima hili shirika liendeshwe katika njia za kubuni, tuwe *creative*.

Wanaposema kama shirika linategemea fedha sijui kodi mpaka lini kodi za nyumba kodi yenyewe ndogo watu wamasikini serikali mishahara midogo lazima wajenge nyumba za kisasa watafute njia na kama huyo mtu hawezi atafutwe mtu ambae ataweza kufanya. Tuangalie mifano Dar es Salaam, yule *engineer* wa *National Housing* ameweza kufanya mangapi nyumba nyingi zinajengwa kwa ajili ya Polisi, Jeshi na *low cost housing.* Anajenga na inawezekana.

Lakini hata kwa mfano Magereza sasa hivi kiinua miguu lile eneo ni kubwa, lakini lile eneo la Magereza lipo mjini wanaweza pia wakatafuta njia kwa sababu Magereza yapo ndani na ile Kiinua miguu ipo ndani ya Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar tukawaondosha wale tukawapeleka maeneo mengine kama watakubali, tukawaridhisha na wao pia halafu pale tukajenga mji mpya. Hata siku za mbele majumba ya Mjerumani inabidi yatengenezwe yale, muwafanyie mpango muanze kuzungumza nao kwa miaka ya mbele majumba yanaharibika, majumba yataanguka. Majumba ambayo yamejengwa kwa historia ambayo ni mazuri kabisa.

Kwa hiyo, nashauri sana Shirika la Nyumba litafute njia ya kuingia mikopo, *ZSFF* waje na mipango maalum na 2020 hapa tuna nyumba ndogo ndogo za kisasa. Mimi sijawahi kuona pahala watu wanatafuta watu wajenge mji mpya waende wakajenge nyumba wenyewe, duniani kote haifanyiki hiyo. Nyumba zinajengwa zinakuwa sare zimependeza halafu watu wanauziwa au wanakodi. Kwa hiyo, hili shirika libadilike.

Sasa mimi pia nataka nizungumzie suala ambalo ni muhimu la Bandari. Mhe. Naibu Spika, Bandari yetu kwa kweli ina changamoto na hayo yote tumefeli kutokana na mipango. Mimi siwalaumu Bandari lakini huyu anaeishauri serikali hapa mipango mibovu ni nani. Mimi kwa kweli haiingi kichwani hapa Mhe. Waziri amekuja amesema anahitaji zaidi ya bilioni mia nne lakini ukiangalia haya makontena Mhe. Naibu Spika, yalioko nje na hizi meli, kuna meli sita na ya saba imefunga pale iko Gatini.

Katika hizo meli na ukifanya hesabu za kontena zote ambazo kutoka June 1 mpaka 14 ni kontena 2800 na katika 2800 mapato ambayo tuchukulie kila kontena moja kama inalipa serikalini milioni nne basi nakwambia mwezi huu tungeingiza bilioni 9.2 na hapo Dar- es Salam kuna makontena 10,000 yanatusubiri kuletwa hapa Zanzibar, ukichukuwa na hayo ya Dar es Salaam makontena yote unapata karibia nimefanya hesabu bilioni 13.2 kontena zote hizo na ukienda moja kwa moja mpaka tarehe 8/7/2016 hizi meli zilizokuwepo ndio zitamaliza kutolewa pale Bandarini na makosa sio ya Banadari; makosa ni mipango waliokuwa wanasimamia ndani ya serikali ni wanasiasa, watendaji ni mahodari wanafanyakazi kufa na kupona, ili sisi tuwe mbele. Inelekea kuwa watu hawawasilikilizi washauri wetu.

Huyo aliekuja na wazo kumpa eneo la Bwawani apewe Manji wakati sisi tunazungumzia leo kula yetu, makontena yako nje, leo tende zipo nje, nguo za siku kuu zipo nje tunawaambia nini wananchi. Yule mtu aliyefanya maamuzi haya alifeli anatakiwa tena ajiuzulu hasa kwa kweli. Hiki ni kisiwa haiwezekani kisiwa munategemea bandari leo meli zote zipo nje na huu msongamano umeanza Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri tangu Februari tarehe 1 ni miezi minne. Kama tutakwenda miezi miwili ijayo pale kaputi, *we are finish*! Kwa hivyo hakuna njia yoyote nyengine Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri nyinyi mungekaa kitako pamoja na hawa wafanyabiashara, hawa ambao wanaoitwa *shipping agencies* mukapanga na mukakubaliana nao kwamba mutarudi kwao. Katika eneo moja munatakiwa murudi kwao ni kuwaambia ni wakati gani mutafanya mpango wa kuyaondoa haya ma-*intake containers* kama Wajumbe walivyochangia hapa. (*Makofi*)

Hakuna njia nyengine, hatuhitaji *can*, tunataka ma-*containers* matupu yaondoke bandarini, tena kesho ikiwezekana. Kwa hivyo Mhe. Waziri atakapokuja hapa atwambie moja kwa moja wananchi wetu bei itapanda juu sasa hivi. *Container* moja imeshapandishwa *two feet* dola mia mbili na hamsini, *forty feet* ninafikiri dola mia tano kama sikosei. Sasa hizi pesa atalipa nani gharama hizi ni mwananchi. Tutaumia sisi na wananchi wetu. Mimi wananchi wangu ni maskini kule Tunguu. Nguo moja siku kuu anataka shilingi elfu tatu akipangiwa mia tano ni ghali. Watu wenyewe tunazaliana watu watano, sita, saba, nane, tisa haiwezekani. (*Makofi*)

Kwa hivyo vyovyote ikiwezekana lazima makontena matupu tunataka yaondoke bandarini. Kama hawezi kupeleka pale Malindi, wayapeleke Mnazi Mmoja potelea mbali lakini wananchi unafuu tuupate. Wamefanya *emergency plan* kwa ajili ya *cholera*, kwa nini bandari hawawezi kufanya maamuzi

magumu, yaende zake Mnazi Mmoja. Tunahitaji unafuu kwa ajili ya wananchi na serikali yote ipo hapa inatusikia. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na suala la *ZMA*. Mimi nikiungana na wenzangu; ninataka kujua haya mapato yanayopatikana hii *ZMA* kutoka huko Dubai kuhusiana na meli. Ninasikia tu inasajili meli ni kiasi gani tunapata, hatujui. Tuleteeni hizo hesabu mutuwekea kwenye vitabu ukurasa ule kule tupate kujua.

Mhe. Naibu Spika, kwenye ukurasa wake niliousoma wa Mhe. Waziri alizungumzia kuhusu changamoto alizokuwa nazo. Na katika moja ya changamoto alizungumzia kuhusu *Maritime labour Convention* ambayo ina *codes* tano. Lakini katika *code number five* ambayo inazungumzia *compliance and enforcement,* pamoja na *port states* na *flag states*

Na nilikuwa ninataka kujua hii katika *code number five* changamoto ipo wapi. Ni zaidi katika hizi meli baina ya Jamhuri na hizi *registered ships ZMA* au katika moja kwa moja kwenye huduma za kawaida. Lakini pia kwenye *code number four* pia, *healthy potential medical care* ningependa kufahamu zaidi.

Mhe. Naibu Spika, suala la barabara. Nilikua ninataka kufahamu pia ninatoa tahadhari kwenye barabara inayotoka Cheju kuja Kaebona, unapofika Kaebona tuna mpango sisi pia kule Mkoa wa Kusini kujenga soko kubwa katika maeneo yale kuunganisha watu wote. Naomba ile barabara atakapokuja aniambie mpango wa soko letu walifahamu katika ile *junction* pale siku za mbele. Lakini pia barabara ya Koani/Jumbi. Hii jamani mpaka ishe nayo Fuoni, haya mabarabara yanazungumzwa kila siku, tumalizeni basi kabla ya mwisho mwaka mambo yawe sawa. Vumbi linatosha, wananchi wa Mkoa wa Kusini wanaathirika vibaya sana na vumbi lile kutoka Mwanakwerekwe kwenda Fuoni. Na munapokuja kujenga barabara ya Fuoni kwenda Tunguu huu uzembe uliofanyika mara hii wa vumbi usije ukafanyika kule kwa wananchi, patakuwa hapakaliki hapa. Barabara ijengwe kwa mpango, tufanyeni mambo kwa mpango. Rais amezungumza kwenye ukurasa wake alipokuja amesema hii hasa *business as usual*, mambo haya tuyaache tuna-*fail* kwa mipango, siyo kama hatuna uwezo. Wataalamu wetu wanajipanga vizuri, wanasiasa, viongozi tuacheni mambo haya tujipangeni vizuri. Haiwezekani leo wataalamu hatuwasikilizi wanachokitaka, wana kazi, wamesoma wanaelewa. Ukiwauliza wanasema aah! hatujasikilizwa juu. Huku juu kuna nini?(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, basi barabara yetu mukija kutujengea kutoka Fuoni kwenda Tunguu, musije mukatuwekea vumbi kama hili, kuna wanafunzi wanasoma

kule, wanapita njia hiyo hiyo, hawatakiwi kuja kuathirika na mambo hayo. Lakini pia kwenye ukurasa wa 43 nimeona kuna suala la wanafunzi wanaokwenda kwenye wizara hii.

Mhe. Naibu Spika, wanawake mbona kidogo Mhe. Waziri. Mhe. Naibu Spika, wanawake waliosoma kwenye wizara yake katika mwaka huu ni kumi na nne, wanaume ni ishirini na nane. Ningependa kutoa tahadhari lazima kidogo wewe uwe ni mpiga debe mkubwa sana wa wanawake na mimi ninakuunga mkono. Hivyo tunaomba wanawake katika wizara wazidi kuendelea kusoma. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, lakini pia baada ya muda Mhe. Waziri kuna mpango kwamba magari yataanza kupelekwa Dar es Salaam kusafiri kutoka Zanzibar. Ningependa kufahamu bandarini munajipangaje katika suala zima la kuhakikisha kwamba yote yanakwenda kwa pamoja.

Sasa nirudi kidogo katika masuala ya Mjini na maeneo... Lakini kuna suala moja dogo nilitaka nilifahamu Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni na sheria za Kimataifa, kuna suala linaitwa *VGM* ambayo ni *Verified Gross Mass* ambayo ni hii *China solars.* Na ikifika siku kumi tarehe moja kutoka Julai inabidi bandari na serikali kwa ujumla ianze ku-*comply*. Na kuanzia *twenty feet containers to twenty eight tons* na *forty feet to forty tons* na *forty six feet to forty eight tons.*

Hili itabidi huyo afisa ninataka atangazwe kabisa ajulikane, ili angalau hizo karafuu zetu tutakapozisafirisha huko nje tuwe tupo tayari. Lakini nikirudi katika suala la barabara na nyumba kwa pamoja na hili suala nilizungumza la *ZANTEL* la mikataba. Haya matatizo yametokea mara nyingi sana hapa kwetu ya uzembe uzembe. Nini *fiber optic* Mhe. Waziri. Naomba sana utakapokuja uiangalie kwa undani ni kwa nini huu mkataba umeshindwa kuwa *implemented* mpaka leo. Hamuwezi kuwa munasema munahitaji fedha halafu fedha zipo tayari hamuzifuatilii.

Halafu pia ninataka kujua kuhusu ndege zinazotua baharini, hizi *amphibious*. Ni utaratibu gani ambao serikali imepanga kwenda mbele na kwa nini hili jambo hatalijafanyika toka hivi sasa. Kwa sababu tunafungua milango mingi na watu kutaka kufanya kazi Zanzibar panakuwa pagumu, haiwezekani kupata utaratibu. Ninataka utupe utaratibu *amphibious* zinaruhusiwa au haziruhusiwi. Kama haziruhusiwi ni kwa nini hizi ndege zinatua baharini, tatizo lipo wapi. Tunafungua milango sasa hivi.

Pia ninataka ajitayarishe Mhe. Waziri kuhusu *airport* ya Pemba. Pemba tunajipanga miaka ya mbele itakuwa ni *airport* nzuri...

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa umebakiza dakika tatu.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Ukiangalia kwa upande wa *Pemba airport* muanze kuyasifia yale maeneo yote ya ardhi ambayo *airport* imejipanga kwa miaka ya mbele. Isije baadae tukaishia pale pa fidia, tukawapa pesa wajenge katika mipaka ya *airport*. Tuhakikishe kwamba watu wetu hivi sasa *airport* linapimwa na linajulikana pia.

Sambamba na ushauri huo huo aanze kupanga maeneo ambayo *helicopter* zitaanza kutua. Na mimi pia ninataka kushauri Mhe. Waziri katika jimbo kwenye Kisiwa cha Uzi na ni matarajio yangu kwamba Rais wa Zanzibar atajenga Ikulu. Kwa hivyo ninatamani kwamba uhakikishe kabisa ile *whole plan* uanze kuitayarisha kule ili mpango wa kujengwa Ikulu kule uwe tayari na Rais atakapokuja kutembelea kwenye Kisiwa cha Uzi iwe tayari pamoja na Kisiwa cha Tumbatu, Kisiwa cha Misali na maeneo yote haya hizi ziwe zimepangwa tayari. Sio baadae tena hatujui *helicopters* zitakuwa zinatua wapi. Watu wanakwenda juu kwa sababu tunakwenda mbele hivi sasa.

Pia katika idadi ya wageni kutoka nje uliyotaja Mhe. Naibu Spika, katika *arrival* wako, umesema ni watu kama laki tatu na kadhaa, laki tatu elfu thamanini na sita, mia nne na kumi na nane. Lakini ukenda kwenye kitabu cha Hotuba ya Rais aliyotaja watalii waliongezeka ni watu laki mbili, ninafikiria kwa mwaka huu kwenye ukurasa wa kumi na tano, nitakuletea kwa maandishi. Lakini kwa nini kuna tofauti. Je, tofauti ni kutokana na hawa watu wanaoishi hapa. Tofauti ni kubwa. Tatizo la data ni ngumu. Ni umuhimu wa kuweka hizi taarifa jamani. Wageni wanaoingia ni wangapi. Unahesabu wageni waliokuja hapa kwa sababu walioingia wameingia katika *manifest* ya *international arrival*, wageni wanaoingia kwenye vile videge vidogo vidogo *of course* hatuwajui wangapi wanaotoka Arusha, wanaotoka Mafia, wanaotoka Dar Es Salaam, wanaingia wanapenya tu pale. Kwa hivyo tutumie *passenger manifest* tujue hasa, *foreigners* wanaingia Zanzibar ikiwa *for business or for pleasure* ni wangapi, tuwajue. Ili kuweka data kamili.

Suala la *airport* pia Mhe. Naibu Spika, ni umuhimu kwamba kila *airport* ni nzuri ya nchi. Tutafute kila utaratibu hii *immigration*, wanaoingia ndani, mtu akifika pale *immigration*, aah! *welcome to Zanzibar, good morning sir*, karibu

the weather is good, wawe na *smile*. Siyo jambo la mwanzo eeh! unatokea wapi, anaangalia pale. Haya mambo yaondoshwe, lazima hizi taratibu, elimu ilitolewe vya kutosha na yale majaa jaa taka taka nje kote ziondoshwe. Mtu akitua kwenye ndege anakuja Zanzibar anaanza kuona majaa pembeni, karatasi inayotoka nje. Haya mambo yote yaondoshwe.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa muda wako umekwisha.

Mhe. Simai Mohammed Said: Naam! Mhe. Naibu Spika, nipe dakika tatu.

Mhe. Naibu Spika: Muda wako umekwisha.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Basi ninamalizia.

Kwa kumalizia basi Mhe. Naibu Spika, mimi kwa upande wangu na kwa niaba ya wananchi wangu ninashukuru sana na mimi ninaunga mkono hoja asilimia 90, nitasubiri asilimia 10 Mhe. Waziri akija ku-*summarize*. Na ninampongeza sana kwa yote.

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi uliyonipa. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Simai. Mchangiaji anayefuata ni Mhe. Hassan Khamis Hafidh baadae atafuata Mhe. Shehe Hamad Mattar na baadae Mhe. Mwanaasha Khamis Juma.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipatia fursa hii ya kuwa mchangiaji katika wizara hii muhimu kwenye maendeleo ya Wazanzibari. Kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Welezo, kwanza ninapenda kuchukua fursa hii kumpongeza Komredi Balozi Ali Karume kwa kuchaguliwa kuwa Waziri wa Wizara hii muhimu, lakini halidhalika na Naibu Waziri wetu Komredi Mohamed kwa kuchaguliwa naye kuwa Naibu Waziri kwenye wizara hii. (*Makofi*)

Vile vile naomba kuchukua fursa kumpongeza Katibu Mkuu Komredi Mustafa Jumbe naye kwa kuchaguliwa kuwa Katibu Mkuu kuongoza wizara hii na Naibu Katibu Mkuu mwana-*DIASPORA* mwenzangu kuwa Naibu katika wizara na watendaji wote, akiwemo Mkurugenzi Uweje. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, sasa ninaanza kuchangia. Mhe. Naibu Spika, tarehe 24/04/2013 Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi

alialikwa katika Jimbo langu la Welezo kwenye Wadi ya Mtofaani. Katika mualiko huo alikuta jinsi gani barabara ilivyokuwa mbovu, jinsi gani wananchi wanavyopata shida, kwa sababu yeye mwenyewe ili aje ilibidi wakaitengeneze hiyo barabara *at least* aweze kuja. Kwa kweli hali ni mbaya na alisikitishwa na hiyo hali. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, katika risala ya wananchi wa Welezo Wadi wa Mtofaani kule Hawai wakamuomba Mhe. Rais kwa unyenyekevu, "Mhe. Rais tunakuomba hali ya barabara yetu umeiona, tunakuomba ututengezee". Mhe. Rais kwa vile yeye ndiye mkuu wa nchi hii na ndiyo Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliwakubalia ombi lile wakwezi wale na wakulima kuwatengenezea barabara yao.

Na Mhe. Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi akatoa agizo kwamba barabara hii naomba muitengeneze. Naomba kuwakumbusha watendaji wote wa serikali. *President's wish is other people's command*. Rais anaposema ni agizo, lazima litekelezwe. Sasa agizo lililotolewa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kuwatolea huduma bora wananchi wake wakwezi na wakulima, masikitiko yangu ni kwamba mpaka hii leo agizo lile la Mhe. Rais watendaji wake wamekataa kulitekeleza. Tangu tarehe 24/4/2013, watendaji hawa wamekaa kulitekeleza. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kizuri cha wananchi wangu walichokifanya baada ya miezi minne Rais kuagiza walitembelea maeneo chungu nzima yanayohusu watendaji na kuwakumbusha majukumu yao ya kutekeleza agizo lile. Waliyoyapata wananchi wangu ni maneno mengine yalikuwa ni kebehi na kejeli dhidi ya agizo la Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Naibu Spika, barua nyingi ziliandikwa, ngazi nyingi walipanda bali hakuna kilichofanyika mpaka asubuhi ya leo saa moja dakika ishirini nipo pale. Mhe. Naibu Spika, kwa hili linaniuma sana, limenisikitisha sana baada ya kuona agizo la Mhe. Rais wangu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi halijatekelezwa mpaka asubuhi ya leo. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, tunayo majina ya wale wote waliokwenda wananchi wangu kuwaambia watekeleze agizo hilo na kuwakebehi na barua mbali mbali zilizoandikwa, tayari nipo najitayarisha kuziandikia *covering letter* kuzipeleka kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kumshukuru kwa kutoa agizo, lakini kumuonesha jinsi gani wale watendaji wake wamekataa kutekeleza agizo lake la kimapinduzi.

Baada ya hatua hiyo ya leo, hatua ya pili ni kupeleka barua ya malalamiko, hatua ya tatu tutamuona Mhe. Rais popote hata Msikitini kumshukuru kwa kuwaonea huruma wananchi wake, lakini kumwambia uso na macho kwamba watendaji wake bado wamekataa kutekeleza agizo lake la kimapinduzi ambalo ni kuwahudumia wakwezi na wakulima. Hilo moja.

La pili Mhe. Naibu Spika, kuna Mfuko wa Barabara. Ndani ya Mfuko wa Barabara baadhi ya Wajumbe wa Mfuko wa Barabara muna wapinga maendeleo na wapinga mapinduzi. Namuomba Muhusika anayehusika na Mfuko huu wa Bodi wa Mfuko wa Barabara avae miwani kama havai miwani, avue miwani kama anavaa miwani, afanye *screening* aangalie *who is who*. (*Makofi*)

La tatu Mhe. Naibu Spika, naomba kumuuliza lini barabara ya Hawai aliyoagiza Mhe. Rais itajengwa kabla ya hatua nyengine kali kama mimi Mwakilishi wao walionituma sijazichukua. Na kwa nini Waziri aje kunijibu agizo la Mhe. Rais wa Zanzibar limekaa kwa muda miaka mitatu na nusu bila ya kutekelezwa. Lazima nijibiwe. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, *point* yangu nyengine hii Zanzibar ni nchi maskini. *Sources* zetu za *income* moja ni bandari. Ninarudia *sources* zetu za Zanzibar moja ni bandari ambayo wanaitumia wafanyabiashara. Wafanyabiashara wanalalamika, wamechoka, maneno yao yameshakuwa makali, wanaitukana serikali. Si vizuri, makontena yapo mengi pale bandarini. Nguo za siku kuu zimo nyingi mule, watoto wetu wanataka kuvaa.

Tafadhali mukakae mutwambie lini mutaondoshea kadhia hii wafanyabiashara ambao tunawahitaji wanaotuingizia pesa kununua madawa ya hospitali. Tusiwakere tumekuwa tunawakera. Wanaitukana serikali na wanaisema vibaya serikali na anayesababisha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kusemwa vibaya ni watendaji wa Mhe. Rais ambao ninahisi hawafanyi kazi yao vizuri. Ndiyo maana makontena yakawa mengi pale bandarini. Nahisi hawafanyi kazi zao vizuri ndiyo makontena yakawa mengi. Yanasababisha Mhe. Rais kusemwa vibaya, serikali yake inasemwa vibaya na wafanyabiashara. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, mimi ni Mwakilishi wa Jimbo la Welezo ninatokea Wilaya ya Magharibi "A". Masikitiko yangu makubwa ninamuomba Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri aje kunijibu, Wilaya ya Magharibi "A" na "B" ndiyo kunako watu wengi Zanzibar, lakini barabara zetu ndiyo mbovu kuliko watu wote duniani, wala serikali sifikirii kama inatambua hilo.

Kila siku nikipita mjini barabara za mjini zinajengwa. Sasa ninataka kuuliza hizi barabara za Wilaya ya Magharibi "A" na "B" zikiwemo za Welezo zitajengwa lini, au kule Wilaya ya Magharibi "A" na "B" ndiyo hakutakiwi na serikali, kwa nini jamani, kuna watu wengi kule kuliko pahali popote ndani ya Zanzibar. Wapiga kura wengi wapo Wilaya ya Magharibi "A" na "B", inaishi watu laki nne na ishirini elfu. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo lini serikali itaanza kutoa miundo mbinu, wananachi wa Wilaya ya Magharibi "A" na "B" wanazaa njiani, barabara kote hakuna. Lakini barabara za mjini zote ukenda zinatengenezwa, ukiambiwa unaambiwa ni Mfuko wa Barabara. Mfuko wa Barabara huu ni wa Serikali ya Mapinduzi na wananchi wanaoishi kule ni wananchi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ndiyo wenye jukumu. Kwa maana hiyo wana jukumu la kuzitengeneza zile barabara wananchi wanazaa njiani jamani haipendezi, barabara kule hakuna hata moja. Sasa hivi twende Wilaya ya Magharibi zote mbili "A" na "B", barabara kule hakuna. Kwa nini barabara za mjini ambazo huduma zipo karibu zinatengenezwa, kwa nini barabara za Welezo na Wilaya ya Magharibi "A" na "B" hazitengenezwi ambako kule huduma zipo mbali za kijamii kama hospitali. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, ndani ya wizara hii ndiyo kuna Idara ya Leseni na Usafirishaji. Madereva wanalalamika wa Zanzibar kwamba hawapewi maslahi mazuri, hawapewi vipando. Wengine wanawaendesha Mawaziri, wanaendesha Makatibu Wakuu, wanatumwa mpaka usiku, wanatumwa *week end* hawapewi maslahi, wanafanya kazi kwa sababu hawana nyengine tu, wamechoka. Ninaomba Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri hili alizingatie awape vipando, awape maslahi yao ipasavyo. Kama leo madereva wapo nje chungu nzima hapo. Leo ni Jumamosi, sisi humu tunapata posho, wao wanapata nini. Aje kunijibu. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, halikadhalika kuna barabara ya Fuoni na barabara ya *Mkapa road*. Mhe. Naibu Spika, barabara ya Fuoni inajengwa. Mhe. Naibu Waziri hapa alisema anajenga barabara bora akatumia neno moja la Kiingereza tutakuwa *viewer current the way*. *Nice and good.* Lakini Mhe. Naibu Spika, hakuna barabara bora duniani kama haina mipindo na mikato ya kusimama gari za abiria na mpaka hii leo naiona barabara ya Fuoni pakusimama gari ya abiria hakuna. Ndani ya barabara yangu ya *Mkapa Road* kila siku ya Mwenyezi Mungu kuna ajali, na barabara ya *Mkapa Road* imejengwa juzi, kwa sababu ajali zinasababishwa na kukosa mipindo zile *cutting road* za kuonesha daladala isimame wapi na vituo, ajali zimekuwa nyingi, wenye daladala wanatuuwa siku zote.

Kwa hivyo, kama barabara ya Fuoni haina mipindo ya kusimama daladala na gari za abira, itakuwa hii sio barabara bora, itakuwa tumetumia pesa za wavuja jasho, wakwezi na wakulima kujengea barabara iliyokuwa sio bora. Natoa tahadhari, kwa sababu barabara hii itatusababisha ajali kila siku. Naomba kuuliza barabara hii hasa itakwisha lini kwa sababu inazuwia wananchi wanyonge kufanya biashara zao mule pembezoni mwa barabara.

Mhe. Naibu Spika, mipindo mingapi au zile *cutting* ngapi za kusimama daladala zitakuwepo katika barabara hii, naomba kujibiwa. Barabara yangu ya *Mkapa Road* Mhe. Naibu Spika, inasababisha ajali, naomba warudishwe Wakandarasi waliojenga barabara ile, ile sio barabara bora na walioipokea barabara ile kwamba barabara hii imekamilika, walifanya makosa,kwa sababu sio barabara bora inajulikana barabara ile inachukua wananchi wengi na kuna usafiri wa daladala lakini hakuna mipindo ya kusimama daladaka.

Mhe. Naibu Spika, juzi kauliwa mtoto mbele yangu, daladala imesimama mtoto kaja kachungulia kaona yuko *safe* kakata kumbe gari inakuja tu, kwa sababu hakuna mpindo. Kwa hivyo, barabara ya *Mkapa Road* sio barabara, kwa sababu haina mipindo, haina viwango na wananchi wamelipa pesa nyingi sana kujengewa barabara ile ambayo sio bora. Naomba hilo.

Mhe. Naibu Spika, jengine zamani kulikuwa kuna Shirika la Mabasi hapa, mimi nilikuwa Rahaleo nasoma, tunapanda mabasi yale ya rangi kama maziwa. Mhe. Naibu Spika, naomba Shirika la Mabasi lirudishwe tumechoka wananchi kuuliwa na wenye daladala, na Shirika la Mabasi likirudishwa basi vitiwe vituo, hakuna nchi duniani gari ya abiria inaambiwa ningoje akangoja, hakuna duniani, sijapata kuona mimi hiyo iko Zanzibar peke yake, abiria anaiita gari. Wakati inatakiwa abiria aifuate gari kituoni, na hii inasababishwa na kwamba hakuna vituo. Mwenye daladala anasimama popote kwa kufuata abiria wa shilingi 300 na hatimaye anasababisha ajali kila siku.

Naomba Shirika la Mabasi lirudishwe, mabasi Zanzibari hayazidi 30, tumechoka kuuliwa na wenye daladala na matibabu yenyewe hakuna. Shirika la Mabasi lirudi ili litowe huduma kwa wananchi, huduma bora na vituo vya daladala Zanzibar virudi.

Naomba tena wizara hii imchukulie hatua dereva yeyote wa daladala atakayesimama pasi na kituo, basi afutiwe leseni na asiendeshe gari tena nchi hii, kwa sababu atakuwa anatuuwa sisi wakwezi na wakulima, ajali zimekuwa nyingi.

Mhe. Naibu Spika, jengine kila Mkurugenzi aliyekuja pale Manispaa kaja na wazo lake, wengine Darajani pale zilikua zinasimama daladala zile zimeondoshwa na zimeletwa Michenzani. Mhe. Naibu Spika, kadhia ile imekuwa kubwa pale ni afisi Kuu ya Chama Tawala, pamekuwa pana shida, pana vurugu kwa sababu tumekosa *National Car Parking.* Naiomba sana wizara hii ifanye utafiti tena kwa haraka, iangalie wapi kadhia ile iipelekwe, pale Afisi Kuu iondoke inatuudhi, tukitaka kwenda kwenye mikutano yetu pale hatuingii kwa raha, pana wizi na pana mambo chungu nzima, ambapo dunia nzima Chama cha Mapinduzi imebakia chama kimoja tu chama tawala, pale iondoke, halafu iangalie utaratibu wa kujenga hiyo *National Car Parking* hapo Mwembeladu yasiwe maneno tu. Wazungu wanasema, *actions speak lauder then words, is time now to act,* tufanye kweli tupeleke kituo cha daladala kiwe pale, *National Car Parking* Zanzibar hatuna, magari yanakwenda kusimama pale, shida na tabu pakupita hakuna.

Juzi *ambulance* imekaa pale kwa muda wa dakika 21 niliihesabu, polisi anatafuta tu itapitaje, mgonjwa angeweza kufa kwa muda wa dakika 21, ile haiwezekani Mhe. Naibu Spika, umefika wakati nchi hii ya kimapinduzi...

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, malizia muda wako umekwisha.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Tunapoongea mambo ya kimapinduzi haya kuwastiri na kuwatolea huduma bora wakwezi na wakulima, lazima tu-*act* wakati umefika, wazee wetu walipoamua kufanya mapinduzi waliamua na waliyafanya kweli na sisi hapa leo tuko salama na tunaishi salama.

Kwa hivyo, naomba sana na nitaendelea kuwakumbusha mawaziri na watendaji wote ambao mmepewa kazi ya kuwahudumia wananchi basi wafanye majukumu yao ipasavyo, kama si hivyo basi sisi watoto wa wakwezi na wakulima tutakuja hapa tutawasema milele daima. Tutawakumbusha majukumu yao wayafanye ili huduma bora kwa wakwezi na wakulima zipatikane. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache naomba sana niliyoyasema nije nijibiwe, naomba kuunga mkono hotubaya wizara hii kwa asilimia 90, asilimia 10 nina-*reserve* mpaka nipate majibu yaliyokuwa sahihi yanayoweza kutekelezeka. Baada ya hayo machache naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Hassan Khamis Hafidh, mchangiaji anayefuata ni Mhe. Shehe Hamad Mattar, baadae atakuja Mhe. Mwanaasha Khamis Juma, baadae ajitayarishe Dkt. Makame Ali Ussi.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi nitowe mchango wangu katika Wizara hii ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji. Kwanza sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uhai na afya, baada ya hapo nije kwenye mchango wangu moja kwa moja kuhusu jambo ambalo limetawala hapa Barazani la kuhusu barabara.

Mhe. Naibu Spika, nianze na hapa tulipo Unguja, mchango wangu niliangalia katika barabara inayotokea Kiwanja cha Ndege siku za mvua. Barabara hii iliwahi kutengenezwa huko nyuma kwa matatizo ya mkondo wa maji, lakini naona tatizo lile bado lipo. Kwa hivyo, naiomba sana Wizara hii ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji iangalie tena ni jinsi gani ya kuweza kuiboresha barabara hii ambayo inatoka katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa, sehemu ambayo wageni wengi wanafika hapa, watalii wetu ambao wanaingiza pato la taifa wanapita hapa, leo mtu anatoka ndani ya ndege akifika nje anakuta mkondo wa maji, vipi mambo haya. Namuomba Mhe. Waziri aliangalie sana pamoja na watendaji wake kuifanyia ukarabati tena barabara hii ya kutoka Uwanja wa Ndege mpaka Kiembesamaki.

Mhe. Naibu Spika, niende katika jimbo langu sasa. Nimeona katika kitabu hiki imeoneshwa kwamba Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji imejenga barabara ya kifusi kutoka Pandani hadi Mlindo. Kwa hili nawapongeza sana ni kilomita 2.6 zimejengwa, kwa kweli pahala pale palikua ni pabaya sana, vijana wanaotoka shule pia na wazazi ilikuwa ni vigumu kufika barabara kuu, lakini kwa sasa maeneo haya yanapitika vizuri kwa barabara hii.

Kwa hivyo naiomba sana serikali kwa kupitia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, barabara hii iendelee hasa ukizingatia eneo hili halina mwinuko mkubwa hivyo hili fusi linaweza likadumu kwa muda mrefu na baadae kuwekwa lami. Kwa sababu hiyo mbele ya barabara hii kutoka pale Mlindo iendelee kupita katika kijiji cha Kivuugo halafu ifikie mpaka Wingwi ambapo inakutana na barabara kuu ya *COJIFA*. Lengo la kupita barabara hii itaondoa ule usumbufu ambao mara nyingi sana nimekua nikidai hapa kwamba mbele yake kwenye kijiji cha Kivuugo kuna bonde ambalo linausumbufu sana, watoto wetu wanapata shida wakati wa kwenda shule na wazee ambao nguvu zao ni ndogo, basi wakati wa mvua kubwa wanalazimika kutumia masafa marefu kitu ambacho inawezekana kutekeleza pale kwa kuweka daraja.

Kwa hivyo, naomba sana serikali iliangalie hili na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji iende kuliangalia eneo hili na wataona kwamba ni kweli kuna haja ya jambo hili. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, tushirikiane katika kulitengeneza daraja pale. Hilo ni kwa upande wa barabara ya Mlindo.

Mhe. Naibu Spika, pia niiombe serikali kwa kupitia wizara hii kuna barabara ambayo ni muhimu sana ni njia ambayo inaunganisha Finya na Wete, njia hii inaweza kutumika kwa dharura, ikiwa kutatokezea tatizo lolote pale Kiungoni, na ikawa barabara kumetokea jambo haiwezi kupitika, basi barabara hii inaweza kutumika kwa kupitia Kizimbani Kwale mpaka Finya. Lakini sasa eneo hili ni miaka mingi sana hawana umeme wala barabara. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri, katika mipango yake barabara hii iangaliwe hawa kwa njia ya fusi kwa hatua ya kwanza.

Jengine nichangie katika barabara ya hapa Malindi. Mhe. Naibu Spika, nimekuwa nikiangalia msongamano wa magari katika barabara ya Malindi kuelekea Bandarini, Msongamano ni mkubwa sana. Kwa hivyo, naomba sana tuangalie uwezekano wa kutengeneza barabara inayotoka bandarini kupitia soko la samaki la Malindi hadi kutokeza kule kwa Simbachai Malindi, ili wanapotoka kule waweze kutoka badala ya kuja kusongamano katika barabara hii inayotokea Malindi Polisi pale. Naomba sana tuliangalie suala hili, huo ni mchango wangu.

Mhe. Naibu Spika, niende katika sehemu ya usimamizi wa usafiri wa barabra. Mhe. Naibu Spika, katika wilaya zangu mbili hizi, maana imechanganyika Wilaya ya Wete na Wilaya ya Micheweni; barabara inayotoka Wete kuelekea Micheweni, tunaita njia kongwe.

Barabara hii zamani ilikuwa ni mbovu sana, lakini kwa kupitia Serikali ya Mapinduzi ya Zanizibar katika jitihada zake za kuwaondolea matatizo wananchi barabara hii sasa inapitika vizuri sana. Kabla ya hapo ilikuwa magari ya abiria ni shida kupatikana, hayaonekani, unaweza kulala mpaka ukaamka siku ya pili basi gari haijafika, hata viongozi walikuwa hawapiti, lakini sasa barabara hii inapitika.

Mhe. Naibu Spika, nauli zilikuwa juu kwa sababu wenye magari ya abiria walikuwa wakisema kwamba barabara ni mbovu. Lakini leo barabara inapitika, kwa hivyo tunaomba sana kuna kilio cha wananchi unatoka Wete kuelekea Finya tu pale unaambiwa shilingi 1,000 wakati barabara nzima ina maili 12 mpaka Micheweni. Suala hili la bei liangaliwe sana, mtu alipe kulingana na masafa aliyokwenda. Lakini leo anayekwenda Micheweni, anayekwenda Finya, anayekwenda Kinazini analipa shilingi 1,000, Taifu halikadhalika, kwa nini iwe hivyo. Ukiangalia barabara inayotoka Wete kuelekea Chake Chake inaunafuu sana, wakati ni mbali zaidi, lakini barabara hii madereva wanafanya wanavyotaka.

Suala hili nilishalizungumza kwa kupitia wakuu wa magari kule Pemba, lakini sijaona hatua iliyochukuliwa. Kwa hivyo, naomba sana serikali kwa kupitia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji iliangalie suala hili.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu usalama barabarani. Barabara zetu zinatumika vibaya hasa kwa vijana wetu, na madereva wale ambao kuwa hawataki kufuata taratibu za sheria ya barabarani. Vijana wanakwenda ovyo, wewe hata kama uwe ni dereva vipi unakwenda kwa usalama basi unakuja kumkuta kijana amekupita hata upande sio. Naomba sana katika suala lile la usalama barabarani linalofanywa na wenzetu kule Tanzania Bara basi na wao hapa walianzishe kwa makusudi, siku ya usalama barabarani ili wananchi wafahamishwe jinsi ya kutumia barabara zetu, barabara zetu ni pana lakini tunazitumia vibaya.

Pia suala hilo hilo la barabara Mhe. Naibu Spika, serikali imejenga barabara kwa ajili ya watu wanaopita kwenda na kurudi, lakini barabara zetu zinakuwa ni maegesho ya magari, ile barabara inakuwa yote inabanika haiwezi kupitika kwa nafasi, na wakati mwengine inaweza kusababisha ajali. Suala hili Mhe. Waziri kwa kupitia wizara yako hii naomba sana wenye magari watafute pa kulaza magari yao na sio kwenye barabara, barabara itumike kwa ajili ya kwenda na kurudi tu.

Mhe. Naibu Spika, nije katika programu ya miundombinu bandari na usimamizi wa usafiri baharini. Bahari ni sehemu kubwa ambayo tunaitumia wanadamu, lakini pia ni kaburi kubwa la binadamu linalotuchukua kwa wingi sana. Kuwepo na mfumo maalum wa mawasiliano, kila chombo ambacho kiko baharini awe ni mvuvi wa samaki, awe ni msafirishaji wa abiria basi kuwe na mfumo wa mawasiliano anapopata matatizo basi kuwe na kitengo ambacho ataweza kueleza taarifa zile aweze kupata huduma kwa mara moja na kunusuru maisha yake au maisha watu aliokuwa nao pale. Tukifanya hivyo tutaweza kuisaidia bahari katika kutunusuru na kufa ovyo ovyo.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye hiyo bandari kuhusu meli ya MV Mapinduzi II, kwa makusudi mazima Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ilifanya jitihada ya kuondoa tatizo hili la usafiri baharini tukapata meli ya MV Mapinduzi II. Lakini kitabu hiki cha hotuba kinatueleza kwamba meli inasafari ya kwenda Unguja na Pemba, lakini Dar es Salaam imetajwa, lakini sijui ni mara ngapi kwa mwezi inakwenda, kama meli hii itakwenda basi itachukua sehemu kubwa ya abiria na mizigo, kitu ambacho kitaweza kutuingizia mapato katika Shirika hilo na kwa taifa kwa jumla.

Sijui wamepangaje katika suala hili kwa vitendo, maana sio kwa maandishi tu. Nina wasi wasi kwamba hii safari ya Dar es Salaam kama inakwenda kama walivyosema humu. Namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa hebu atuthibitishie kwamba meli yetu hii inakwenda mpaka Dar es Salaam, kweli?

Mhe. Naibu Spika, kuhusu meli hiyo hiyo ya MV Mapinduzi II, meli yetu hii ilitangaziwa na humu inaonesha kwamba inabeba mizigo. Suala hili wajumbe wenzangu wangi wamesema kuhusu ubebaji wa mizigo bado ni tatizo. Kwa suala la mizigo harakati za maisha zilivyo sasa hivi basi meli hii ingeweza kuingiza fedha nyingi sana kama kusafirisha magari na mizigo mingine.

Leo inashindwa hata kwenda kupakia karafuu zetu kule Pemba, ikiwa inataka kwenda kupakia karafuu kule Pemba basi inakuwa ni kazi kubwa sana na hulazimika hata kutumia meli za binafsi wakati mwengine. Kwa nini iwe hivyo chombo chetu hiki ambacho kimetugharimu sana tusikitumie. Kwa hivyo, mfumo huu uliotengenezwa meli hii ya kwamba mzigo una matatizo ilikuaje. Kwa taarifa niliz

opata kwamba meli hii kwanza wataalamu walikuja wakapima mawimbi ya bahari yetu ya Nungwi, wakaangalia bandari zetu, leo inakuaje meli mpaka leo inafika unaambiwa kwamba haiwezi kuchukua magari, na ni nadra sana kupakia gari.

Kwa hivyo, naomba uwepo uwezekano wa meli hii iweze kuchukua magari kwa wingi na mizingo mingine kwa usalama, lakini pindipo itafanyiwa marekebisho mengine. Naomba sana wizara iangalie ni hatua gani itaweza kuchukua ili kuboresha meli hii na iweze kubeba mizigo kama ilivyokusudiwa. Ukiangalia sasa hivi hapa MV Maendeleo ambayo ni ndogo basi imefanya kazi kubwa sana kulingana na muundo wake.

Kwa hivyo, meli yetu hii tunaipenda ni nzuri sana, lakini mapato hayapatikani ipasavyo. Leongo la kuanzisha meli hii ni kutoa huduma, lakini baada ya muda iweze kununua meli nyengine. Lakini kwa mtindo huu hatutaweza kuipata meli mpaka itakufa kama ilivyokufa Mapinduzi II.

Mhe. Naibu Spika, ukiangalia hapa takwimu za msigo, mzigo uliochukuliwa kwenye Maendeleo ni mkubwa sana kuliko MV Mapinduzi kwa muda huo huo. Tofauti ni tani 2,626 ni mzigo mkubwa sana huo, kwa nini isiweze kufanya kazi hiyo. Naomba sana wizara iliangalie suala hili kama ni kuboresha meli au kutengeneza bandari zetu ili meli iweze kuchukua mzigo.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye meli ya MV Ukombozi, meli hii kwa taarifa ziliopo ni kwamba imekodishwa, lakini imekodishwa kwa nani, kitabu hiki hakikuonesha kwamba imekodishwa kwa nani. Lakini pia naomba niulize kwa nini serikali ikaamua kuikodisha, wakati sisi tunaweza kuifanyia kazi kwenda kuchukua mzigo tukapeleka na fedha zile zikaingia, kuliko kuikodisha. Mhe. Waziri atakapokuja aniambie kwa mwaka inaagiza kiasi gani meli hii, katika hiyo hatua ya ukodishwaji.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye Shirika la Bandari, shirika hili limetajwa humu katika hotuba ya Mhe. Waziri kwamba anafanya matengenezo makubwa katika gati ya Wete. Je, mradi huu umemaliza, maana humu haikuoneshwa. Kwa hivyo, naomba sana atakapokuja Mhe. Waziri aniambie kama matengenezo yamemaliza au bado yapo asilimia ngapi. Lakini ninashauri kwa ninavyojua bandari ya Wete, mimi huu mpango wa kutengeneza gati hii isingekuwepo ingalijengwa, ijengwe gati nyengine mpya. Kwa sababu hata kitakwimu utakuta Mkoa wa Kaskazini Pemba ndio wenye idadi kubwa ya watu, huko Mkoani basi kama wataamuwa watu wa Kaskazini hawendi ile bandari itakuwa haina watu. Ni vyema sana Serikali ikaliangalia suala hili la kujenga gati ya Wete, sio kutengeneza gari, uwepo mpango makusudi wa maendeleo wa kutengeneza gati hii itaweza kupiga hatua kubwa sana katika kutoa huduma kwa wananchi lakini na mapato yataongezeka kupitia bandari ile.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye programu ya utawala na uendeshaji. Nawapongeza Wizara ya Mawasiliano kwa kuona katika kitabu hiki wametoa nafasi ya kwenda kuwajengea uwezo wale wafanyakazi wake wapatao hamsinina mbili, wakiwemo humu muna Wahandisi, lakini sasa ninapata mashaka Wahandisi hawa wanakwenda kusoma kuisaidia Serikali au kuja kujisaidia wenyewe kwa mishahara? Kwa sababu barabara zetu zimejengwa kuna Wahandisi lakini leo nashangaa barabara tunazisifia hapa nzuri pana, lakini mimi napita barabara hizo tayari hazijakabidhiwa zimeshaanza kupasuka, ilikuwaje? Wahandisi hawa hawakuwepo, kitu gani kilichosababisha, hebu mimi naomba Mhe. Waziri, utakapokuja kupitia na Wahandisi wako nipate sababu halisi kwa nini barabara zile zimekufa muda mfupi kabisa, barabara iliyojengwa na KOJIFA tokea miaka 90 iliweza kufika miaka kumi haijatokezea athari, lakini barabara leo iliyojengwa mwaka 2012 inakabidhiwa mwaka 2014 tayari imeanza mipasuko, na hii iliyomaliza juzi nayo ni hali kadhalika, hivyo sikuhadithiwa nimeiona mwenyewe.

Mhe. Naibu Spika, niende katika masuala ya bandari hii ya Mpigaduru. Katika hotuba hii Mhe. Naibu Spika, imeonesha kwamba imetumia kuna shilingi

374,400,000 zimepatikana katika Wizara hii na katika hotuba yake inaonesha kwamba kuna ujenzi wa bandari ya Mpigaduru, mbona mimi sijaona kujengwa bandari hii au zimetumika vipi fedha hizi; inawezekana pengine sijaona lakini atakapokuja Mhe. Waziri, hapa anieleze na alieleze Baraza lako hapa kuona kwamba Bandari ya Mpigaduru imejengwa vipi.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu usimamizi wa miundombinu na mawasiliano. Mhe. Naibu Spika, naomba Waziri alifahamishe Baraza lako pamoja na mimi mwenyewe kuhusu mkonge wa mawasiliano. Wakati wa uunganishaji wa umeme kutoka Tanga tuliambiwa umeme ule ndani yake mna waya wa mawasiliano ambao kuwa utaondosha usumbufu wa *Internet* kule kisiwani Pemba. Lakini nataka nijuwe je, waya huu umeshaanza kutumika kwa hayo mawasiliano yaliyokusudiwa. Kwa sababu leo ikifika tarehe 24 au 25 wakati wa mishahara huwezi ukenda ukapata fedha, siku tatu mfanyakazi anatokea Konde anakwenda Chake Chake anakuta hapati mshahara wake anaambiwa *network* hamna, sasa hili tatizo ni nini, mawasiliano haya vipi, tunahakikisha vipi wananchi kwamba mkonge huu tunaweza kuutumia ili kuondosha lile tatizo ambalo kuwa linatufika siku nyingi. Naomba sana Mhe. Waziri, utakapokuja tulione kwamba jambo hili utaweza kunisaidia kuona kwamba na wananchi wanasikia tatizo ni kitu gani kuona kwamba mawasiliano haya ya *Internet* hayapatikani ipasavyo.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu Shirika la Bandari la Zanzibar hapa Unguja kwenyewe, namalizia hapa Mhe. Naibu Spika. Pale pana wafanyakazi makundi mawili kundi A na kundi C. Lakini katika wafanyakazi hawa wengi wao ni hawa wana umri usiopunguwa miaka ishirini na bado ni *daily paid* na wafanyakazi hawa ndio wale waliowekwa katika zile sehemu za hatarishi, tena wengine ni vizee kwenye makontena, lakini kilio chao ni kikubwa sana, wafanyakazi hawa malipo yao ni kidogo, hawana *overtime*, ni rahisi kupata matatizo, vitendea kazi wanajitafutia wenyewe, inafika mtu wakati wa mvua hata ule mwemvuli huku anakamata *paper* huku atafute pahali pa kukaa yeye mwenyewe, hata *raincoat* tu, yaani vifaa vya kujikinga hawana, tatizo hili aliitwa Mhe. Rais na yeye akaanza kuunda Tume, lakini wenyewe wanasema kwamba bado hakuna kilichotekelezwa.

Naomba sana Mhe. Waziri, uwaangalie wafanyakazi hawa, leo wanafika hadi kustaafu hawana huduma za matibabu, hawana bima, watu hawa ndio wale ambao kuwa wanaifanya bandari izalishe fedha kwa wingi, lakini kundi A ndio lile linalobakia ofisini wakizunguka na kiti, uwajali wafanyakazi wetu hawa ambao kuwa ndio watenda kazi. Mhe. Waziri, naomba sana uliangalie hili.

Mhe. Naibu Spika, mwisho mimi sina zaidi isipokuwa nasema kwamba kwa upande wa Serikali Wizara hii majukumu ni mengi, lakini bajeti yake ni ndogo. Kwa hivyo, ninaiomba sana Serikali katika kutekeleza majukumu yake ipasavyo Wizara hii naiomba Wizara hii ipewe fedha zake kama ilivyoomba kwenye kitabu hiki kwenye bajeti yake, naomba sana sana.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kwa niaba ya Jimbo langu la Mgogoni naiunga mkono hotuba hii mia juu ya mia, lakini Waziri aje atoe maelezo kwa mule nilimotaka atoe maelezo ili wananchi waelewe nini kinachofanyika. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Shehe Mattar, mchangiaji wetu anayefuata ni Mhe.Mwanaasha, baada ya Mhe. Mwanaasha, nimemtaja Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi na baada ya Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi, anafuata Mhe. Hamad Abdalla Rashid Gerey yupo? Kwa maana hiyo atafuata Mhe. Omar Seif Abeid.

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi hii niwezekuchangia hotuba ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaali uzima na afya kusimama hapa ndani ya chombo hichi cha wananchi. Lakini mimi nilitaka nigusie katika ukurasa wa 28, Progaramu ya Miundombinu na Huduma za Usafiri wa Barabara. Wachangiaji wengi wamegusia masuala mazima ya barabara, lakini Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na mimi nataka nizugumzie suala zima la barabara ambalo linaathiri kazi na shughuli zote ndani ya Jimbo langu la Chukwani.

Mhe. Naibu Spika, programu hii ni nzuri, ni mzuri kwa sababu imepangika kimaandishi na ni nzuri kwa sababu watendaji wa Mhe. Waziri na Naibu Waziri, tayari wamebaini vitu vingi ambavyo vinahusu programu hii katika nchi yetu au maeneo mbali mbali. Lakini nije katika suala hili la barabara kwa upande wa Jimbo la Chukwani. Jimbo la Chukwani tayari kuna barabara ambazo zina makero mengi na katika masuali yangu Mhe. Waziri, alinijibu na kunijibu yake mimi nazungumzia barabara ya Kisauni kwendea Shakani. Majibu aliyonipa barabara ile tayari ina utanuzi wa Uwanja wa Ndege, sawa nimekubaliana nae lakini bado ile barabara wananchi wa Jimbo la Chukwani wakiwemo watu wa Shakani barabara ile wanaitumia na kipindi kikubwa kibwa hivi sasa tumekubaliana kuwa ni ujenzi wa Uwanja wa Ndege lakini bado wananchi ile njia wanaitumia au barabara ile inatumika.

Mhe. Naibu Spika, namuomba sana sana sana Mhe. Waziri, atakapokuja hapa aniambie ni lini Wizara yake ichukuwe hatua za makusudi. Wananchi wale sio kama lazima wanataka ile barabara itiwe lami, lakini ile barabara ni mbaya ni mbaya sana kutoka Kisauni kwendea Shakani kwa Mohammed Hijja, ile barabara ni mbaya na inawapa usumbufu mkubwa sana wakaazi wa eneo lile, kuna waja wazito ambao muda wao ukifika wanataka kwenda hospitali, kule hakuna mashimo kuna mahandaki, naomba sana sana Mhe. Waziri, namuomba sana kama itawezekana na kama hajapitia eneo lile apite aone kadhia ile ya njia inayowasumbua sana watu wa eneo la Jimbo la Chukwani wakiwemo Shakani, namuomba akija anieleze ni hatua gani ambazo watazifanya kwa makusudi mazima kuona kwamba njia ile inapitika, hawahitaji lami kwa sababu tayari kuna ujenzi wa Uwanja wa Ndege nimelikubali hilo, lakini naomba Mhe. Waziri, aje hapa anieleze suala zima la barabara ile.

Mhe. Naibu Spika, na kwa sababu tu, tayari njia ile ni kubwa na watu wanasafiria au wanaenda, watu matajiri wenye daladala zao hawataki kuwapelekea huduma wananchi wa kule kutokana na ubovu wa njia ile. Kwa hiyo, ninamuomba sana Mhe. Waziri, afanye kwa makusudi mazima ikiwezekana hata kesho tuifanyie kazi barabara ile ili wananchi wa eneo lile na wao wajione wako katika nchi yao na wanapata huduma ya usafirishaji au huduma ya barabara ile kwa urahisi na kuwaondoshea kadhia ile.

Mhe. Naibu Spika, lakini jengine nakuja tena bado kwenye hii barabara. Jimbo la Chukwani bado kuna barabara ilitolewa ahadi na Mhe. Rais. Mhe. Rais, alitoa ahadi njia ya barabara ya Chukwani/Buyu kutoka ilipomalizikia ujenzi wa lami pale, barabara ya lami kuanzia Tawi la Chukwani kwendea Buyu pwani na ile Mhe. Rais wa Awamu ya Sita alikuwa Mhe. Amani Karume aliahidi ndani ya wiki mbili katika kipindi chake barabara ile itatengenezwa kwa kiwango cha lami pale palipobaki, mpaka hii leo miaka ni mingi sana.

Kwa hiyo, namuomba sana Mhe. Waziri, akija anieleze vizuri kuhusu barabara ile. Lakini katika masuali niliyowauliza walinambia tayari barabara ile iko katika mashirikiano au Waziri wa Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Vikosi Maalum, basi nilikuwa nawaomba kwa vile hii ni ahadi ya Rais washirikiane Wizara zote mbili tulitatue tatizo lile ili kuwajengea imani wananchi wa Jimbo la Chukwani ikiwemo Buyu wajenge imani kwa nchi yao na yule Rais ambaye aliyepita aliyetoa tamko lile la kuwa barabara ile itajengwa kwa wiki mbili, lakini hivi sasa ni miaka mingi, namuomba sana Mhe. Waziri na Waziri wa Idara Maalum kama walivyonijibu washirikiane kwa pamoja tuone tunatua changamoto lile ndani ya Jimbo la Chukwani.

Mhe. Naibu Spika, bado ninarudi tena katika suala zima la mawasiliano. Kwa vile Serikali iliamua kufanya upanuzi wa kiwanja cha ndege na upanuzi huu wa Uwanja wa Ndege waathirika wakubwa ni watu wa Jimbo la Chukwani pamoja na Kiembesamaki. Namuomba Mhe. Waziri, atakapokuja kufanya majumuisho anieleze ni wananchi wangapi wa maeneo hayo mpaka sasa wamelipwa fidia na wangapi mpaka sasa bado hawajalipwa na kama wako ambao hawajalipwa ni sababu zipi zilizofanya hata watu hawa wasilipwe fidia katika maeneo yale ambayo wametaka kufanyiwa upanuzi wa Uwanja wa Ndege. Najuwa Serikali ilikuwa na nia nzuri tu na wananchi nina imani ziliundwa Kamati mbali mbali, walishajihishwa na wamelikubali hili, lakini bado kadhia hii ya kuwa malipo yao bado hayajafanyika, imani inawatoka wananchi wa majimbo haya. Kwa hiyo, ninamuomba Mhe. Waziri, aje anieleze ni wananchi wangapi ambao hawajalipwa na kama wapo ambao wamelipwa pia ni idadi yao ngapi na kama bado hawajalipwa kuna tatizo gani ambalo limesababishwa wananchi hawa wasilipwe.

Mhe. Naibu Spika, jengine bado niko katika Jimbo la Chukwani kwa sababu linanihusu sana na mimi ndiye mwakilishi wao na wamenituma nije niwawakilishe. Kuna Chuo cha Sayansi *Marine* ndani ya Jimbo la Chukwani na ule ujenzi unaendelea. Lakini hawa Wanachuo cha Sayansi *Marine* ambao wamejitolea kule kujenga chuo kile, Mhe. Naibu Spika, waliomba ruhusa kupitia Wizara hii kuwa waruhusiwe kufanya matengenezo ya barabara zile za ndani kuunganisha Buyu - Shakani kiwanda cha makuta, lakini mpaka sasa bado ruhusa ile hawajapewa. Namuomba Mhe. Waziri, aje aniambie ni sababu gani ambazo zimefanya wanachuo hawa kuwa hawajapewa ruhusa ambayo ya kuunganisha barabara ya Buyu kwendea Shakani kiwanda cha makuta. Na wakiwapa ruhusa hii, tayari hawa wale wananchi wa Jimbo la Chukwani ambao wanataka kufika Shakani au wa Shakani wakitaka kufika Chukwani tayari pale patakuwa pana urahisi wa wao kupita katika maeneo yale.

Kwa hiyo, namuomba sana Mhe. Waziri, atakapokuja aniambie ni sababu gani ambazo zimesababisha kuwa ruhusa hiyo haijatolewa na pia nataka Mhe. Waziri, aje aniambie ni lini mimi na yeye tuongozane ili tuone kama kuna taratibu zozote za ile njia au kitu chochote ambacho kinasababisha ruhusa ile isitolewe kwa hawa wanachuo ambao wamejitolea kwa moyo mzuri tu, tuone kuna tatizo gani ili lipatiwe ufumbuzi na ruhusa hii waitoe kwa kuwanufaisha wananchi wa Jimbo la Chukwani halikadhalika na watu wengine.

Mhe. Naibu Spika, lakini chengine pia naomba Mhe. Waziri, aje anipe ufafanuzi kuhusu kampuni ya *DP* Sharpiya juu ya madai ya wafanyakazi wa hiyo Kampuni. Mhe. Naibu Spika, wafanyakazi wa Kampuni hii wanalalamika

hii miezi tisa mpaka leo hawajapewa mafao yao yoyote na wafanyakazi hawa wanapoifata hii Kampuni, madai yao wanasema Wizara wanaidai, kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri, aje anipe ukweli au anitolee ufafanuzi juu ya suala zima la Kampuni hii kama kuna ukweli madai hayo yapo na kama yapo aniambie, lakini pia awaangalie hawa wafanyakazi, kwa sababu wafanyakazi hawa ni Wazanzibari ambao walikuwa wakiifanyia hii Kampuni kazi, lakini pia bado mafao yao hawajalipwa. Namuomba sana sana Mhe. Waziri, aje anipe ukweli kuhusu Kampuni hii na kadhia inayowapata wafanyakazi hawa.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilikuwa na hayo ya kuchangia, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Chukwani tunaunga mkono hotuba hii ya Makadirio ya Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Usafirishaji, kwa asilimia 100, lakini akija akiniletea ufafanuzi mzuri wa masuala yangu ambayo nimeyawasilisha hapa kwake basi nitamuongezea baada ya mia itakuwa mia na kumi. Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Mwanaasha, mchangiaji wetu anayefuata sasa hivi ni Dkt. Makame Ali Ussi, baada ya Dkt. Makame Ali Ussi, atafuata Mhe. Omar Seif Abeid na ajitayarishe Mhe. Hamadi Abdalla Rashid Gerey.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi na mimi niwe mmoja katika wachangiaji wa hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji. Kwa kweli hotuba hii ni nzuri, niseme kweli kabisa hii hotuba ni nzuri ingawa kuna mapungufu ya hapa na pale, mapungufu haya yameshaelezwa na wengi katika wachangiaji, nadhani Waheshimiwa viongozi wakuu wa wizara hii hawajawa na muda mkubwa kwa sababu ni karibuni tu wameteuliwa, hawakuwa na muda mkubwa wa kuyatatua haya, kwa hivyo, hatuwalaumu sana kutokana na matatizo hayo ambayo yameelezwa. Kwa hivyo, nianze kwa kusema kwamba, mimi ninaiunga mkono hii hoja ya Mhe. Waziri au Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, kwa asilimia mia.

Sasa niingie kwenye Jimbo langu la Mtopepo kwanza kabla sijasema haya mengine niliyotaka kuyachangia. Jimbo la Mtopepo ni jimbo ambalo lina mabonde, miteremko na ni jimbo ambalo linapakana na msitu wa Masingini. Kwa hivyo, tegemea kwamba inaponyesha mvua jimbo lile linapata mvua kubwa sana na mteremko wa maji katika hali ya ardhi ile unakuwa ni wa kasi kabisa kabisa. Naweza kusema kwa kipindi cha miaka 5 huduma za jimbo lile zilikuwa hazikutosheleza. Barabara pamoja na kwamba zimehudumiwa hazikutosheleza kabisa kwa sababu ni mbaya mno.

Hivyo hivyo nigusie ingawa ni Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira inahusika lakini na hata miundombinu ya maji basi kuna wachache wale waliokuwa wanapinga pinga walithubutu kuiharibu ili wapate kutumia visima. Yaani niseme tu kwamba maji imekuwa kama ni siasa katika jimbo litu. Kwa hivyo, ninaiomba sana serikali nzima kwa sababu lazima tushirikiane sote kule kuna magonjwa ya Kipindupindu tumeyaona, kule kuna hali ya njia mbaya tumeziona, kule kuna matatizo ya *dispensary* kuwa hakuna, yaani kuna matatizo yote yale ya jamii. Hata hii barabara ya Mkapa ambayo mwenzangu hapa jirani yangu Hassan aliieleza, barabara ile mimi nasema barabara si mbaya, barabara ni nzuri sana na bidii kubwa imefanyika kuitengeneza barabara ile, lakini imekosa matunzo na huduma zile zinazotakiwa na mambo kama hayo aliyoyataja, hamna *parking*, hamna pahala pa kuegesha magari ili abiria waweze kupanda, hilo ni tatizo.

Halafu hakuna hata *speed limit,* madereva utawakuta siku hizi za kukimbilia kufutari, mimi nakuwepo sana kule wakati huo wanakwenda kwa *speed* kubwa sana wanataka wawahi kwenda kunywa uji. Sasa anaona ende mbio kubwa awahi uji kuliko maisha ya watu ambao na wao wana haraka ya kukimbilia wanakata njia. Kwa hivyo, kwa kweli ile barabara inahitaji iangaliwe ziwekwe *speed limit* kwenye barabara ile kama kuna haja ya kuwekwa matuta iekwe matuta ili *speed* zile zipunguwe. Kwa kweli ajali ni nyingi katika barabara ile.

Sasa barabara zetu za ndani nazo ni mbaya sana. Kuna muekezaji alichimba shimo kule kwa ajili ya kuchimba mchanga, sheria inamtaka anayechimba mchanga aihuishe ile ardhi kwa kuipanda miti lakini aliiacha vile vile. Sasa wakati wa jua kali linakauka, lakini inaponyesha mvua ni maafa makubwa. Mle mmechimbwa choo, pamejengwa pale, sasa yale maji ya mafuriko yanayotoka kwenye choo yote yanateremka chini kunakuwa na mito kwenye hizo njia ambazo ndio tunazisema zinazojengwa kwa kifusi zinaendelea kuharibika na maji mengi yanakuja zake mpaka mtaro ule wa chini ule wa barabara ya Mkapa pale Garagara yanakuja maji kwa kasi pale, yale mawe yaliyowekwa pale sasa hivi kama hapajachukuliwa hatua kubwa yakamalizwa na barabara ile ikajengwa vile inavyotakiwa, yale ikija mvua kwa ninavyoijua hali yatakwenda na maji yote yale yatabururwa.

Eneo la Mtopepo kwa kweli hasa pale Garagara si mahala pa kujaa maji yakafurika kwenye majumba ya watu wakahama kama miundombinu ni mizuri. Kwa hivyo, sasa ushauri wangu ni kwamba tulishughulikieni Jimbo la Mtopepo, Waheshimiwa Mawaziri wale wasiokuwa na Wizara maalum, Waheshimiwa Mawaziri wa Wizara mbali mbali twendeni Mtopepo tukalisaidie Jimbo liweze kutatua huduma. Barabara za ndani zinatumiwa na

wajawazito, zinatumiwa na wagonjwa, watu wenye ulemavu na kadhalika, lakini hazipitiki, hizo gari hazendi, hata daladala kule hakuna wamegoma kwenda wenye daladala kwa sababu hakuna njia seuze hizo gari za watu binafsi ambazo haziwezi kupita. Sasa mgonjwa lazima abebwe, ni kweli wazazi wengine wanazalia njiani. Kwa hivyo, tunaomba sana tuihudumie barabara ile.

Jengine ninaloliomba kwa watendaji wa hii wizara, watu wanapokwenda na matatizo kuwaomba wawasaidie, kumpa mtu *alternative* ende pahala pengine ile si lugha nzuri, ni bora tu umwambie tutakupatia au mwambie halipo bovu au chochote kile. Lakini ukimwambia bora nenda mahala fulani na yeye anajua mahala fulani lile lipo lakini kaona huku kutakuwa na nafuu zaidi, akipata maneno ambayo hayaridhishi kwa kweli inakuwa haifurahishi. Nawaomba sana tuwahudumie wananchi kwa yale mambo ambayo wanataka na tuwape lugha nzuri pale ambapo hatuwezi kuwahudumia.

Naingia kwenye bajeti, kuna programu kuu ya pili kuhusu miundombinu ya bandari na viwanja vya ndege. Hapa katika bajeti imeelezwa kwamba kwenye *programme* ndogo ya kwanza kwenye *page* ya 8, imeelezwa kwamba ziliidhinishwa, yaani wizara au hii sehemu ilipangiwa kutumia bilioni 151.5, lakini ikapata bilioni 1.7. Sasa sijui hapa kuna tatizo gani. Tatizo ni bajeti au tatizo ni nini. Nadhani kwa hali hii ya *allocation* ya fedha ya aina hii nadhani hatuwezi kufika popote. Asilimia 1 ndio inayopatikana, yaani hata kama mtendaji mzuri wa namna gani sidhani kama ataweza kufanya lolote. Kwa hivyo, mimi naomba tuangalie kuna bajeti waliokuwa wameipanga na wameomba haikukubaliwa kwa sababu ya fedha wakaidhinishiwa, wakatakiwa watumie kiasi fulani, lakini hata hivyo hakikupatikana, kwa hivyo, hili ni tatizo. Na hivyo hivyo katika *sections* nyengine zote hizi ni *less than fifty* hazikupata fedha ambazo zinatakiwa, hii kwa kweli inakwamisha maendeleo.

Nikiendelea kwenye ukurasa wa 17, kifungu cha 54, kinasema kwamba;

> "Katika mwaka wa fedha 2016/2017 Mamlaka inatarajiwa kukusanya...."Mamlaka ya Viwanja"...inakusudiwa kukusanya na kutumia jumla ya bilioni tisa laki saba na tisiini elfu".

Sasa inakusanya na kutumia, sasa hapa imeweza kutumia bilioni nane laki saba, kidogo mimi inanipa shaka neno 'kukusanya', kukusanya ni *probability,* yaani wewe unataka kukusanya mapato, wewe kweli ushajua nitakusanya hapa na hapa lakini *probability;* inaweza ikapungua na inaweza isipungue. Sasa kusema kwamba utakusanya kiasi hiki na kuweza kutumia kiasi fulani, hapa kidogo mimi naona kuna tatizo la kimahesabu. Nadhani ni vizuri isemwe tu kwamba

tutakusanya kiasi fulani lakini na matumizi kutokana na hivyo yatakuwa ni kiasi fulani. Lakini kukusanya ni kama kwamba utapewa kiasi hicho na utatumia kiasi hiki ambacho nitakupa. Nadhani hapa nimeeleweka.

Baada ya kumaliza kwenye bajeti hii sasa niingie moja kwa moja kwenye mambo ya mawasiliano hususan usafirishaji. Sasa nianze kwenye anga kwa sababu kuna usafirishaji wa anga, njia ya barabara, njia ya baharini na kadhalika. Sasa nianze kwenye anga, tuangalie sana kuna ndege hizi ndogo ndogo kwa kweli nyengine ni chakavu mno, zinakwenda hewani huko, yale mawimbi ya upepo yanavyokupigeni unakiona kindege kile kinakaribia kuanguka kabisa na hata ule mngurumo unahisi hasa, chote kinatetemeka, unahisi hasa kwamba hiki kindege si madhubuti. Nadhani ni vizuri kuangalia ile ndege ambayo haiko kwenye kiwango kwa nini tusiitoe na tukaziruhusu zile ndege tu ambazo ziko kwenye kiwango kwa ajili ya usalama wa wananchi wetu.

Sasa usafiri wa barabarani, wenzangu wengi wamechangia sana, wamechangia kuhusu kuwepo kwa mahala maalum pa kuegeshea magari, wamechangia kuhusu kuwepo kwa mabango haya ya *speed limit*, na mimi nawaunga mkono lazima barabara zetu ziwe na mabango ya kuonesha *speed limit*, mwahala mwa ku-*park* na ikiwezekana basi tuwapangie *time-table*, mfano gari namba fulani linaingia na litasimama mahala fulani kwa muda dakika tano, likisha linaingia gari namba fulani litasimama kwa muda tano. Huo ndio mfumo wenzetu wanavyofanya magari utayakuta yana-*flow* hayakai pale kwa muda wote na wala hayasimami ovyo ovyo kila mahala, akisimamishwa tu dereva anasimama. Au dereva mwenyewe anaamua tu huyu anakwenda kwa miguu labda anataka kusafiri anakwenda kumsimamishia gari mbele pale. Kwa hivyo, utaratibu uwe kila gari iende kwenye *stand* yake na pale ndio abiria wapande.

Kwa hivyo, ninasisitiza sana mambo ya mabango haya kila ukipita utakuta bango la *Tigo* na matangazo mengine, *advertisement*, sasa yale maandishi ya kusema kama hapa tunaelekea Bumbwini, hapa tunaelekea wapi, mabango yale hakuna. Nadhani yangekuwepo mabango yale pia yangewasaidia hata watalii kwa sababu si mara zote mtalii anatembea na hawa mapapasi, wakati mwengine anaweza kuamua anatembea mwenyewe akipita barabarani anajua bango lile pale linanionesha mimi nakwenda mahala fulani. Bango hili hapa linaonesha ninakwenda mahala fulani. Mabango haya nadhani ni vizuri yawepo. Na kwa sababu ya barabara zetu chache, nadhani kuna haja ya kuanza kutayarisha zile *pedestrian bridge* ni zile njia za watu za kuvuka kwa juu, yaani gari zinapita chini na watu wanapita juu hasa upande wa Darajani pale panapokuwa na msukumano wa watu pakijengwa *pedestrian bridge* moja watu

wakawa wanavuka magari yanapita chini ni usalama mzuri pia kwa watu. Huo ni kwa upande wa barabara.

Sasa usafiri wa baharini, jamani hapa tumeshuhudia maafa mengi, watu wengi wamekufa, Mnazimmoja pale kulikuwa kuna maiti nyingi sana waliokufa kwa kuzama kwa meli. Ninachotaka kusema hapa tuangalieni sana, zile Sheria za usalama wa baharini zifanyike, tuwe na maboya hata haya madau, mitumbwi ya watu binafsi hawa nao wapatiwe maboya ili wanapozama waweze kuwa na kitu cha kuwaokoa.

Halafu mawasiliano kwa simu nayo nasema mitandao tuiangalie sana, simu inachangia umaskini kwa wale watu waliokua hawana kipato. Kwa sababu mtu ukimgaia elfu moja anakwenda kununua simu, anakubali akae na njaa. *Charges* wanazozitoa ni kubwa ziangaliwe, waelezwe hawa kwamba *charges* hizi wazipunguze kwa faida ya wananchi. Na hii minara inayojengwa pia iangaliwe kwa sababu minara mingine iko chini ya nyumba za watu, iangaliwe kama ina madhara ifanyiwe utafiti. Kama ina madhara basi hatua zichukuliwe ili madhara haya yasiwepo, lakini kama haina madhara pia wananchi wajulishwe, lakini tusije tukangoja mpaka watu wanaugua kutokana na mionzi inayotokana na pale halafu ndio tukaanza kushtuka. Bora tufanye utafiti wa kutosha ili tuweze kujikinga na maafa yanayoweza kutokea.

Nasema haraka haraka kwenye nyumba, kwa kweli nyumba zetu zichakuwa chakavu ni muda mrefu zimejengwa zinataka *maintenance* za hali ya juu. Kwa sababu nyumba hizi kwa wenzetu wanaziwekea viwango maalum, miaka 50 libomolewe lijengwe jengine, lakini sisi hatuna uwezo huo. Basi hizi *maintenance* zifanyiwe, lisiachiwe jumba likapasuka, pale lilipopasuka lirekebishwe palipofanya ufa parekebishwe. Siku moja mimi niko Kilimani pale kwenye jumba ile *canopy* kilianguka pale watu wote tulianza kufukuzana, kilitoka kwenye ghorofa ya juu kikaanguka, kikavunja chini kikenda chini pale. Kwa hivyo, nadhani majumba haya tuyaangalie kwa kina, tuyatunze vizuri ili yasije yakaleta maafa makubwa baadae.

Namalizia bandari, bandari jamani kuna bandari bubu, kuna na bandari hizi. Naomba bandari hizi ndogo ndogo hususan bandari ya Mkokotoni tuiimarishe isaidie hii bandari, kwa sababu bandari hii hapa *congestion* ni kubwa, Unguja nzima kuna bandari moja tu. Sasa tukiimarisha ile bandari ya Mkokotoni pale tunaweza tukapata kitu ambacho kitasaidia sana *congestion* ya hapa Malindi.

Baada ya kusema hayo nadhani muda ndio hauniruhusu, naomba kusema tena kwamba naunga mkono hoja hii ya Mhe. Waziri, ni hoja nzuri na sote ninakuombeni tuikubali kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Naibu Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia takakutana hapa leo tukiwa wazima wa afya. Pia, nachukua fursa hii kukupongeza na kukushukuru wewe kwa kunipa na mimi nafasi ya kuchangia katika wizara hii muhimu ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

Mhe. Naibu Spika, kama tunavyojua kwamba wizara hii ni moja katika wizara muhimu sana na ni wizara ambayo ni tegemeo na ni miongoni mwa wizara mama za serikali. Sina budi kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kumteua Balozi Ali Abeid Karume kuwa ni Waziri wa Wizara hii. Lakini pia nampongeza tena kwa kumteua Katibu Mkuu, watu hawa wawili waliopewa wizara hii wana kila sababu ya kujivunia Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na kuwa na sisi sote tuna haki ya kujivunia Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964. Mwenyezi Mungu amlipe na amlaze mahala pema kiongozi wetu huyu mahala pema peponi, *Amin,* kwa ushupavu wake alioufanya kwa kuona kwamba iko haja sasa ya Wafrika wazalendo kupata nchi hii.

Ni imani yangu kwamba viongozi waliokabidhiwa dhamana ya wizara hii watatekeleza yale yalioachwa na viongozi wazee wetu waliotangulia na mimi sitaki nipoteze muda sana, nataka nijikite moja kwa moja kwenye masuala yenyewe.

Mhe. Naibu Spika, kila anayelia husema mama yangu, hasemi mama yetu, pamoja na kuwa sote tuko mama mmoja, baba mmoja lakini ukifika msiba kila mtu hulilia mama yake. Mimi nalilia wananchi wangu walionituma wakanipa kura kuja kuwawakilisha kilio kikubwa cha barabara iliyopo Konde/Msuka na Konde/Makangale kutoka Kiuyu Kwamanda, barabara hii ya Konde/Msuka ina urefu wa kilomita 4.3 na barabara ya Makangale ina urefu wa kilomita 6.

Sasa Mheshimiwa, nina kila sababu ya kuelekeza kilio changu huko, kwa sababu barabara ya Msuka, barabara hii tulianza kupata ufadhili kutoka serikali ya Japan tukaweza kuitekeleza kwa kiwango cha kifusi mwaka 2013. Lakini barabara hii kwa sasa inaendelea kuharibika siku hadi siku na kwa bahati sijaona katika barabara ambazo watazifanyia matengenezo kwenye ukurasa wa 49 kwenye jadueli lao kwamba na barabara yangu ipo, pamoja na kuwa ni ahadi ya Mhe. Rais katika ufunguzi wa kampeni pale Kaskazini Pemba kwenye

kiwanja chetu cha Konde. Kwenye kampeni zake Rais aliahidi kwamba barabara hiyo ataijenga haraka iwezekanavyo.

Kwa hivyo na mimi napenda kuchukua fursa hii kuwataka watendaji wa wizara hii pamoja na mambo mengine, lakini wasije wakaisahau barabara hii kwani ni barabara muhimu kwa ajili ya wananchi inatoa mazao mengi na pia, ni muhimu kwa wavuvi. Pia, ikumbukwe kuna kituo chetu kikubwa kule cha askari wataendelea kupata tabu wa usafiri kama itaachwa na kuharibika.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, barabara ya Makangale ni barabara muhimu kwani ni moja katika sehemu zinazotuletea fedha nyingi za kigeni. Ni eneo ambalo lina maeneo ya uwekezaji, watalii wengi huwa wanakwenda kule, vile vile, wizara yenyewe wana kituo chao, kuna mnara mkubwa wa historia kule uliojengwa zaidi ya miaka mia moja na zaidi iliyopita. Kwa hiyo, iko kila sababu ya kuzifanya barabara hizi zikapewa kipaumbele cha kuzifanyia matengenezo ili ziweze kutumika. Mhe. Naibu Spika, ni matumaini yangu kwamba wizara imekisikia kilio changu na ni imani yangu suala hili litapatiwa ufumbuzi wa haraka.

Mhe. Naibu Spika, pia, napenda kuikumbusha wizara juu ya barabara zote za Pemba zilizotengenezwa kwa kiwango cha kifusi kwamba, habari tulizonazo hivi sasa barabara zile zimeanza kukatika japo wanasema kwamba watazitengeneza. Lakini ikumbukwe kwamba barabara ya kifusi ikimaliza mvua ya Masika barabara hizo zinaharibika kila siku. Kwa hiyo, wito wangu kwa wizara tuzibe ufa tusisubiri kuja kujenga ukuta, pale zinapohitajika kutengenezwa barabara hizi ni wajibu kuzitengeneza kwa haraka. Kwa hiyo, namuomba waziri kwenye majumuisho yake atakapokuja aniambie ni lini barabara yangu ya Msuka itaanza kufanyiwa marekebisho. Mhe. Naibu Spika, atakapokuja Mhe. Waziri, namuomba jibu hili nipatiwe.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka kwenye barabara, naingia kwenye Shirika la Bandari. Mhe. Naibu Spika, Shirika la Bandari kama nilivyotangulia kusema kwamba wizara hii ndio mama, ni wizara ambayo macho na masikio yetu yote sisi humu tunayaelekeza kwenye wizara hii, na ndio maana inatengewa bajeti kubwa sana ya serikali kwa kuona umuhimu wa wizara hii.

Mhe. Naibu Spika, wenzangu wamesema mengi kuhusu habari ya mrundikano wa makontena pale bandarini. Mimi sina haja ya kuyaeleza sana, nilitoa ushauri wangu juu kule kwamba wenzetu wote yanapowakuta mambo kama haya wanaanzisha bandari kavu. Mimi nataka niulize kuna kigugumizi gani cha wizara cha kuanzisha bandari kavu ili kuondoa mrundikano wa makontena

uliopo pale bandarini? Hebu tuambiwe kuna tatizo gani kubwa au kikwazo gani kinachosababisha, ikiwa ni gharama, bora kuongeza gharama lakini tukaongeza na ufanisi. Tunaongeza gharama kidogo ya kuliondoa kontena pale, tunalipeleka kwenye bandari kavu au maeneo kama aliyoyataja Mhe. Nadir, maeneo tunayo, kwa nini kontena ziendelee kubakia bandarini.

Mhe. Naibu Spika, jambo hili ni suala la kuchukuliwa hatua za dharura, vyenginevyo, tutakosa kufikia malengo tunayoyakusudia, na hapa itakuwa hapana wa kulaumiwa, itabidi sisi tujilaumu wenyewe, kwa sababu tatizo limeonekana kuwa tatizo ni mrundikano mkubwa wa makontena upo, lakini utekelezaji wake unakuwa mdogo. Mheshimiwa, tusisubiri kulaumiana wakati umefika sasa wa serikali kupitia wizara inayohusika ikayatafutia ufumbuzi wa haraka kwa kuyaondoa makontena matupu ili kutoa nafasi kwa meli ziweze kushusha makontena na kutoa huduma nyengine.

Leo meli ngapi ambazo zipo nje zinahitaji kufunga na kushusha mizigo. Mhe. Naibu Spika, lakini ukiangalia wapi utaweka mizigo ni kwamba hamna.

Mhe. Naibu Spika, viwanja vya Maisara naomba vitumike, kiwanja cha Kibanda Maiti kitumike kwa haraka ikiwa uwezekano wa kuanzisha bandari kavu ni mdogo basi viwanja vile kwa sababu ni vyetu vitumike, kuna kigugumizi gani? Naomba Mhe. Waziri, akija atwambie kuna kigugumizi gani kinachofanya suala hili kuwa ni gumzo ndani ya Baraza. Kwa hiyo, tunaiomba wizara ichukue hatua haraka za utekelezaji kuona kwamba jambo hili linapatiwa utatuzi wa haraka iwezekanavyo ili tufikie lengo tulilolikusudia.

Mhe. Naibu Spika, pia, kwenye hilo hilo Shirika la Bandari, ukurasa wa 18, kifungu cha 58, naomba kidogo nikisome;

"Kwa upande wa miradi ya shirika, shirika limenunua vifaa vya kufanyia kazi bandarini kwa ajili ya kuongeza ufanisi wa huduma na mizigo katika bandari zetu. Hadi kufikia Machi, 2016 shirika limetumia jumla ya shilingi 5,634,580,998 kwa kulipia vifaa hivyo".

Mhe. Naibu Spika, vifaa vyenyewe vimetajwa hapa; kreni 2, *terminal tractor* 2, *trailer* 2, *reach stacker* 2, *fork lift* 3 na *empty handler* 1, ambapo baadhi ya vifaa hivyo vimewasili. Kwa ujumla nasema mradi huo utatumia shilingi bilioni 11,035,176,377. Lakini hawakutwambia vifaa ambavyo vimeshafika ni kifaa gani na gani, wametutajia orodha ya vifaaa vilivyonunuliwa na wamesema baadhi yao vimefika lakini hawakututajia. Kwa hiyo, naomba

waziri atakapokuja atuambie ni kifaa gani na gani ambacho kimeshawasili bandarini na kimeshaanza kutumika kufanya kazi au bado.

Vile vile, katika kifungu hicho hicho anasema;

"Aidha katika kuimarisha usalama wa vyombo vya baharini shirika limenunua maboya saba mapya na taa tano za *solar* za maboya ambayo yametumia jumla ya shilingi milioni 448,649,370 hawakutwambia…"

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa, umebakiza dakika tatu.

Mhe. Omar Seif Abeid: Hawakutwambia kwamba kila boya limegharimu bei gani na ni maboya ya kiasi gani Mheshimiwa, yaliyotumia pesa hizi. Maana mimi naona ni ghali sana maboya haya, lakini Mhe. Naibu Spika, mimi napenda kuchukua fursa hii kuishukuru Mamlaka ya Usafirishaji wa Anga kwa kuboresha Uwanja wa Ndege wa Pemba, sasa hivi sisi ni mashahidi sote tunaamua kwenda Pemba leo asubuhi na jioni tunarudi tunakuja kuwajibika kwenye Baraza hili, ambacho ndio chombo pekee cha wananchi kinachotetea maslahi ya wananchi.

Mhe. Naibu Spika, napenda kuyashukuru mashirika yote ya ndege ya ndani likiwemo shirika la *Assalam.* Shirika hili napenda kulipongeza kwa sababu ni mkombozi wetu sisi Wapemba, ni shirika ambalo la kupigiwa mfano kwa sisi. Mimi napongeza sana kwa ununuzi wa ndege nyengine kubwa mpya, lakini naliomba lisiishie kutoa huduma zake mchana tu hata usiku liweze kufanya huduma, kwa sababu uwanja wa ndege tayari umeshafungiwa taa, ni hatua za kujivunia.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo naunga mkono asilimia mia kwa mia hotuba hii, lakini namuomba Mhe. Waziri, atakapokuja asisahau majibu yangu ili niweze kujiridhisha. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa na mimi nafasi ya kuchangia.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Mhe. Naibu Spika, ahsante na mimi kunipa fursa hii ya kuchangia hotuba ya bajeti ya Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Usafirishaji.

Mhe. Naibu Spika, mimi moja kwa moja niende kwanza kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kuweza kuweka sawa kitabu chao ambacho kwa namna moja au nyengine kilipangwa kitaalamu.

Mhe. Naibu Spika, sasa niende moja kwa moja kwenye upande wa barabara. Mimi ningemuomba Mhe. Waziri, kama nilivyoomba huko nyuma kuna haja ya kuhakikisha wanaziboresha zile barabara ambazo Wizara ya Kilimo wamezianzisha kwa njia ya fusi ili barabara zile ziweze kutumika kwa muda mrefu na kuipunguzia mzigo mkubwa serikali, kwa sababu inaonekana dhahiri kwamba tunatengeneza barabara kupitia wizara nyengine ambapo baadae inaachwa inakufa kabisa, baadae tena Wizara ya Usafirishaji ndio inatengeneza tena barabara ile.

Sasa ili kuipunguzia mzigo serikali mimi nafikiri ingekuwa vyema kabisa pale wizara moja inapoanzisha mradi ule basi bila kuchelewa wizara nyengine imalizie kwa sababu barabara hizo ziwe madhubuti ili kupunguza usumbufu wa usafiri kwa wananchi wetu. Halikadhalika, nimpongeze Mhe. Waziri, kwa hatua hii aliyoanza nayo, nawapongeza sana kwa sababu naona hapa Unguja sasa hivi wameamua kuziba mashimo kila lilipo, pia, nimepata taarifa hata Pemba wameanza.

Mimi naomba niwapongeze kwa juhudi hii walioanza nayo kwa sababu mwanzo mzuri wa kutunza barabara zetu ni pale inapotokezea athari ndogo kuishughulikia kabla ya kungoja makubwa. Ingekuwa ni afya ningesema kwamba, '*prevention is better than cure'*. Mhe. Naibu Spika, hatua hii itatupunguzia malalamiko makubwa kwa wananchi wetu hususan waendesha magari, kwamba barabara zetu mbovu na hii ni juhudi rasmi ya Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein anayotaka kuhakikisha kwamba wananchi wake katika nchi yake hawasumbuki, upande wa usafiri wanasafiri vizuri na upandaji wa malazi wanalala vizuri. Kwa hivyo, ni vyema uamuzi huo aliouchukua Mhe. Waziri, unaendelea hivi, *speed* hii naomba isipungue.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye usafiri wa majini, naipongeza wizara pamoja na Mhe. Rais, baada ya athari kubwa iliyotokea nchini kwetu kuweza kuleta meli ile mpya ya Mapinduzi II. Napenda kuwapa hongera kubwa meli ile inafanya kazi kisawa sawa, imewapunguzia dhiki wananchi wetu na kuwapa usafiri wa uhakika ndani ya visiwa vyetu hivi viwili. Lakini kuna tatizo moja bado halijakuwa tayari usafiri sasa hivi wa Dar-es-Salaam/Zanzibar, Zanzibar/Pemba hauna wasi wasi, napenda kutoa pongezi kubwa. Tunataka usafiri sasa hivi serikali ishughulikie usafiri wa kutoa Tanga/Pemba. Mimi nafikiri ile *MV*. Maendeleo kama imeshaanza ni pongezi kubwa na naomba iendelee hivyo. Pale pana wafanyabiashara wengi, kuna wananchi wengi wanasafiri pale, sasa ikiwa *MV*. Maendeleo imefikia utaratibu wa kuanza safari pale mimi napenda kutoa pongezi kubwa kwa wizara hii. Lakini nina lalamiko moja dogo tu, naomba tena Mhe. Waziri, unisikilize na hili ulishughulikie kwa

umuhimu sana, ile meli yetu mpya ya *MV.* Mapinduzi II kuna mapato pale tungepata zaidi kuliko hivi tunavyopata sasa.

Kuna tatizo la ule mlango hebu Mhe. Waziri, utakapokuja utwambie ile meli ina tatizo gani ule mlango wa kupakilia sehemu ya mizigo ukawa haufunguki, kwa sababu kuna mapato makubwa pale yanakwenda kwenye mashirika binafsi, kwa mfano ile meli yetu ingekuwa inafunguka ule mlango kuna nafasi kubwa kule chini yangeweza kupakiwa magari, mizigo mizito, lakini meli yetu ile kazi yake ni kupakia abiria na mizigo midogo midogo. Lakini ina nafasi na uwezo wa kupakia magari zaidi ya 50 mle ndani, ni jambo la kusikitisha kwa nini ule mlango haufunguki. Mimi nakuomba Mhe. Waziri, utakapokuja hapa hebu tuelezeni vizuri kwa nini ule mlango haufunguki, kuna tatizo la mtaalamu hajaja, ufunguo wake haujuulikani, yule *Captain* aliyepewa hajui. Lakini pale tukufungua mlango ule tutapata mapato makubwa kwenye serikali yetu. Naomba Mhe. Waziri, hili ulishughulikie na ukija utueleze hasa tatizo ni nini.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende kwenye usafiri wa anga. Mwenzangu aliyetangulia amepongeza sana usafiri wa anga kwa mashirika binafsi. Hebu tujiulize hivi kuna tatizo gani na sisi tusianzishe shirika letu la usafiri wa ndege la Zanzibar, nina hakika kwamba hata nauli itaweza kupungua tukawapunguzia mzigo wananchi wetu ukiachilia mbali yale mashirika binafsi. Mimi nayapongeza kwamba yanatoa huduma pale, lakini na sisi tungeweza kuweka shirika letu la ndege la Zanzibar likaweza kutoa huduma katika visiwa vyetu hivi na hata nje ya nchi tukaongeza pato la serikali.

Mhe. Naibu Spika, niende katika bandari na bandari yangu kubwa mimi Mheshimiwa, nataka ile ya Mkoani pale. Pale kuna mapato tunapata kwenye bandari ile kwa namna ile ile ya kuteremsha mizigo, lakini mashine iliyokuwepo pale Mhe. Naibu Spika, ni moja tu. Kwa hiyo, ningemuomba Mhe. Waziri, angeweza kuongeza ule utaratibu au zile zana za kuinulia mizigo kwa sababu mzigo unapokuwa mkubwa kidogo ile mashine pale haiwezi kubeba ule mzigo, inabidi inatafutwa kampuni binafsi kubeba ile mizigo au tajiri wa mizigo apakie kwenye meli ambayo inaweza kwenda mpaka juu kama meli ya Kasa na Jitihada. Kwa hivyo, ingekuwa ni vyema na pale tungeongeza uwezo wa zana za kupakulia mizigo kwenye meli ili nayo tuweze kupata mapato ya uhakika.

Mhe. Naibu Spika, niende upande wa nyumba za maendeleo. Mimi kwanza naipongeza wizara pamoja na Mhe. Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuwajengea wananchi nyumba zile za maendeleo ambapo kwa kiasi kikubwa sasa hivi wananchi wetu wananufaika na faida za Mapinduzi ya 1964.

Nyumba zile zinawasaidia wananchi wetu, lakini ningependa kujua utaratibu kwa sababu majumba yale kila ninapopita yamechakaa sana. Ni majumba mazuri ambayo kama yangetunzwa na yakawa yanapata ule ushughulikiaji mzuri kwa kila wakati basi zingeendelea kupendeza nyumba zile. Lakini sasa hivi inaonekana zimepoteza ile nuru au bashasha nzuri hata kwenye mji wetu ile haiba inaondoka ondoka, kwa sababu zile nyumba zinaachiliwa muda mrefu hazitengenezwi. Hivi kwa nini Mhe. Waziri, asingeweka utaratibu kwa wale ambao wamekodishwa zile nyumba kama wizara haiwezi kuzitengeneza kwenye mikataba yao ikaingizwa na neno la kutengeza na ikapunguzwa bei ili zile nyumba zikaleta haiba nzuri kwenye nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu zile nyumba zinaonekana nyengine nina wasi wasi sasa hivi hazikaliki tena. Sasa ningemuomba Mhe. Waziri na taasisi zake hebu wazipitie zile nyumba na wajaribu kufanya utafiti wa kina ili ziweze kutengenezwa na zipendeze, kwa sababu lengo la serikali ni kuhakikisha wananchi wake wanakaa kwenye makaazi mazuri.

Mhe. Naibu Spika, la mwisho kabla sijalisahau mimi niipongeze hii Kampuni ya *MECCO,* mwenzangu kapongeza kampuni za ndege, mimi naipongeza ya *MECCO* ya kujenga barabara ya kisasa kule Pemba. Kwa kweli ile kampuni imefanyaa bidii kubwa, imejenga barabara ya kisasa yenye miundombinu inayotakikana kwa sababu barabara nyingi za nchi yetu ukitembea kilomita mbili, tatu huwezi kukuta *culvert*, huwezi kukuta daraja maalum, huwezi kukuta zile alama sahihi za kwenye madaraja, lakini kampuni hii imeziweka. Kwa hiyo, mimi naomba hata maegesho imeweka sehemu za kusimama daladala tu kwa uhakika ili abiria wetu waweze kuteremka wakiwa salama.

Mhe. Naibu Spika, nakuja upande wa Chake-Chake ninaiomba wizara, Mhe. Waziri pamoja na Naibu Waziri, Afisa Mdhamini kule Pemba tunaomba tuekewe *stand* za abiria kwenye barabara zetu. Lakini sio za abiria tu pale Chake-Chake hapana *stand* hata ya yale madalala yote, ni mji ambao umefinyika, kwa nini wizara haifanyi utaratibu maalum. Kule Qatar kuna sehemu mimi nafikiri kama ile ingejazwa kutoka pale sokoni Qatar mpaka kule Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, ingejazwa kifusi ile tukaondoa ile mikoko kungekuwa ni kuzuri tu. Kwa hiyo, tungeweza kupata mapato makubwa lakini na magari yetu yangekaa kule kwa usalama, abiria wasingesumbuka na tukaendelea vizuri. Mimi ningeomba Mhe. Waziri, hili alitilie maanani ili kuondoa ule msongamano wa magari na msongamano ule Mheshimiwa, kuna siku ulisababisha hata magari kutokuingia na kutokutoka kule *stand* na ukasababisha usumbufu kwa wafanyakazi wetu, wananchi wetu na wafanyabiashara.

Mhe. Naibu Spika, mwisho, mimi napenda kumpongeza Mhe. Waziri, tena na nathubutu kusema kwamba naiunga mkono hotuba hii ya Mhe. Waziri, asilimia mia moja na moja, navuka lengo. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana. Sasa anayefuata Mhe. Bahati Khamis Kombo, baada ya Mhe. Bahati Khamis Kombo, atafuata Mhe.Mussa Foum Mussa na ajitayarishe Mhe. Mihayo Juma N'hunga.

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipa nafasi mchana huu nikaweza kuchangia hotuba hii. Kwanza kabisa Mhe. Naibu Spika, nimshkuru Mwenyezi Mungu aliyeweza kutufikisha hapa tukiwa wazima wa afya na leo tuko ya Baraza lako Tukufu kujadili mbali mbali ya wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, nachukuwa fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa hotuba yake nzuri ambayo hutuba imetupa changamoto mbali mbali katika majimbo yetu. Mhe. Naibu Spika, nimpongeze sana Mwenyekiti na Makamo Mwenyekiti wa Kamati yetu Mhe. Suleiman Sarahan Said, kwa jinsi alivyoiwasilisha hotuba jana, hotuba ile aliyoiwasilisha akiwa mahiri sana kama tunavyomuona kwamba ni jembe na jembe ambalo hili halitaki kutiwa cherehe, ni jembe liko makini kabisa.

Mhe. Naibu Spika, mimi niende moja kwa moja katika barabara ya Ole/Kengeja. Nimwambie Mhe. Waziri, kila atakaesimama katika Wilaya ya Chake Chake na Mkoani ataisema sana barabara ya Ole/Kengeja. Kwa sababu barabara hizi Mhe. Naibu Spika, zimeigusa Ole, Wawi, Chonga, Chambani, Kiwani na Mtambile na kila mtu anaelia anasema mama yangu, hasemi mama yetu.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa kumpa kilio changu na akaweza kuchukuwa fursa ya kwenda kuziangalia zile nafasi za barabara zetu za Pemba ambazo zina matatizo na akaweza kutuahidi kwamba barabara zile atazifanyia matengenezo ya awali. Leo hii namuomba Mhe. Waziri, atuambie kwamba ile barabara ya Ole/Kengeja itakayofanyiwa matengenezo ya awali ni mwezi gani itaanza kufanyiwa matengenezo.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, tumeungana na wenzetu ambao wapo katika eneo la Kiwani, hawa wenzetu mimi nimepakana nao na nimeanzia Kichaka/Ukutini, kwa kweli Mhe. Naibu Spika, watu hawa wanahitaji kuonewa huruma sana sana sana, kwa sababu kutoka Kichaka ukija Ukutini Mgonjwa hachukuliki

wakati wa mvua, ni lazima utumie kitanda au gari la ng'ombe, haya ni mambo ambayo kuwa sasa hivi yameshapitwa na wakati, wanahitaji kutiliwa angalau kifusi. Vile vile, Mheshimiwa, kutoka Pale Chwaka kuelekea Kendwa ni sehemu mbovu sana sana sana, Mhe. Naibu Spika, tunaomba Mhe. Waziri, atakapokuja atuambie barabara hii ya Ole/Kengeja tayari tumeambiwa imeshatimia miaka minne tokea kutengenezwa, je, barabara hii itamalizwa mwaka gani?

Mhe. Naibu Spika, lakini vile vile, niende katika barabara iliyoko Ngomeni, Ngomeni Puyuni, lile tumepakana na Jimbo la Chonga, barabara ile Mhe. Naibu Spika, inatoa zao la karafuu la kupigiwa mfano katika Wilaya yetu ya Mkoani. Namuomba Mhe. Waziri, aione barabara ile kwa jicho la huruma angalau kwa kifusi kabla ya kuchuma karafuu.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, niende katika ujenzi wa zile nyumba za marehemu Mzee Abeid Amani Karume ziliopo katika Jimbo la Kiwani Kengeja. Mhe. Waziri, ile nyumba pale ya majenzi Kengeja ni nyumba mbovu na tayari Mhe. Naibu Waziri, keshakwenda kuiangalia ile nyumba kuhusu ubovu wake jinsi ilivyo. Je, Mhe. Naibu Waziri, imechukuliwa hatua gani mpaka sasa hivi ile nyumba na wanaishi wananchi ndani ya nyumba ile. Vile vile, Mhe. Naibu Spika, tuna nyumba zilizopo Kilimatindi Chake Chake, zile nyumba pale ni mbovu, kwa kweli ukiingia ndani ya zile nyumba huwezi kuamini kama zile nyumba zinaishi wananchi walio na watoto, zile nyumba ni mbovu tena mbovu sana, tunamuomba Mhe. Waziri, atuambie nyumba zile kazipangia lengo gani la matengenezo kwa mwaka huu wa 2016/17.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, mimi nitakwenda katika utendaji wetu wa wafanyakazi wetu wa juu. Mhe. Naibu Spika, tunapotoa tenda za Makandarasi, tukajengewa zile barabara wanahitaji hawa watendaji wetu wa juu kuzipitia zile barabara zinazojengwa, kwa sababu wale Wakandarasi nao ni binaadamu kama sisi wanaweza wakakosea, lakini imeonekana kwamba watendaji wetu wanachelewa kwenda kuziangalia zile barabara mpaka tayari wameshafikia hatua kubwa ndio linaonekana kosa.

Hili Mhe. Naibu Spika, tunawaomba watendaji wasimame imara na tuone kwamba tufuate ule mfumo aliosema Mhe. John Pombe Magufulu "hapa ni kazi tu", tusikae tu maofisini tukaona kwamba wakandarasi wetu wataendelea tu kufanya vizuri, lengo lao ni hilo lakini na sisi tuwe nyuma yao kuangalia ujenzi, mtu anapojengewa ni lazima yeye mwenyewe awe mbele kuangalia msingi huu niliochimbiwa kweli nyumba yangu haitabomoka au nyumba yangu

itabomoka, watendaji tunawaomba tushirikiane kwa pamoja ili kufanikisha lengo la Serikali kuwaondolea wananchi matatizo yao.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitakwenda kidogo katika wafanyakazi wa Bandari. Mhe. Naibu Spika, kama tunavyojua kwamba baadhi ya wafanyakazi wanafanyakazi pale Bandarini wakilipwa lakini bado si waajiriwa rasmi. Sasa nimuombe Mhe. Waziri, kwamba, hawa wafanyakazi ambao tayari pengine wameshatumia miaka 20 wanafanya kazi kubwa kubwa pale bandarini umewapangia mpango gani juu ya kuwaajiri wafanyakazi hawa na tukiangalia sana wafanyakazi wengine wanastaafu na tunajuwa kwamba pale wafanyakazi sasa wana mapungufu, wale waliokwisha staafu na hawa wanaoendelea kustaafu, lakini sikuiona katika hotuba yako kwamba humu utaongeza wafanyakazi angalau kidogo kuziba yale mapengo yaliyopo pale. Namuomba Mhe. Waziri, atakapokuja fanya majumuisho atuambie ni lengo gani alilowapangia wale wafanyakazi wanaofanya kazi pale na bado hawajapatiwa ajira rasmi.

Mhe.Naibu Spika, ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Bahati, mchangiaji anaefuata ni Mhe. Mussa Foum Mussa, baada ya hapo atakuja Mhe. Mihayo Juma N'hunga na baada ya Mhe.Mihayo, ajitayarishe Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipa ruhusa ya kuchangia bajeti hii. Kwanza Mhe. Naibu Spika, na mimi nimpongeza Mhe. Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa utendaji wao mzuri kwa muda mfupi tu huu walioingia katika Wizara hii. Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo na mimi kwanza nataka nichangie katika barabara ya Mgagadu Kiwani.

Mhe. Naibu Spika, kwanza napenda niipongeze Serikali kwa jitihada zake kubwa za kutaka kuimaliza barabara hii kwa sababu kwa muda mkubwa sana imekuwa wananchi wa sehemu hii walikuwa na kilio kikubwa kwa barabara yao hii. Kwa vile tunategemea kwa bajeti hii kwa mwaka huu huenda ile barabara yetu ikamalizika kwa utiaji wa lami.Lakini Mhe.Naibu Spika, nataka niseme kwamba barabara ile mpaka hivi sasa imetiwa kifusi kutoka Mgagadu mpaka Kiwani Sokoni, lakini nataka niseme kwamba Mhe. Rais alipokuja Kiwani kuzinduwa kituo cha hospitali kilichopo pale Kiwani, aliahidi kwamba barabara ile itajengwa kutoka Mgagadu mpaka Bandari ya Kiwani Pwani, lakini mpaka hivi sasa imetiwa kifusi mpaka pale sokoni tu, sasa tumejengwa na wasi wasi kwamba, je, itakuwa inamalizia pale au itafuatwa ile amri au

maelezo aliyotoa Mhe. Raisi. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri, atakapokuja hapa atueleze kwamba, je, ile barabara yetu Mgagadu Kiwani itafika mpaka pwani kama alivyoeleza Mhe. Rais. Hilo la kwanza.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kutoka hapo sasa niende katika barabara yetu ya Mtambile Mwambe na hizi ni barabara ambazo zimejengwa si muda mrefu sana ni barabara ya Mtambile/Mwambe, Mtambile/Kangani na Mizingani/Wambaa. Kwanza tupongeze sihaba tulikuwa na dhiki kubwa sana katika barabara zetu hizi kwa vijiji vilivyoelekea. Lakini tuseme kwamba barabara hizi ujengaji wake ulikuwa si wa kiwango, si muda mkubwa sana barabara zimeanza kuchimbuka, sasa nataka niseme kwamba Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri, zile barabara zinataka *maintenance* kubwa ili zisije zikamalizika na mapema.

Mhe. Naibu Spika, baadae niseme kwamba katika ujenzi uliofanywa barabara ya Mtambile/Mwambe, ujenzi huu kuna wananchi wengi walipoteza au walichukuliwa vipando vyao na mpaka hii leo bado fidia haijalipwa na muda umekuwa mkubwa si chini ya miaka mitano au sita tokea wakati wa Mhe. Amani, Rais wa Zanzibar alipokuwa yeye, ndio zilipojengwa barabara zile na wananchi vikaumizwa vipando vyao kwa ujenzi na mpaka hii leo bado wananchi hawajalipwa mafao yao. Sasa namuomba Mhe. Waziri, atakapokuja atueleze kwamba, je, wananchi hawa watalipwa fidia yao lini, ili na sisi tujuwe vya kwenda kuwaeleza suala hili.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kuondoka hapa, sasa na mimi vile vile niende katika ujenzi wa barabara ya Ole/Kengeja. Mhe. Naibu Spika, kwanza tupongeze Serikali kwa nia safi kabisa ya kwamba inataka kuwaondoshea wananchi wa ukanda wa Mashariki juu ya ujenzi wa barabara hii. Lakini Mhe. Naibu Spika, mimi bado nina masikitiko makubwa juu ya ujenzi wa barabara ya Ole/Kengeja, kwa sababu muda umekuwa mkubwa, mrefu sana wa utajo wa barabara hii lakini ujenzi wake bado unasuwa suwa.

Mhe. Naibu Spika, mimi nasema kwamba bado ikiwa nia ipo kwa Serikali ya ujenzi wa barabara hii bado ninaomba Serikali itafute Kampuni yenye uwezo wa kujenga barabara hii. Kwa sababu barabara ya Ole/Kengeja ni barabara ambayo kuwa itakuwa ni mpya kwa ujenzi wake, haitaki mchezo katika ujenzi wake, inataka kampuni iliyokuwa kabambe yenye uwezo. Mhe. Naibu Spika, sote tunafahamu kwamba barabara hii wakati huo wa *Afro*-Shirazi iliyoanzishwa na mzee mmoja aliyekuwa akiitwa Rashid Abdalla maarufu Mamba, barabara hii inahitaji madaraja tena makubwa, ujenzi wake bado ni mkubwa, sasa kuzipa kampuni zenye kusuasua ni kujidanganya, na kwa upande

mmoja hii barabara itakuwa si ndogo kwa sababu imepita sehemu nyingi tu, imeanzia Ole, Vitongoji, Pujini, Chambani, Ukutini, Kichaka, Kendwa, Nanguji na Kengeja yenyewe. Sasa barabara itakuwa ni ndefu kidogo nadhani ina kilometa kama 35 hivi.

Mhe. Naibu Spika, sasa mimi ninaiomba Serikali ijitahidi kutafuta kampuni ambayo kuwa itakuwa na uwezo wa kujenga barabara hii kwa sababu imetajwa kwa muda mrefu sana zaidi ya miaka 10 na kwa ujenzi huu unaoendelea hivi sasa ikiwa haikubadilishwa basi inawezekana ikafika miaka kumi, je, hii ambayo kuwa inataka ujenzi, kwa mfano ikatwe minazi, ifanywe nini, kwa hiyo, naiomba Serikali itafute kampuni ambayo kuwa itakuwa na uwezo wa kujenga barabara hii.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo vile vile niseme kwamba, kuna barabara ambazo kuwa zilipitia msaada wake Wizara ya Kilimo, kwa mfano kama Jimbo langu mimi iko barabara inayotoka Ukutini/Mtangani Pwani, barabara hii imetiwa fusi safi kabisa, kwa hiyo, tunaiomba Wizara, Wizara husika ni hii kwamba zile barabara sasa wazichukuwe wao kwa sababu washafanyiwa kazi kubwa tu ili wafanye jitihada waziweke lami kwa sababu inaponyesha mvua yale matumaini ya wananchi wa vijijini kuondolewa tatizo la usafiri bado litakuja rudi pale pale, kwa hiyo, tunaiomba Wizara hizi barabara waziweke lami ili ziwe madhubuti zaidi ikinyesha mvua zisiharibike.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo, vile vile, narudi tena katika Wizara ya Mawasiliano kwamba kuwaeleza hivi, kwanza katika Wilaya yetu ya Mkoani, sehemu ambayo tunategemea kupata fusi ya kujengea barabara ni kutoka shehia ya Muwambe. Lakini tuseme kwamba wazee wa zamani wanasema; 'ukitaka uzuri lazima uzurike'. Sasa tunataka kujengewa barabara lakini lazima itabidi pafanyike uharibifu, sasa niseme kwamba kule Muwambe kuna sehemu inaitwa Makaani na hasa jina maarufu 'Mbuyu Hoja' kule ndio kinakotoka kifusi cha barabara zote zinazojengwa Wilaya ya Mkoani, sasa nataka niseme kwamba mawasiliano inachimba fusi Makaani na Makaani ni sehemu ya wananchi wa Muwambe walikotegemea kulima, lakini kwa bahati mbaya kwanza yale mashimo yanayochimbwa mafusi yanakuwa makubwa zaidi, wanaenda chini zaidi mpaka yanatoka maji na yanakuwa mengi, sasa wananchi wanashindwa kuendeleza kilimo katika maeneo hayo.

Mhe. Naibu Spika, sasa naishauri Wizara kwamba itakapokuwa inachimba sehemu zile na hizo sehemu ambazo kuwa wameshaanza kuchimba basi alau kidogo wafukie kule chini kwa udongo, wachukue udongo sehemu wanazojenga barabara walete pale ili kwanza watakuwa kidogo wamesaidia

uharibifu wa mazingira na baadae wananchi wanarudi tena kupata sehemu za kulima, lakini hivi sasa sehemu zote walizochimba kifusi basi hazilimiki. Mheshimiwa, sasa naiomba Serikali kupitia Wizara ili kupunguza lile joto, lile joto ambalo kuwa mashimo yanakuwa mengi, wananchi hawapati kulima tena, kwa hivyo, wakifanya hivi na ule uharibifu wa mazingira, kwa sababu mara nyingi Serikali inakataza wananchi wasiharibu mazingira, lakini sasa kwa upande wa pili Serikali iwe ni mfano kwa sababu wakianza kufukia mashimo yale waliyochimba kifusi basi itaonekana kwamba Serikali iko mstari wa mbele kutokuharibu mazingira.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa nataka niende Shirika la Bandari. Mhe. Naibu Spika, hapa tumeelezwa katika ukurasa wa 19, naomba ninukuu kidogo hapa;

> "Vile vile, Shirika linaendelea na matengenezo ya eneo la kuwekea makonteni katika Bandari ya Mkoani kwa kuweka uzio, taa, pamoja na kuliwekea sawa eneo hilo".

Mhe. Naibu Spika, kwanza mimi napenda nishukuru maelezo haya ikiwa yatafanyika kweli, lakini sasa kwanza nataka niulize kwamba hayo makontena yataletwa pale bandarini kutoka nje moja kwa moja au yataletwa kutoka wapi? Kwa sababu mara nyingi tulikuwa tunaambiwa kwamba Bandari ya Mkoani itawekwa zana na meli zitakuja kutoka nje kufunga gati pale, ili kupata kupakua mizigo kutoka nje, lakini mpaka hii leo bado haya mambo yanasua sua. Sasa mimi nataka niulize kwamba, je, hayo makontena yatakapoletwa pale yatapakuliwa na zana gani na hizo zana za kutumia kwa kupakua makontena pale hazipo hivi sasa. Je, tutaifanya ile bandari kwa wale wafanyabiashara wa Pemba badala ya kufunga Unguja zitakuja kufunga gati pale Mkoani na patakuwa na yale mambo ambayo yatatumika katika kuteremsha makontena.

Kwa sababu kuna baadhi ya wakati mwengine unaleta gari pale inashindwa kuteremshwa, je, makontena. Sasa atakapokuja Mhe. Waziri, atueleze kwamba makontena hayo yatatoka nje moja kwa moja au yatatokea wapi?

Mhe. Naibu Spika, mimi naomba nifikie hapo na naunga mkono bajeti hii kwa asilimia 90, 10 mpaka pale Mhe. Waziri, atakapokuja kutueleza au kunieleza yale masuala ambayo nilimuuliza. Moja ni barabara ya Mgagadu/Kiwani, je, itafika pwani kwa kuheshimu kauli ya Mhe. Rais na je, hii barabara ya Ole/Kengeja bado itakuwa inajengwa na kampuni gani, aje atueleze ili tujue.

Jengine ni kwamba wale wananchi wa barabara ya Mtambile/Mwambe walioharibiwa vipando vyao watalipwa fidia hiyo lini? Baada ya maelezo hayo akinijibu vizuri ili nami nipate kuchukua jambo la kwenda kuwaeleza wananchi wangu basi nitakuwa sina masuala ya kupiga buti.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo nashukuru sana.

Mhe. Mihayo Juma N'hunga: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana nami kwa kuniona na kuweza kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

Kwanza awali ya yote nami nitumie fursa hii dakika angalau moja au sekunde 30 kutoa hisia zangu za dhati katika moyo wangu na masikitiko yangu hasa kwa wananchi wote ndani ya Kisiwa cha Pemba kwa ile kadhia kubwa ambayo wanaipata kutokana na kikundi cha watu wachache kisichokuwa na dhamira ya dhati na taifa hili. Niendelee kuwaomba wananchi wote wa Kisiwa cha Pemba kuwa wastahamilivu, wasikivu, watulivu, serikali yao makini ipo inayasikia, inayatambua na kwa busara kubwa sana ambayo serikali hii inatumia ipo siku itakuja na majibu stahiki kwa wale wote ambao wanahusika na kadhia ile. *(Makofi)*

Pili, niingie moja kwa moja katika mchango wangu huu kama ambavyo wachangiaji wengi wamejaribu kuchangia kwa namna moja ama nyengine. Nami naomba niguse katika maeneo machache ambayo kwa pamoja tunaweza tukasaidia taifa letu la Zanzibar kusonga mbele kupitia wizara hii. Sambamba na hilo nichukue fursa yangu ya dhati kumpongeza sana Mhe. Waziri na Naibu Waziri kwa jitihada kubwa sana ambazo wameanza kuzionesha na kutoa matumaini mapya kwa Mhe. Rais kama vile ambavyo matarajio yake amekuwa akiyahitaji kupitia wizara hii.

Mhe. Naibu Spika, niende moja kwa moja kwenye huduma ya barabara. Serikali imekuwa ikitumia pesa nyingi sana kuhakikisha miradi ya barabara inakamilika na inatekelezeka. Lakini sijajua na nikilio cha muda mrefu sana, wakati mwengine serikali inatumia gharama kubwa hali ya kuwa usimamizi wa shughuli ile unakuwa si mzuri. Ni jambo la kusikitisha sana barabara ya Amani/Dunga mimi huwa nasema mpaka sasa barabara hii tangu ikabidhiwe haijafika kipindi cha miaka miwili, lakini barabara hii mpaka hivi sasa haina tena uhudumu wa kuweza kufika miaka miwili ijayokuja, kwa sababu tayari hii imeshaanza kukatika mpaka katika lami yenyewe. Bahati nzuri watu wa mawasiliano wapo, watu wanaohusiana na suala la barabara wapo, tunasubiri mpaka barabara ikatike halafu ndio tuje tuanze kutafuta mradi mwengine mpya

wa kung'oa na kutia lami tena, kitu ambacho si sahihi. Pesa za wananchi zinatumika, lakini pia pesa za walipa kodi Wazanzibari wanyonge zinatumika vibaya na watu wenye dhamana ya kusimamia maboresho ya barabara hii.

Mhe. Naibu Spika, nimuombe sana Mhe Waziri na Naibu wake, mimi najua hawa ni watu makini, waipitie barabara hii kuanzia Amani, Masingini, Mtofaani, Meli Sita, Regeza Mwendo mpaka Mwera barabara hii pembeni kote tayari imeshalika; kwa kuinusuru warudi waifanyie maboresho ya haraka ili kuweza kuisaidia na kuweza kutoa huduma kwa kipindi kirefu.

Mhe. Naibu Spika, bahati nzuri Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa dhamira njema sana ya kuwahudumia watu wake imekuwa ikijenga barabara hizi, lakini kwa kilio cha muda mrefu sana tangu kujengwa kwa barabara ya Amani/Dunga wananchi wa Mwera Mabonde ya Mpunga mpaka hivi leo wamekuwa wakitaabika kuweza kufuatilia stahiki zao na mpaka hivi sasa bado hawajalipwa. Kwa maana hiyo, tumuombe Mhe. Waziri, atakapokuja kufanya majumuisho yake hapa ya msingi azingatie pamoja na kutoa kauli kwa watu hawa wa Mwera Mabonde ya Mpunga ambao mwezi wa Novemba, 2015 ilitoka barua rasmi kutoka kwa aliyekuwa Katibu Mkuu wa wizara hii kutoa majibu kwa watu hawa kwamba, siku si nyingi stahiki zao watazipata. Sasa tunategemea sana Mhe. Waziri, atakuja na majibu ambayo watu hawa wataweza kufarijika angalau nao wapate kujisikia na maendeleo ya ujenzi ule wa barabara ambao umefanyika, nyumba zao kubomolewa kwa kuweza kupitisha ujenzi ule.

Pia, nikitizama kwenye kitabu cha Mhe. Waziri, wakati akiwasilisha katika ukurasa wa 27, kuna vipaumbele vyake ambavyo ameweza kuvi-*initiate*, lakini vile vile katika ukurasa wa 41, tayari kuna barabara ambazo zimeshatengewa fungu lake. Kwa mfano, naomba kunukuu.

Kiambatisho Namba 2(2), kinasema:

> "Ujenzi wa barabara tatu za vijijini Unguja Kizimbani-Kiboje, Jendele-Cheju-Kaebona na Koani-Jumbi (*km* 25.3)".

Tayari barabara hizi zote zimeshatengewa fungu lake kama ambavyo linaonekana hapa, lakini tukija kwenye vipaumbele hapa bahati nzuri barabara zote hizi za Jumbi, Jendele na Kaebona zinaonekana katika kipindi hiki zinaweza zikafanyiwa utekelezaji wake. Sasa wasi wasi wangu unanipa katika barabara ya Kizimbani-Kiboje. Barabara ile ni muhimu sana kwa wale wakulima wote katika maeneo yale mpaka kufikia maeneo ya Uzini. Barabara

hii haipo katika vipaumbele vya wizara na serikali, sasa ni vyema Mhe. Waziri, atakapokuja kutoa majumuisho yake hapa aweze kujibu kwa wananchi wote wa Zanzibar wanaohusiana na maeneo haya kwa nini barabara hii ambayo tayari serikali imeshatenga fungu kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo lakini bado barabara ile haimo katika vipaumbele vikubwa vya serikali katika mwaka huu. Sijajua kama itakuwa walikosea kuandika ama vipi, lakini natumaini Mhe. Waziri, atakuja na majibu mazuri sana katika hili.

Mhe. Naibu Spika, niendelee kutoa ushauri wangu sana kwa wizara hii hasa katika eneo la bandari. Zanzibar ni miongoni mwa mataifa machache ambayo yanafaidika sana na bahari, ni miongoni mwa maeneo yaliyokuwepo katika visiwa. Uchumi wetu mkubwa tunategemea kupata mapato kutoka katika sehemu mbili; sehemu ya kwanza ni utalii lakini sehemu ya pili ni bandari. Lakini kwa kujaribu kutizama ilipokuwa ikiwasilishwa hotuba hii na Mhe. Waziri, bado sijaona kwa kina kwa kipindi hiki cha mwaka 2016/2017 bandari hii itaweza kutoa *advertisement* za aina gani ili kuweza kuwasaidia wafanyabiashara wengi kuweza kurudi tena kufanya biashara zao Zanzibar.

Maana kwa kipindi kirefu sana wafanyabiashara wamekuwa wakihama kushusha mizigo yao Zanzibar na kwenda katika maeneo mengine, jambo ambalo linapunguza mapato katika serikali yetu hii hasa tukitegemea uchumi wetu mkubwa mapato mengi tunategemea kutoka katika taasisi yetu hii ya bandari.

Mhe. Naibu Spika, tukiamini sana, tuna watendaji wazuri katika bandari, tukiamini sana wizara hii ina Katibu Mkuu ni mtu mweledi ambaye ana uchungu wa dhati sambamba na mzee wake Mzee Aboud Jumbe Mwinyi. Sasa tunaamini kwa kushirikiana na Mhe. Waziri, suala hili la bandari wanaweza kuifikiria zaidi kadhia hii ili angalau kuwapa faraja wafanyabiashara wetu kuweza kurudi tena. Kwa sababu kwa kiwango ambacho makontena yamekuwa yakipungua na kwa kiwango ambacho meli zimepungua kufika Zanzibar inakuwa sio kitu kizuri.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia niende katika eneo la bahari. Katika bahari yetu kuna eneo wanaliita wenyewe *pilot ground* lipo karibu baina ya Fungu la Fatawa na maeneo ya Bumbwini. Eneo hili limeshakuwa *recognized* kimataifa kuwa ni eneo ambalo biashara zinaweza zikafanyika pale hasa katika zile biashara zinazohusu maeneo ya bahari. Kwa kipindi hiki tunashuhudia kuna meli nyingi sana za mafuta zimekuwa zikifanya biashara zake pale, kuna meli kubwa sana zinazotoka katika maeneo ya Msumbiji na mataifa mengine zimekuwa zikifika pale na kufanya biashara hii ya mafuta. Kipindi cha nyuma

tulikuwa tumeona Mamlaka ya Bandari ilikuwa ikipeleka huduma zake pale na mpaka hivi sasa mamlaka hii inapeleka huduma pale kwa mfano kama huduma za maji na nyenginezo.

Sasa nimuombe Mhe. Waziri, atapokuja hapa angalau atwambie kupitia biashara hizi zinazofanyika pale na biashara hizi ni chanzo cha miongoni mwa uuzwaji wa mafuta ya magendo, jambo ambalo linapelekea wakati mwengine kulipunguzia taifa hili mapato. Sasa naomba atakapokuja hapa atupe majibu kwa kipindi cha mwaka 2015/2016, kipindi ambacho kuna meli nyingi sana zimekuwa zikifanya biashara ya mafuta katika eneo lile basi atwambie serikali imepata mapato yake pale kwa kiwango gani na kiasi gani. Maana kadri ambavyo tunaendelea kuruhusu mataifa makubwa yakifanya biashara zake pale hali ya kuwa sisi tunachokipata wakati taifa husika zina sheria zake za ndani kuhusiana na utaratibu huu itakuwa tunaikosesha serikali yetu mapato kitu ambacho hakitakuwa kizuri sana.

Mhe. Naibu Spika, sambamba na wachangiaji waliopita kusema mengi, lakini nirudi kidogo katika suala zima la barabara. Mheshimiwa, katika jimbo langu la Mwera kwa kipindi kirefu sana tumekuwa na kadhia ya barabara za ndani jambo ambalo watu wengi wamekuwa wakitaabika na kunyanyasika. Lakini leo watu wa Mwera wamefarijika sana tangu kuteuliwa kwa Mhe. Balozi Ali Karume kuwa waziri wa wizara hii, hasa wale wananchi wote wa eneo la masingini wakiamini kuwa tangu mwaka 1970 kipindi ambacho Hayati Baba wa Taifa hili, Sheikh Abeid Amani Karume alipopanga mawe katika ujenzi wa barabara ya Masingini kutokezea Kijichi, lakini tangu kuondoka kwake katika dunia hii, barabara ile imepewa kichogo.

Sasa tuna imani sana na yeye kama ambavyo Rais aliyepita wa nchi hii alivyoamua kuweza kuenzi yale majumba ya Michenzani kwa kumalizia lile jengo ili aweze kumuasisi Mzee wake, na wananchi wa Masingini wanafarijika sana wakitambua kwa jitihada za Mhe. Waziri na yeye ataamua kuikamilisha barabara hii angalau kwa kiwango cha kifusi ili iweze kufika maeneo ya kule ili wananchi wa Masingini watakaotokea Dole mpaka Kijichi nao waweze kunufaika. Lakini itakapokamilika barabara hii hata watu wa mawasiliano wenyewe kuweza kufika katika mitambo ya redio kule na mitambo mengine ya mawasiliano nao pia wataweza kunufaika kama barabara hii itaweza kukamilika. Sasa tumuombe sana Mhe. Waziri, atakapokuja hapa aweze kuwapa majibu ya kina wakaazi na wananchi wa Mwera hasa katika eneo la Masingini kuhusiana na barabara hii.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa, umebakiwa na dakika tatu.

Mhe. Mihayo Juma N'hunga: Mhe. Naibu Spika, ahsante. Lakini kwanza niipongeze serikali kwa kuchukua maamuzi magumu kwa maslahi ya taifa hili ya kuweza kukamilisha ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri. Niipongeze sana serikali kwa uamuzi waliouchukua lakini bado nina neno dogo ambalo naweza nikaongezea hapa. Kwa sababu tayari tulishakuwa na wataalamu wetu wa ndani ambao nao waliwahi kutoa mapendekezo ya ujenzi wa bandari hii ukajengwa katika maeneo ya Mangapwani. Kwa sababu eneo la Mangapwani inaonekana kiujenzi ni eneo zuri zaidi kwa kuzingatia masafa kutoka eneo la ufukwe mpaka eneo la kina cha bahari, kuna takriban mita mia saba na kidogo wakati eneo hili la Mpigaduri tayari lina masafa takriban mita elfu mbili na zaidi, jambo ambalo ujenzi huu utang'arimu pesa nyingi sana na zaidi serikali kama ambavyo ingechukua maamuzi ya kwenda kujenga katika eneo la Mangapwani.

Sambamba na hilo nimuombe sana Mhe. Waziri katika majumuisho yake atapokuja kwa kushirikiana na wataalamu wetu wa ujenzi, ni vyema akatwambia madhara sasa ya kujenga bandari ya Mpigaduri hali ya kuwa tayari katika eneo la mkabala na eneo hili tumeshampa mwekezaji wa ndani, Ndugu Said Salum Bakhresa kuweza kujenga kitu kingine pale. Sasa waje watupe madhara ya kujenga bandari hii pale na katika eneo lile. Lakini zaidi ya hapo niipongeze sana serikali kwa uamuzi wake huu, nina imani serikali hii sikivu, serikali hii ina nia njema ya dhati kabisa ya kuwasaidia wananchi wake.

Mhe. Naibu Spika, zaidi ya kusema hayo naunga mkono hotuba hii ya Mhe. Waziri, hasa pale nitakapokuja kupata majibu ya kina ya ujenzi wa barabara ya kutoka Masingini kuelekea Kijichi. Mhe. Naibu Spika, ahsante sana.

Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa: Mhe. Naibu Spika, ahsante. Kwanza na mimi nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia leo hii kuweza kutoa machache niliokuwanayo. Lakini pili nikushukuru wewe kunipa nafasi hii ya kuweza kuzungumza hapa.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nampongeza Mhe. Waziri, aliyesoma hotuba hii kwa kukaa kuipanga yeye na wafanyakazi wake na kuiandaa kuja kutuletea sisi ili kuweza kuichambua kwa ajili ya kuwaletea maendeleo wananchi wetu walioko mitaani.

Mimi naanza na suala la wafanyakazi wa *UUB* Kibele. Ninamuomba Mhe. Waziri, akija hapa aje anambie neno la uhakika ili nimfahamu, namuomba au naiomba serikali iwaongezee mapato wafanyakazi hawa wanaofanya kazi Kibele. Wafanya kazi hao wanatoka nyumbani saa 12 wanarudi usiku katika

kazi zao hizo, lakini kazi zao ni za nguvu, za kokoto, kifusi na kupika lami. Wafanyakazi hao wanapotoka asubuhi hawana muda wowote wa kusema angalau wanakwenda kupanda shina la mgomba lipate kuwasaidia katika maisha yao. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri, akija hapa aje anambie atawasaidia vipi, namuomba awasaidie kwa nguvu zake zote ili wafanye kazi nzuri kwa ufasaha kutokana na maslahi yao.

Mhe. Naibu Spika, jengine pia niipongeze Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kutujengea barabara yetu nzuri kutoka Mtoni-Amani na pia, naiomba serikali barabara ni nzuri imenyooka, iko safi mtu yuko Mtopepo anaona mpaka Amani. Naiomba serikali Mhe. Naibu Spika, basi ili kwa kupendeza zaidi itutilie na sisi taa tuzidi kujiona na sisi tuko Mjini.

Lakini jengine Mhe. Naibu Spika, sisi watu wa Shehia ya pale Karakana na Shehia ya Mtopepo serikali ilitusaidia sana kutupa maendeleo na kuweza kutujengea na skuli mbili; moja Chumbuni na moja Mtopepo, tunaishukuru serikali kwa hilo. Lakini kikwazo kikubwa tunachokipata Mhe. Naibu Spika, barabara yetu nzuri lakini uendeshaji wa magari makubwa ya mchanga wanatuuliwa watoto wetu.

Mhe. Naibu Spika, magari makubwa yakipita yakiteremshwa kutoka Mtopepo kupandisha juu halina sumile na wa wala halijui kama pahala pale kuna skuli na watoto hawa wanatoka skuli ya Mtopepo na Chumbuni, hawafikirii mawazo hayo ingawaje alama zipo, lakini nadhani hawashughulikii. Basi namuomba Mhe. Waziri, azungumze na madereva wake wa magari makubwa wanatuuwa vibaya.

Jengine katika matengenezo hayo ya barabara yetu iliyokuwa nzuri tunamuomba basi sisi wananchi wa Chumbuni na Mtopepo Mhe. Waziri, atutilie angalau matatu pale angalau wananchi wasalimike kupipa na watoto wetu na watu wazima, tunaumia vibaya, la si hivyo Mhe. Waziri, akija hapa anambie anawasaidia nini wananchi wa Mtopepo na wananchi wa Karakana kutokana na shida, tabu na ajali za kila siku hadi siku wanapata ajali, atatusaidiaje sisi wananchi wa Mtopepo ili tusalimike na ajali hizo za kusudi tunazofanyiwa na madereva wetu wa magari ya michanga na daladala.

Mhe. Naibu Spika, sina mengi naomba kuunga mkono hoja, lakini naomba Mhe. Waziri, akija aje kunambia atatusaidiaje. (*Makofi*)

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Shaurimoyo nikushukuru kwa kunipa nafasi hii

nikaweza kutia tia nyama kidogo katika hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwanza mchango wangu wa mwanzo nataka niwaombe sana Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwamba, bajeti hii tuiunge mkono kwa umoja wetu, tena tuiunge mkono kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, ninazo sababu za kusema hivyo, kwa sababu wizara hii kwa kweli wamefanya kazi kubwa sana na ukiangalia kiasilimia kwa Zanzibar karibu barabara zote kuu za Unguja na Pemba Mhe. Naibu Spika, karibu zimekamilika, kwa kweli zilizobakia ni chache. Kwa hivyo, tuunge mkono hotuba hii ili sasa tumpe nafasi Mhe. Waziri, akamilishe hizo barabara kubwa zilizobakia halafu sasa aje katika kuunganisha barabara za vijiji kwa vijiji.

Mhe. Naibu Spika, nataka Mhe. Waziri wa Fedha anisikilize vizuri sana kwa sababu kitabu hichi ukiangalia katika wizara ambazo zinatengewa mafungu makubwa sana katika bajeti ni Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi. Lakini fedha hizi zote sio kwamba anazo Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Miundombinu. Fedha hizi nyingi ziko Wizara ya Fedha lakini na yengine ziko Mfuko wa barabara. Kwa hiyo, kunatakiwa mashirikiano makubwa sana baina ya Wizara hii ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi na Wizara ya Fedha.

Mhe. Naibu Spika, tukiangalia historia takribani miradi mikubwa mikubwa mingi ya wizara hii, bajeti yake ya mwanzo inayoletwa inakuwa ni tafauti na bajeti ambayo inamalizia. Ukiangalia Mhe. Naibu Spika, kumbukumbu katika mradi wa *Apron* na *Taxiway* ya Uwanja wa Ndege wa Zanzibar, mwanzo ilikuwa karibu bilioni sitini na tano lakini mradi ulimalizia karibu na bilioni thamanini na moja.

Lakini vile vile ukiangalia mradi wa ujenzi wa fensi ya Uwanja wa Ndege wa Zanzibar ilianza karibu bilioni nne lakini ulimalizia karibu bilioni saba. Lakini vile vile ukiangalia ujenzi wa Uwanja wetu wa Ndege *Terminal II* ulinza karibu bilioni sabini lakini utamalizia karibu bilioni mia moja na arubaini mpaka arubaini sita, karibu mara mbili. Lakini vile vile Mhe. Naibu Spika, kamati yangu kwa bahati nzuri iliwahi kupata nafasi ya kutembelea kisiwa cha Pemba kabla ya bajeti na tulikwenda kwa sababu kulikuwa na manunguniko kidogo kuna barabara ilijengwa kidogo ikawa na matatizo lakini vile vile kulikuwa na madai ya mkandarasi.

Baada ya kwenda kufanya utafiti Mhe. Naibu Spika, tukagundua kwamba wakati mwengine ucheleweshwaji wa fedha kutoka Wizara ya Fedha unasababisha wakandarasi kudai malipo halafu yanakuja na *interest* na ukiangalia hoja zao Mhe. Naibu Spika, zinakuwa za msingi kwa sababu mikataba ipo, lakini kunapokuja na *delay* hapo Mhe. Naibu Spika, ndio pale utakuta kunakuja na *interest* na vingine. Lakini vile vile kuna zile *additional works*, hizi hazina tatizo zimo katika kuboresha. Lakini tatizo kucheleweshe kutoa fedha halafu kuna na masuala ya *interest*.

Sasa hili ndio maana nikasema kwamba naomba sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mhe. Waziri wa Mawasiliano basi wawe karibu sana na kwa sababu sisi tulichogundua kulikuwa na udhaifu hasa katika zile barabara za Pemba ambayo Wete/Konde na Wete/Gando mpaka sasa hivi kuna madai ambayo tumejaribu kumshauri Mhe. Waziri na tunamshukuru Mhe. Waziri wetu ni msikivu sana, suala lile tena alituwekea na *time limit* ya kwamba ataweza kulishughulikia, lakini yeye ni mpya sasa tuangalie historia na yeye yasijekumkumba yale yale ambayo yaliwakuta hao wenzake waliopita kwamba, inapifika pahala inatolewa *certificate* ya malipo zaidi ya *certificate* tatu na malipo hayajafanyika, hapo lazima kutakuwa na tatizo. Kwa hiyo, panapotokea matatizo kama haya mawaziri wenyewe; Waziri wa Mawasiliano na Waziri wa Fedha wakae ili matatizo kama haya yasije kujitokeza huko mbele.

Lakini jengine Mhe. Naibu Spika, katika hilo hilo nataka nimpongeze sana ujenzi ambao uliofanywa katika barabara za kule Pemba. Lakini katika mradi wa barabara za Pemba tuliambiwa kuwa kuna barabara tatu; Wete-Gondo, Wete-Gando na Wete-Chake. Hii barabara ya Wete-Chake mpaka sasa hivi bado na kwa kweli hali yake ni mbaya sana na sisi kutokana na raha tuliyopita na kamati tukaona zile barabara nyengine zilivyokuwa zimejengwa vizuri katika kiwango bora, barabara ya Wete-Chake na Wete-Gando, sasa wakati wa kurudi tukasema hebu tupite hii ambayo haijajengwa ili sasa tupate na ladha na hii barabara mbovu. Kwa kweli barabara ni mbovu sana.

Sasa katika Bajeti Kuu ya Serikali mnakumbuka kuna fedha zilitengwa karibu bilioni moja na milioni mia saba kwa ajili ya Barabara Wete-Chake kama fedha za kulipa fidia. Lakini katika kitabu nimejaribu kuangalia sasa hivi ukurasa wa 41, kiambatanisho namba 2, tunaambiwa ujenzi wa barabara Wete-Chake kilomita 22.1 imetengewa bilioni moja milioni mia tatu na thamanini, kwa nini? Kwenye Bajeti Kuu wa Serikali nakumbuka tumetenga karibu bilioni 1.7, huku kwa nini zikawa zimepungua? Sasa hili kidogo itabidi tuje kufanya *cross-check* katika Bajeti ya Serikali na katika hii Mhe. Waziri.

Lakini hapo pia nilikuwa namuomba Mhe. Waziri wa Fedha, kama nilivyosema Mhe. Waziri wa Mawasiliano, yeye fedha hana fedha zinatoka Wizara ya Fedha moja kwa moja. Kwa hiyo, katika mchango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambao mchango huu ndio unakwenda kulipa fidia ili ile barabara ianze huo ujenzi. Nilikuwa namuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha, mara tu baada ya kupitisha bajeti kama hali inaruhusu basi zianzwe kutangalizwa ili wale wananchi kule waweze kulipwa fidia ili sasa ile barabara nayo iweze kukamilika ujenzi wake.

Kwa sababu kila siku zikienda tunajua gharama za vifaa zinaongezeka, lakini vile vile hii barabara inawezekana pengine kwa mwaka huu wa fedha isikamilike. Lakini zikitoka mapema hizi fedha ile barabara tunategemea inaweza ikakamilika mapema. Lakini pamoja na yote kwa kweli tunapongeza jitihada kubwa za ujenzi wa barabara ambazo zinazoendelea hivi sasa.

Mhe.Naibu Spika, nimfarijaka sana baada ya kupata taarifa kwamba barabara ya Mwanakwerekwe-Fuoni tayari wamekwisha kutoa tenda kwa ajili ya ukamilishaji wa utiaji wa lami, hatua ya mwanzo kwa kweli imekamilika lakini wananchi walikuwa wanapata tabu sana. Kwa kweli sina haja ya kusema maneno mengi kwa sababu tumeona zile kazi ambazo za uwekaji mabomba ambazo kazi zinafanywa na *ZAWA*. Isipokuwa tunaomba Mamlaka ya Maji kwa sababu waswahili wanasema "Anapochelewa ng'ombe wa mbele, unamchapa bakora ng'ombe wa nyuma".

Wizara ya Miundombinu barabara tayari wameshaanza kujenga lakini fedha haziko kwao, fedha ziko katika Mfuko wa barabara. Sasa mimi naomba inapokuja miradi kama hii basi tunaposema tu tunaanza basi zile fedha tayari ziko *stand by* kwa chochote kinachotokezea ili kukimbia hii *delay* ambao inatusababishia matatizo mengi. Barabara ile kwa kweli imejengwa kwa nia njema na serikali, lakini ilifika pahala wananchi wamekosa imani, wanasema matusi wakati mwengine, kama ukipanda daladala kwa sababu wakati mwengine na sisi pamoja na kuwa tumepewa fedha za kununulia gari lakini wakati mwengine ili upate taarifa sahihi kwa wananchi inabidi upande daladala kidogo usikilize yale matapiko. Lakini mimi nadhani Mhe. Waziri, akija kuwathibitishia wananchi kwamba barabara ya Mwanakwerekwe-Fuoni itakamilika katika kipindi kifupi kijacho, naamini yale maneno yatakuwa yamemaliza.

Lakini hapa nilikuwa na ombi pamoja na kwamba ni Mwenyekiti wa Kamati, lakini pia ninayo nafasi ya kuisaidia mchango mwengine vile vile. Ile barabara inamalizia pale Fuoni kituo cha Polisi. Kwa nini Mhe. Waziri, tusiimalize tena

mpaka kule ambako kulikokusudiwa *roundabout* ya Jumbi. Kwa sababu unajau wakati mwengine tunarejea umo kwa umo kwa kweli haileti ladha sana. Sasa mimi nilikuwa naomba kama Mfuko wa barabara fedha zipo mimi naomba Mhe. Waziri, tufanye *extension* ya barabara ile ili tuweze kuikamilisha halafu sasa tena tusirejee tena pale na tuangalie maeneo mengine.

Lakini kwa kweli kazi inaendelea vizuri na tunakuombea dua Mhe. Waziri, upate nguvu na afya njema pamoja na Naibu wako Waziri na watendaji wako ili muweze kukamilisha yale malengo yaliyokusudiwa.

Mhe. Naibu Spika, katika hichi kitabu kimeelezwa zile barabara ambazo zinazotegemea kujengwa. Mhe. Naibu Spika, nashukuru sana baada ya kuona kwamba katika hizi programu za ujenzi wa hizi barabara nyengine za kuunganisha maeneo kuna barabara ya Fuoni-Kombeni. Mhe. Naibu Spika, barabara ile ya Fuoni-Kombeni kwa kweli kama itajengwa itaweza sana kuwasaidia wananchi kupita katika mzunguko mkubwa sana na vile vile kupunguza lile zogo katika barabara ya Fuoni.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu barabara ile unaweza ukatokea upande wa Kaskazini na hii nakusudia mpaka na ile barabara inayoka Mwera pale kujia hapa Fuoni meli 7. Tena ile ya Mwera-Fuoni imeshatiwa kifusi kizuri pale waende wakakamilishe kuweka lami, wakikamilisha na hii barabara ya Fuoni-Kombeni kwa kweli Mhe. Waziri, bajeti inayokuja wewe huna haja hata ya kusoma bajeti, ukija hapa tunakupigia makofi shughuli inakwenda mambo yanakuwa mazuri. Na kwa ninavyomua Mhe. Waziri...

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa, muda wako umekwisha.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Naomba nimalizie la mwisho kidogo la Jimboni kwa ruhusa yako na mimi ni Mwenyekiti.

Mhe. Naibu Spika, unajua ninapokuwa kwenye kamati huwa sitaki kuzungumza *conflict of interest* kwa barabara yangu ya Shaurimoyo hadi Daraja bovu. Mhe. Naibu Spika, barabara ile ina ahadi ya Maraisi wawili Dkt. Amani Abeid Karume na Dkt. Ali Mohd Shein, si vizuri sana kurejea ahadi za Maraisi hapa ikawa hazitekelezwi, kwa kuwa nina nafasi kwenye kamati nitashauriana na Mhe. Waziri na Naibu Waziri, kwa bahati nzuri barabara ile iliwahi kutiwa mpaka Ilani ya Uchaguzi wa mwaka 2010 na kwa kuwa wizara hii wamepewa makada, nafikiri hawataichezea sana Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, naamini wataweza kufanya kazi nzuri waweze kukamilisha.

Baada ya hayo machache, kwa mara nyengine tena nawaomba Wajumbe wote wizara hii tuipitishe kwa asilimia mia moja bila ya hata chembe ya buti moja. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Mhe. Shamata Shaame Khamis: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi mchana huu nikapata fursa ya kuniona na mimi nikawa miongoni mwa wachangiji katika hotuba ya bajeti ya wizara hii.

Mhe. Naibu Spika, awali ya yote sina budi kwanza nitangulize shukurani zangu kwa Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia bado nikiendelea katika hali ya afya na salama na uzima kabisa na Waheshimiwa wengine tukiwa tunaendeleza majumu yetu.

Lakini kwa haraka haraka nichukuwe fursa hii kuwapa pole wananchi wa Jimbo la Micheweni kwa mashaka mengi ambayo wanayapata, naomba tu Mwenyezi Mungi awape subira katika kipindi hichi hususan baada ya kumalizika kwa uchaguzi wa marudio.

Baada ya hapo naomba niende moja kwa moja katika kaunza kuchangia. Kwanza kabisa napenda nichukuwe fursa hii kusema kwamba, wananchi wa Jimbo la Micheweni mimi wamenituma kuja kuwatumikia na moja ni kupaza sauti zao.

Kwa mara ya kwanza nadhani leo nitaweza kusema kwamba katika kipengele hichi cha ujenzi wa barabara au matengenezo ya barabara mimi niseme wazi wazi kwamba mimi sitounga mkono Hotuba ya Bajeti ya Wizara hii. Na kwa nini sitounga mkono hotuba ya wizara hii kutoka na sababu zangu ambazo ninazo ambazo wananchi wangu wa Jimbo la Micheweni wametaka niziwasilishe kwa Mhe. Waziri. Wamenambia kwamba wana imani kubwa na waziri ambaye amepewa wizara hii na Naibu waziri wanawapenda sana na mimi binafsi nasema kwamba nakipenda sana Chama cha Mapinduzi, naipenda sana wizara na viongozi wake pamoja na viongozi wengine wote. (*Makofi*)

Lakini ifike wakati sasa tuone kwamba serikali inafanya mambo kwa mujibu ambavyo tumedhamiria ama tumeahidiwa. Wananchi wa Jimbo la Micheweni kwa miaka mingi sana wamekuwa wakichagua viongozi wao mbali mbali Wawakilishi katika awamu tafauti, sasa mimi mwaka huu wakati nilipokuwa majukwaani niliwaahidi kwamba kwa mwaka huu naamini kwamba barabara za Micheweni zitajengwa.

Lakini nilipoingia hapa ilikuwa nafuatilia kuanzia Ilani ya Chama cha Mapinduzi, nikaangalia hotuba ya Mhe. Rais aliyoisoma hapa Barazani, nikapekuwa mpaka nikaangalia na hotuba ya bajeti ya wizara hii. Sijaona hata sehemu moja, hata zile barabara za ndani au katika mpango wowote sijaona sehemu ambayo imegusa barabara za Micheweni.

Mhe. Naibu Spika, napenda kusema kwamba wananchi wa Micheweni wamekuwa wakijitahidi sana katika kuiunga mkono Ilani ya Chama cha Mapinduzi, lakini vile vile kuiunga mkoni Serikali ya Mapinduzi kwani walijitahidi sana katika ushindi huu wa kishindo katika Mkoa au katika Jimbo ambalo katika Mkoa wa Kaskazini wamejitokeza kwa wingi zaidi ukilinganisha na Majimbo mengine ni Jimbo la Micheweni.

Lakini si hilo tu, wananchi wa Jimbo la Micheweni wana rasilimali ya mawe au wana maliasili ya mawe na fusi. Sasa hivi barabara zote zinazojengwa katika Mkoa wa Kaskazini Pemba tokea kuwepo kwa ulimwengu huu barabara hizi zinajengwa, na majengo mbali mbali yanajengwa kwa kutumia maliasili kutoka Micheweni, lakini inanishangaza sana na najiuliza wananchi wa Jimbo la Micheweni kuna tatizo gani ambalo kila awamu zinazokuja, viongozi waliopita wanapiga makelele lakini jambo hili halijafanikiwa mpaka leo. Imekuwa ni sehemu moja ambayo ikizungumzwa masuala ya umaskini, inaonekana ni Micheweni, lakini hii pia inasababishwa na kutokana na kutokuwepo kwa barabara katika maeneo ya Jimbo la Micheweni.

Sijaona hata ahadi ya kifusi kwenye bajeti hii. Naomba Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba Jimbo la Micheweni ndilo ambalo linasaidia kujenga majengo mbali mbali kwenye Kisiwa cha Pemba, na barabara zote za Mkoa wa Kaskazini Pemba zimejengwa kwa kupitia maliasili kutoka Jimbo la Micheweni.

Leo kilichobakia rasilimali tuliyonayo kule au uasili tulionao sasa hivi ni kwamba mashimo makubwa yaliyojaa katika ardhi ya Micheweni, ambayo inapelekea wananchi na wao pia kuweza kuitumia fursa kuanza kuichokonoachonoa mawe na hiyo angalau kupata rizki ili kabla ya ile maliasili haijamalizika.

Niseme sasa wananchi wa Jimbo la Micheweni wamesema wamechoshwa na hali hii. Naiomba serikali sikivu kwa kupitia Waziri na Naibu Waziri, kwamba sasa ni muda wa kutafuta namna hata kama kwamba bajeti hii haikuonesha kipengele ambacho au sehemu ambayo itaweza kufanikisha jambo hili.

Sasa wananchi wa Jimbo la Micheweni nao wanahitaji barabara, na ninaomba nisiambiwe ni barabara ya kifusi, ni barabara ya lami ya viwango. Kwa nini wao ambao ndiyo wanazozijenga, wanaozisaidia kuzijenga barabara hizi na miundombinu hii ya Pemba, maeneo mengine yaonekane umaskini unapungua, wao maliasili hii inaondoka na wao wanabakia mashimo matupu, hatimaye hakuna, wao hawapati barabara ambazo zina viwango.

Kwa hivyo naomba Mhe. Naibu Spika, kwamba Waziri atakapokuja aniambie ni lini, na atamke hadharani wananchi wa jimbo langu wamsikie ili kuona kwamba sasa muda umefika wa wananchi wa Jimbo la Micheweni nao kupata barabara yenye viwango.

Na ninaomba nimkumbushe tu kwamba Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri barabara ninazozizilia hapa ni barabara ambayo inatoka Micheweni Maziwa Ng'ombe, inayotoka Gongoni Kiuyu Mbuyuni, Micheweni Shumba Mjini na Msituni mpaka Msasani kupitia mjini Wingwi.

Mhe. Naibu Spika, hizi ndizo barabara ambazo zinakuwa katika jimbo langu ndiyo wadau ambao wanazisaidia barabara nyengine kuweza kufaidika na maliasili iliyoko maeneo yale.

Mhe. Naibu Spika, inaniuma sana kwamba kuona kuwa unakuta unasikia kuna kilomita 35 ambazo barabara za Ole/Kengeja, halafu ujenzi wa Wete/Chake Chake wakati wananchi wa Jimbo la Micheweni hawana hata bidhaa moja ambayo hawahitaji kusafirisha.

Wale wavuvi ambao wanavua katika jimbo hili ni lazima wakishapata samaki wao wanahitaji wasafirishe barabara hazipitiki, hususan kipindi cha mvua. Inanisikitisha sana kwa sababu viongozi ambao wa awamu mbili; Marais wawili wameshafika Micheweni, na baadhi yao wameshatoa ahadi. Moja katika kipindi ambacho kulizuka mgogoro baina ya wanakijiji wa Mjini Wingwi na Maziwa Ng'ombe, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein alikutana na wanavijiji hao sehemu mbili hizo, na baada yake ninadhani kazi hii au mazungumzo haya yalifanyika Ikulu na Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini alikuwemo katika kikao hicho. Moja katika jambo alilolalamikiwa na wananchi wa Jimbo la Micheweni ni kutokana na maafa makubwa wanayoyapata wananchi wa Jimbo la Michweni kwa kutokea maafa ya kusafirisha wagonjwa, na imeshawahi kutokea kwamba mgonjwa anayesafirishwa kupelekwa kijiji kimoja kupelekwa Hospitali ya Wilaya, huweza gari likakwama njiani kutokana na barabara imejaa maji na

hatimaye mgonjwa akafa hapo hapo kabla ya kufika eneo ambalo alitarajiwa kwenda kufanyiwa matibabu.

Vile vile kuna mfanyabiashara mmoja ambaye alikuwa anajishughulisha na shughuli za biashara ya kuuza nazi naye pia aliweza kupata ajali ndani ya barabara hii na kuweza kufa hapo hapo. Na mwengine pia ambaye alitokea katika familia yangu, aliweza naye kupita wakati anakwenda baharini akaendesha baiskeli akaanguka kwenye shimo na baadae akagongwa na msumari wa baiskeli na ikawa moja kwa moja akaondoka duniani. Haya ni maafa makubwa ambayo yamekuwa au ni madhara ambayo yameweza kujitokeza kupitia barabara hizi za ndani katika Jimbo la Micheweni.

Mhe. Naibu Spika, ninamuomba sana Mhe. Waziri endapo ataniahidi ninadhani na mimi nitaungana na wenzangu katika kuunga mkono baadae lakini siyo sasa hivi, sasa hivi ninasimama kwamba siwezi kuunga mkono bajeti au hotuba ya bajeti ya wizara hii. lakini tukija katika masuala ya usafirishaji Mhe. Naibu Spika, mimi niipongeze wizara kupitia kitengo hichi au Shirika la Usafirishaji kwa kujitahidi sana kwa kuliona kuwa sasa hivi tumepata meli ya MV Mapinduzi ambayo inafanya kazi nzuri. Na kwa kweli Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein anahitaji kupongezwa kwa asilimia kubwa mno, kwa kazi nzuri ya kuweza kufikiria kuona kwamba wananchi wake wanaweza kutatuka na kero ambazo na maafa makubwa tuliyoweza kuyashuhudia yakitokea baharini miaka hadi miaka. *(Makofi)*

Pamoja na kwamba meli hiyo tunayo na nzuri, lakini ningeshauri sana kwamba tuweke mkakati zaidi katika kuona kwamba meli hii inatunzwa vizuri na hatimaye vile vile...

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa kidogo umebakiza dakika tano, lakini naomba nimpishe Mhe. Mwenyekiti aweze kuendelea na kikao. Mhe. Mwenyekiti karibu.

Hapa Mhe. Mwenyekiti (Shehe Hamad Mattar) alikalia kiti

Mhe. Mwenyekiti: Endelea Mheshimiwa.

Mhe. Shamata Shaame Khamis: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niendelee katika suala zima la usafiri. Kama nilivyosema kwamba meli ya MV Mapinduzi imeletwa katika kuwakomboa wananchi wetu kwa wasafiri kati ya Unguja na Pemba.

Ni jambo zuri na ninalipongeza sana lakini nilikuwa ninashauri kwamba wizara iangalie kwa kina zaidi katika kuongeza hadhi ya meli yetu kwa kuifanyia matengenezo ambayo yanayostahiki, lakini sambamba na hilo ni moja kwamba wasafiri wanapata shida sana wakati wa usafiri, hususan katika muda wa kupanda na kushuka.

Mhe. Mwenyekiti, meli yetu hii ni kwamba ina mlango mmoja ambao wakati abiria wanashuka basi wanakuwa wanasongamana sana. Hatimaye kunaweza kukapelekea mazingira ambayo ya kusababisha afya za wasafiri kuweza kuleta udhaifu fulani.

Hivyo ninashauri wizara ijitahidi katika kuangalia uwezekano kuona kwamba tunaongeza mlango mwengine ili abiria waweze kupanda kwa ufanisi zaidi na kushuka kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini vile vile katika upande mwengine niishukuru sana wizara kwamba MV Maendeleo sasa imefanya kazi kuelekea Tanga. Ni jambo moja la msingi sana, imeweza kutusaidia katika hali hii kwa sababu kila mwaka inapofika tunasikia kuwa ajali za baharini zinakuwa zikitokezea. Hivyo naiomba wizara iongeze ufanisi zaidi katika suala zima la kuona kwamba linaelekeza nguvu zake pia kwa Mkoa wa Kaskazini Pemba. Kwa sababu Mkoa wa Kaskazini Pemba ni sehemu ambayo kwa kweli ni kiunganishi kizuri na kina wasafiri wengi kuelekea Tanga ambapo kunapelekea vile vile suala zima la kuongeza mapato linaweza likatokea zaidi kwenye bandari hii ya Wete. Kwa hivyo ningeomba sana kwamba wizara iangalie utaratibu mzima wa kuona kuwa zile juhudi ambazo imesema itazifanya katika kuitanua au kuifanyia ukamilishaji wa bandari ya Wete uweze kufanikiwa, na hizi meli pia nazo ziweze kufanya *route* angalau Tanga kuja Wete. Kwa sababu ukiangalia kwanza pale sasa hivi tumeshakuwa na Manispaa. Tuna Manispaa sasa hivi ya Mji wa Wete. Nadhani pamejengwa soko kubwa, na soko lile linahitaji bidhaa, na bidhaa kwa urahisi zinahitaji ili kuepusha kwamba bidhaa ziende kwa wakati na kwa usalama zaidi, ni vyema tuelekeze nguvu katika kuona kwamba bandari ya Wete inafanya kazi sambamba kwa *route* ya Tanga ili kuweza kusaidia kuona kwamba tunaongeza uzalishaji mzuri kwenye soko letu, lakini vile vile mapato na ile azma ya serikali kuifanya Wete ni Manispaa inaweza kuleta tija zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo mimi nasema kama nilivyosema kuwa sitounga mkono bajeti hii kwanza mpaka nitakapopata ufafanuzi kupitia Waziri, kwamba kuona kuwa na mimi sasa anapeleka jicho katika Jimbo langu la Micheweni na baada ya hapo nikishapata maelezo sitokuwa na haja ya

kupiga buti, lakini ninamuomba sana Mhe. Waziri afikie hapa atoe tamko ili wananchi wa Jimbo la Micheweni walionituma, walioniambia kwamba nisiunge mkono waweze kuwa na matumaini na mimi na vile vile wawe na matumaini mema na serikali yao.

Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Shamata Shaame Khamis. Sasa anayefuata ni Mhe. Suleiman Makame Ali na baadaye atafuatia Mhe. Wanu Hafidh Ameir na baadae Mhe. Miraji Khamis Mussa ajitayarishe.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi ninashukuru kwa kuweza kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia kwenye hotuba hii ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza napenda nimpongeze Mhe. Waziri Balozi Ali Abeid Karume kwa kuteuliwa kuwa Waziri katika wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, nimtake tu ushauri Mhe. Balozi Karume. Mhe. Rais Magufuli Rais wetu mpendwa alikuwa Waziri kwenye wizara kama hii. Hebu Mhe. Balozi Ali Abeid Karume wawekee vitu wananchi barabara wakipita watandike walale. Pengine huenda Mwenyezi Mungu na wewe akakujaalia mwaka 2020 ukaipata nafasi kama hiyo hapo. Ninakuombea dua *in shaa Allah*. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, niende masuala ya barabara. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri alizungumza hapa kuhusu barabara ya Wesha/Mkumbuu.
Mhe. Mwenyekiti, mimi nimuombe sana Mhe. Waziri barabara hii ya Mkumbuu ni barabara muhimu kati ya barabara zilizo na umuhimu na hii ni mojawapo, kwa sababu roho ya Pemba ni Ndagoni. Kule ndiko uliko umeme kutoka Tanga, na nilisema hapa kwamba mnamo 2013 wale walinzi wetu walifika kuzama baharini kwa sababu ilikuwa njia ile haipitiki. Sasa hivi tunashukuru ina kifusi lakini kutokana na mvua zilizoendelea kuonyesha na zinazoendelea kunyesha barabara hii baadhi ya maeneo yameshaanza kuchimbuka. Kwa vile ninamuomba sana Mhe. Waziri aliangalie hili, na aiangalie kwa jicho la huruma barabara ya Ndagoni. Hivyo ninamuomba sana Mhe. Waziri aangalie kwa jicho la huruma kwenye barabara hii.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, pia vile vile nimuombe Mhe. Waziri nina barabara katika jimbo langu kusema la ukweli, nina barabara yaani ukiacha barabara ya Chake Chake iliyopita njia kongwe Ziwani ikaenda zake mpaka Wete ningesema

Jimbo la Ziwani hakuna barabara hata sehemu moja. Nina barabara ya Birikau haipitiki, hata punda barabara ile hapiti, haipitiki barabara ile. Nina barabara ya Gombani Michungwani barabara ile nayo haifikiki, ni mbovu. Kwa hivyo ninamuomba Mhe. Waziri na hizo pia aziangalie kwa jicho la huruma, lakini zaidi hususan kwa sasa hivi aangalie kwa barabara ya Ndagoni kwa sababu roho ya Pemba ipo kule. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, pia napenda nimuulize Mhe. Waziri hapa anipe jibu akija kutoa ufafanuzi kwenye suala la leseni. Mhe. Mwenyekiti, kwenye suala hili la leseni kuna watu wanaendesha gari kama ilivyokuwa serikali hii au nchi hii ni ya babu yao, hawana leseni, wanaendesha gari lakini sasa mimi cha kushangaza kwamba mtu huyu hana leseni, lakini anapotokezea akapata ajali hutoa hata milioni mbili, tatu, nne, tano kwamba kesi isiende mbele. Lakini sasa shilingi laki moja ya kutafuta leseni huwa mtu huyo anashindwa.

Mhe. Mwenyekiti, hapa nitaomba jibu ni madereva wangapi waliokwisha kamatwa na kupelekwa Mahakamani kwa uzembe huu wanaoufanya.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitaki niseme mengi sana, kwa sababu wenzangu wengi wameshachangia na mara nyingi mimi nikisimama huwa sisemi mengi sana.

Kwa hivyo mimi naiunga mkono hotuba huu kwa asilimia mia moja na simnyimi hata asilimia moja.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri ninamuunga mkono kwa hotuba hii asilimia mia moja.

Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mheshimiwa. Sasa anafuatia Mhe. Wanu Hafidh Ameir na baadae atafuatia Mhe. Miraji Khamis Mussa.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kukutana hapa leo kujadili hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji. Lakini pili nikushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niseme machache katika hotuba hii. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuanzia naomba nianze kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake wa hotuba, lakini pongezi zaidi ziende kwa

watendaji ambao walikuwa nyuma yake katika kuona kwamba hili linafanikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze katika Shirika la Bandari. Ninapongeza sana juhudi za serikali kuona kwamba watu wanapata huduma hii ya usafiri na inawasaidia katika shughuli zao za kujiendeleza kwenye shughuli zao la siku.

Mhe. Mwenyekiti, kilio changu katika Shirika la Bandari ni ukaguzi wa mizigo bandarini.

Mhe. Mwenyekiti, kumekuwa na usumbufu mkubwa sana kwa wanaotumia bandari hizo kutokana na utaratibu ambao unaotumika pale kukagua mizigo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini hata wale wale wakaguzi wenyewe sifikirii nao wako salama, kwa sababu ukaguzi wenyewe unatumika kwa kufungua mifuko na mabegi ya watu na kutia mikono bila ya *gloves* na bila ya chochote, na haiwi ukaguzi tena unakuwa ni upekuaji.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, naomba hili kama wizara wakishirikiana na Shirika la Bandari wafanye namna ili kuona kwamba hili tatizo ambalo limeshakuwa sugu sasa hivi, kwa sababu kwanza linaleta msongamano pale lakini pia ule utaratibu unaotumika Mhe. Mwenyekiti, haupo vizuri. Hivyo naomba sana Shirika nimeona katika malengo yao ya mwaka 2016/2017 wamejiwekea kuimarisha ulinzi na usalama bandarini pamoja na kununua vifaa vya kukagulia mizigo ya abiria.

Kwa hivyo naomba sana hili lifanyike na litimizwe katika kipindi hichi cha bajeti ili kuona kwamba ule usumbufu pale unaondoka. Sasa hivi *population* inayoingia pale imeshakuwa kubwa. Watu wawili watatu kukaa pale na kuanza kupekua mabegi ya abiria wote wanaoshuka pale, kwa kweli inakuwa ni usumbufu. Kwanza wanauchukua muda wetu lakini pia haipendezi upekuzi wenyewe, kwa sababu watu wenyewe watie mikono kwenye mabegi. Watu siku hizi wanachukua mambo tofauti kwenye mabegi, watakuja kukutana na mambo huko yaje yawadhuru wao. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, lakini jengine ambalo silioni kama lina mantiki, kwa sababu tunakotoka kwenye *point of exit*, kwa maana ya kwamba kule bandari ya Dar es Salaam kuja Zanzibar, kule tayari tutakuwa tumeshachekiwa, tunachekiwa tena tunakaguliwa kwa mashine. Sasa umetoka kwenye kukaguliwa na mashine unakuja Zanzibar unaanza kupekuliwa begi. Sasa ile mashine au hii mikono yao ina *x-ray* sijui kwa wale wakaguzi. Maana umetoka kwenye mashine na

bado unakuja Zanzibar unakaguliwa kwa mikono. Sasa sijui ipi ipo *perfect* zaidi, hiyo mikono yao au ile mashine unayotoka kule. Kwa hivyo mimi ninasema kama Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Simai Mohamed Said siku moja amesema hapa haoni mantiki kwamba umetoka kwenye *point of exit* umekaguliwa, *point of entry* unakaguliwa tena. Tena umetoka kukaguliwa kwa mashine unakuja kukaguliwa kwa mikono.

Mhe. Mwenyekiti, hili ni tatizo na ninaomba sana wizara ilifanyie kazi, tumeshachoka, yaani usumbufu mkubwa, ina-*consume time* sana mukifika pale.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, lakini jengine nimeona kwamba kuna mashirikiano mazuri baina ya Wizara na Taasisi za muungano ambazo zipo Tanzania Bara, ambazo kwa namna moja au nyengine majukumu yao na Wizara ya Miundombinu yanafanana. Kwa hivyo nipongeze ushirikiano huu na niwaombee kwamba uendelee kuwepo lakini uwe ni ushirikiano wa manufaa, siyo ushirikiano *for sake of* ushirikiano, uwe ushirikiano ambao unaleta manufaa kwetu pamoja na kwa wao. Ninasema hili kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, tunaona jinsi gani kule kwao kunavyoimarika kama sehemu za bandari na viwanja vya ndege. Kwa hivyo haya mashirikiano yaliyokuwepo yalete pia uimarishaji huku katika nchi yetu ya Zanzibar ili kuona kwamba angalau na sisi tunafikia vile vigezo ambavyo wenzetu wengine wanavyo.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, naomba niingie katika Mamlaka ya Viwanja vya Ndege. Ninapongeza sana juhudi ambazo Mkurugenzi wa Mamlaka anachukua kuona kwamba viwanja hivi kwa namna moja au nyengine vinatoa huduma katika *level* ambayo inayotakiwa kutolewa.

Mhe. Mwenyekiti, lakini hapa nina sikitiko kubwa sana katika utaratibu wa *luggages collection*, pale sehemu ambayo *arrivals* wanapofika wanachukua mizigo yao.

Mhe. Mwenyekiti, *wallahi* inatia aibu. Mimi juzi nimeshuka pale kulikuwa kuna ndege ya *International flight* imeingia na mimi nimeingia na *domestic flight*, nafika pale nasubiri mzigo wangu nimekuta wazungu na wao wamejipanga na wao wanasubiri mizigo yao, wanachoki-*discuss* pale Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa ninaona aibu mimi, yaani nimeziba uso hivi chini kwa yanayozungumzwa.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, niwaombe sana pale watafute *convey belt* waweke, kile kitendo kinatutia aibu, ulimwengu wa sasa wa *dot com* mtu

anashuka katika kiwanja cha ndege anasubiri begi lake libebwe kutoka kule atupiwe bwa! ndio achukue, wakati wenzetu wameweka *belts* zile ni rahisi inakuwa. Kwa hivyo, ninaomba kama wanavyoimarisha mambo mengine ni vyema na viwanja vya ndege pale hasa pale katika *point of luggage collection* wakaiboresha ile sehemu kwa sababu kwa kweli inatia aibu.

Mhe. Mwenyekiti, yaani haya mambo tunayoyafanya ya kizamani sana wanatushangaa sana yaani, wenzetu wameshapita zamani sisi ndio kwanza tuko pale pale. Kwa hivyo, niombe sana Mamlaka ya Viwanja vya Ndege hili walifanyie kazi, lakini pamoja na kulifanyia waje watoe maelezo hapa Mhe. Waziri akija aje atoe maelezo, wana mpango gani katika kuona hili linafanikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naamini kwamba hili litafanyiwa kazi na ile *embarrassment* ambayo inatukuta iwe angalau katika kipindi hichi cha Mhe. Balozi na mimi namuamini yeye ni mtu ambaye yuko *very expose* hata Mkurugenzi yuko *very expose* yale mambo ya zamani sana ya kutupiwa begi, umepita *point of arrival* unatupiwa begi unabeba. Kwa hivyo, naomba sana wayafanyie kazi ili kuona kwamba angalau na sisi tunanyanyua nyuso mbele za watu tuna-*airport* ambayo tunaweza tukasema ni *international*, ule utaratibu unaofanyika pale ule sio *international* hata kama tunasubiri hii *terminal* nyengine imalizike, lakini acha tuboreshe hichi ambacho tulichonacho kabla hatujaingia katika ile nyengine.

Kwanza lile jengine nalo hata halitambulikani linamalizika lini, kila siku tunaambiwa limekosewa sijui muelekeo, sijui jengo linatakiwa liwekwe hivi, mara wengine wanasema sijui lielekee hivi, kwa hiyo hatujui. Kwa hivyo, bora tuboreshe hichi ambacho tulichonacho mikononi kuliko kusubiria lile ambalo tunaambiwa labda litakuwa ndio la kisasa zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, jengine niombe sana haya ambayo nimesema Mamlaka wayafanyie kazi, kwa sababu tumeona kunakuwa kuna juhudi sana za kuboresha hizi *business centers* katika viwanja vya ndege na tunajua kwamba vinaboreshwa *business center* kwa sababu kule kuna mapato na kuna *interest* za watu, lakini katika huku kuboresha ambazo zinapatiwa pale kidogo ile *speed* ya kuboresha inakuwa ndogo, kwa hiyo tunaomba sana waboreshe hayo ambayo tumeyasema.

Mhe. Mwenyekiti, jengine naomba niingie katika huduma za usafiri wa barabara. Kwanza kabla sijasema naomba nichukue pia nafasi hii kupongeza wizara kwa kazi nzuri ambayo imekuwa inafanya lakini mimi nimekuwa nina

kilio cha siku nyingi sana, na sio mimi na wengine pia wameshazungumzia kwamba hii barabara ya kuelekea Kisakasaka kwenda Machinjioni nadhani ni ya 4 *kilometers* imekuwa imo katika Ilani nadhani tangu ya *ASP* kila Ilani inatajwa, kila Ilani inatajwa, lakini bado barabara ile haijafanyiwa kazi na kila Ilani inayokuja sijui ya mwaka gani, yaani Mwenyekiti tangu ya *ASP* barabara imo, yaani ile barabara imo kwenye Ilani, mpaka leo barabara haijafanyiwa kazi, *please* tunaomba sana ile barabara ifanyiwe kazi.

Kila siku mimi nimeshawahi kuuliza hapa nikaambiwa oh! imetiwa sijui kwenye mradi gani, sijui kwenye mradi gani, mpaka leo kimya, wananchi usumbufu, magari ya abiria hayafiki kule kwa ubovu wa barabara, inabidi watembee kutoka kule ndani waliko mpaka huku juu sijui Kombeni ndio wachukue gari za abiria waende na safari zao, kwa hiyo pia ile inarudisha nyuma maendeleo ya wananchi wanaokaa kule.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo niiombe sana serikali iifanyie kazi hii barabara ili tuondokane na ahadi ambazo zinakuwa hazitekelezeki na tunazitaja katika Ilani zetu. Maana Mhe. Mwenyekiti, ile ilani ni mkataba baina ya serikali na wananchi ambao ndio wapiga kura, mnapowaelezea kitu ambacho kila siku hamkifanyi mnashusha matumaini ya wale wananchi katika serikali ambayo wanaiweka, *please* naomba hili jambo lifanyiwe kazi ili tuone kwamba mambo yanaendelea.

Mhe. Mwenyekiti, lakini jengine katika huduma za barabarani Mwenyekiti nalia sana na usalama wa barabarani. Mhe. Mwenyekiti, hakuna maendeleo ambayo hayana changamoto, lakini hizi taa za *barabarani* wallahi zitatumalizia nguvu kazi ya taifa.

Mhe. Mwenyekiti, yaani kumekuwa na uzembe sana katika mataa haya ya kuongozea barabara hasa hii *point* ya Kwa Mchina yaani imekuwa uzembe mkubwa mno, naomba sana hili kama wizara kama wasimamizi wa usalama wa barabarani pamoja na vitengo vyote ambavyo vinahusika walisimamie uzuri kwa sababu kumekuwa kuna ajali nyingi katika hizi *point* na imekuwa ikipelekea kwamba kupoteza nguvu kazi za taifa hili. Hata sisi Baraza tumeshawahi kumpoteza mtu kwa uzembe ule ule wa pale, uzembe wa mtu mwengine tukapoteza nguvu kazi yetu kutokana na ajali ambayo yule mfanyakazi mwenzetu amepata katika sehemu ile.

Mhe. Mwenyekiti, lakini jengine kwa kumalizia naomba sana na mimi nitoe wito kwa wananchi kufuata sheria za barabarani hasa humu katika sehemu za kuongozea magari katika mataa kwa sababu imekuwa changamoto kubwa sana,

kwa hiyo tunakubali kwamba hakuna maendeleo yanayokuja bila ya changamoto lakini na sisi madereva tupunguze uzembe katika hizi *point* ili kuona kwamba mambo yanakwenda kama yalivyokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mheshimiwa kwa uchangiaji wako. Sasa anafuata Mhe.Miraji Khamis Mussa na baadaye atafuatia Mhe. Salma Mussa Bilali.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi

Mhe. Mwenyekiti: Kwanza subiri Mheshimiwa, naomba ukae. Waheshimiwa maongezi mmeyafanya makubwa kiasi ambacho sauti zinaingiliana, naomba mpunguze maongezi; endelea. (*Makofi*)

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nishukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuwa miongoni mwa wachangiaji wa siku ya leo kwa Wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba moja kwa moja niende tu kwenye programu ya miundombinu na huduma za usafiri wa barabara.

Mhe. Mwenyekiti, katika eneo hili karibu maeneo yote ya ujenzi au miundombinu ya barabara ndio kunakuwa na kasoro kubwa sana, kila Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi akiongea barabara kuna tatizo. Sasa na mimi naomba sana niiombe wizara hususan kwa viongozi walioingia mara hii wawe waangalifu sana katika kukamilisha programu za ujenzi za miundombinu za barabara, yamefanyika mengi, tunaandaa programu wenyewe lakini inafika pahala tunakuja humu majibu tunayopatiwa kuwa Mkandarasi huyu kakimbia, huyu hajamaliza tumemuongezea muda, na sie sie ndio tunao ma-e*ngineer* wa kutuongoza na wa kutuelekeza katika ukamilishaji wa programu hizi. Naomba sana viongozi waliopewa dhamana ya wizara hii tuwe makini sana sana, la si hivyo serikali tutakuwa tunaendelea kuitia hasara katika maeneo haya ya miundombinu ya barabara.

Mhe. Mwenyekiti, niizungumzie barabara ya Jendele - Unguja Ukuu, Jumbi-Mwera, barabara hizi zote zimepewa Mkandarasi mmoja *DB* Shapriya, hivi sasa hivi hayupo naye amesita, serikali hii hii kupitia wataalamu wetu ndio iliyompitisha na kumpa zabuni ile ya ujenzi.

Nimezungumza mwanzo tuwe makini na katika eneo hili umakini umekosekana, kwa sababu leo tumeingia mkataba na Mkandarasi baadaye anatoweka tunafukuzia kwenda kukamata magari yake si jambo la busara sana kwa serikali yetu hii makini kufikishwa katika maeneo hayo na watendaji wetu. Kwa hivyo, naiomba serikali katika eneo hili iniambie ikija hapa kufanya majumuisho imechukua hatua gani ya umalizaji wa ujenzi huo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini la pili kwa kuwa mjenzi huyo ameshindwa, hatua gani serikali imezichukua mpaka kufikia sasa.

Jambo la tatu, kwa sababu tulijaza mkataba nao kwa vyovyote kutakuwa kuna *general conditions* katika *contracts* tulizoziweka ndani ya mkataba ambao tumeujaza. Ningeomba zile ambazo zinailinda Serikali katika eneo hili, kwa hiyo naomba sana *general conditions* nije nizipate ili tuangalie kuna *security* gani ambayo inatulinda sisi kwenye mikataba hii, kwa sababu tusije kuingia katika mikataba ambayo baada ya muda hawa wawekezaji hawa wakandarasi wanaondoka inakuwa ndio tumemalizana nao. Lakini hapo hapo katika mkataba wowote lazima kuna *performance security* ambayo inazuia sehemu ya fedha za mkandarasi, asilimia ngapi katika fungu hili kulizuia au kama hakuna *performance security* ambayo tulikwenda nayo waje watuambie ni kwa nini tuliingia katika mkataba ambao haukuwa na kitu kama hicho.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende sasa katika Bodi ya Wakandarasi ambayo ndiyo inatuzalishia wakandarasi ovyo, wakandarasi ambao hawana uwezo wanakuja kutushughulisha katika mazingira haya, sasa Bodi hii nayo pia iko ndani ya Wizara hii.

Wakandarasi wanakuja wanaomba vibali wa kuwa watumishi ndani ya nchi yetu hii katika maeneo ya ujenzi, ikiwa ya *civil* au *building* lakini wao ndio wanawapasisha. Sasa leo chombo hichi pia tunachokizungumzia cha Bodi ya Wakandarasi pia nayo kimemaliza muda kwa taarifa nilizonazo mimi, akija waziri anambie ni utaratibu gani ambao anautumia wa kuendesha shughuli zao, wakati Bodi yenyewe ina Mwenyekiti tu ambaye yuko *valid,* lakini wajumbe wake hawako *valid,* utaratibu upi? Lakini tokea kuanzishwa kwa Bodi hii pia aje anambie ni leseni ngapi za *Class A* walizozitoa na serikali imepata kiasi gani cha fedha tokea kuanzishwa kwa Bodi hii, kwa hiyo katika *Class A* nijue za *civil* ngapi na za *building* ngapi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini mwisho katika eneo hili namuomba pia waziri aje atuambie fedha ambazo anakusanya zinaingia katika mfuko gani wa serikali, kuna mfuko wa Bodi, kuna mfuko wa Idara au Mfuko Mkuu wa serikali, na

auditing yake ya mfuko huu imefanywa lini? Kwa hivyo, Mhe. Waziri, nakuomba sana kwenye eneo hili uje unipe taarifa hizo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini niende katika eneo la mashirikiano na Taasisi za Muungano. Ameelezea hapa katika kitabu Mhe. Waziri, kuwa tunashirikiana kikamilifu katika maeneo haya ya Taasisi hizi za Muungano.

Naelewa kuwa Taasisi hizi ziko kwenye serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini maeneo mawili naomba niyazungumzie zaidi, eneo la Mamlaka ya Mawasiliano *TCRA* lakini na aneo la Shirika la Posta Tanzania *TPC*.

Maeneo haya kwa kiasi kikubwa wanatoa mapato makubwa sana na lazima Serikali ya Mapinduzi ifaidike japokuwa tuko katika Muungano, kwa hiyo naiomba Wizara itakapokuja kufanya majumuisho itwambie ni asilimia ngapi ya mgao kwa maeneo haya ya serikali inafaidika. Lakini la pili ni kiasi gani cha fedha kimepatikana kwa mwaka huu wa fedha 2015/2016.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa nielekee eneo la Mizingani *Sea Wall Project.* Eneo hili najua kama *client* ni Wizara ya Fedha, wakiwa wahusika wakuu ni wizara hii ambayo iko mbele yetu, kwa sababu mamlaka mbili zinaingia katika uratibu wa suala hili, inaingia *UUB* inaingia na Mamlaka ya Bandari pale. Kwa hivyo, mimi hapa nataka kujua tu wala sitaki kujua fedha zilizotumika, nataka kujua ni lini kazi hii inakamilika kwa sababu ni muda mrefu, tunaona tu wameweka mabati wenzetu hatujui kinachoendelea, kwa hiyo nataka ujenzi huu aje anambie Mhe. Waziri unamalizika lini.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa nielekee *Airport.* Katika eneo hili Mhe. Mwenyekiti, mwenzangu aliyekaa hapa mwisho alizungumzia suala la mizigo, zipo Kampuni mbili za *ZAT* na *Trans World*. Inavyosemakana na taarifa zilivyo ambazo ninazo mimi kuwa Kampuni hizi mbili mmiliki mmoja wamebadilisha tu majina, hakuna ule uhalisia wa ushindani katika kutoa mizigo na kuondoa mizigo pale, lakini hata hivyo Kampuni ya *Trans World* imepewa mkataba kwa kuendesha huduma hii hata eneo la kuhifadhia ile mizigo hawana.

Mhe. Wanu hapa kazungumza ni aibu, huwezi kuingia mikataba na Kampuni ambayo itahifadhi mizigo ya watu katika kuwatolea hata eneo la kuhifadhia hawana, siku za mvua mabegi ya watu yanaroa, utumbo mtupu. Sasa namuomba waziri atakapokuja kwenye eneo hili atuambie ni kwa nini Serikali kupitia wizara yake iliingia mkataba huu ambao tunajua tu kwa kiasi kikubwa hawa tuliowapa uwezo wao haujakamilika katika kufanyia kazi maeneo haya.

Mhe. Mwenyekiti, mimi leo mchango wangu utakuwa mfupi kwa sababu wengi waligusa maeneo yangu ya kuchangia, lakini naomba niseme tu naunga mkono hoja kwa asilimia 90 asilimia 10 nabakisha nipate majibu katika vibuti nitakavyokuja navyo. Nakushukuru sana Mheshimiwa. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Miraji Khamis Mussa kwa mchango wako. Sasa anafuata Mhe. Salma Mussa Bilali na baadaye atafuatia Mhe. Masoud Abrahman Masoud.

Mhe. Salma Mussa Bilali: Ahsante Mhe.Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa hii kwa wakati huu kuchangia hotuba hii.
Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa na mimi sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyenipa uzima na salama kwa mchana huu kuweza kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa muda huu.

Mhe. Mwenyekiti, pia kwa dhati kabisa naomba nimpongeze Mhe. Waziri na Naibu Waziri pamoja na Watendaji wao wote kwa jumla kwa umakini na umahiri wao waliouonesha katika kuitayarisha bajeti hii. Mhe. Mwenyekiti, na mimi naomba nichangie machache katika bajeti hii na hasa ukizingatia kwamba Waheshimiwa wengi tayari wameshaichangia.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze katika sekta ya usafiri wa nchi kavu. Mhe.Mwenyekiti, naomba nichangie kwamba katika bajeti humu wameeleza kwamba kuna barabara sugu, barabara sugu hizo ambazo mara nyingi huwa zinafanyiwa matengenezo lakini kila baada ya muda zinakuwa zinachakaa sana.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nipate maelezo, kuna barabara sana inakuwa *roundabout, roundabout* tuseme ya Amani, *roundabout* ya Kwerekwe, *roundabout* ya hapa Mombasa. *Roundabout* hizo ni maeneo sugu sana kila baada ya muda zinafanyiwa matengenezo na kila mwaka zinafanyiwa matengenezo, lakini matengenezo yale inapoanza tu msimu wa mvua mashimo yale yanarudia tena, inakuwa kila siku ni kazi hiyo kwa hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Waziri, aniambie ni tatizo gani, hatuna ma-*engineer* wa kutosha, hatuna makandarasi wa kutosha, ni kwa nini hasa inasababisha kila kipindi cha mvua katika maeneo yale kunakuwa yale mashimo yanafunguka na kufikia hadi kwamba inakuwa barabara zile hazipitiki.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo naomba niende barabara ya Miwani. Barabara ya Miwani - Kizimbani, barabara ile Mhe.Mwenyekiti, ni barabara ya wakulima, wananchi wa Miwani na Kizimbani yanajulikana hasa ni maeneo ya kilimo, lakini barabara ile sikuona kutajwa katika bajeti hii, ilitajwa sana nyuma, tumeshaisemea sana, barabara ile hata madereva wanashindwa kupeleka gari kutokana na ubovu na uchakavu wa barabara ile.

Wananchi wa Miwani wanapiga kelele sana, wanafika kuchukua hatua mbali mbali za kusindikiza ile barabara ile itengenezwe lakini barabara ile naona bado kabisa Serikali haijawa tayari kuitengeneza. Naomba sana Mhe. Waziri, aniambie ni lini wananchi wa Miwani wataondokana na tatizo la barabara.

Mhe. Mwenyekiti, pia niende katika Idara ya *UUB*. Mhe. Mwenyekiti, *UUB* niwapongeze sana, niwapongeze sana na wanafanya kazi nzuri, lakini katika hali ngumu sana, vifaa vyao ni chakavu, vya muda mrefu, lakini wanafanya kazi vizuri hivyo hivyo.

Naomba sana Mhe.Waziri uione sana hii Idara, inasaidia sana kwa kweli, inafanya kazi kubwa, lakini inafanya kazi katika hali ngumu mno, naomba sana uione hii Idara na uisimamie, na najua kwa umahiri wako unaweza ukarejesha katika hali ya kawaida, wanataka na wao wafanye kazi zao kwa kujiamini, lakini wanashindwa kabisa kutokana na uchakavu na ukongwe wa vifaa ambavyo wanatumia.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo naomba niende katika Idara ya Usafiri na Leseni. Idara ya Usafiri na Leseni ni Idara ambayo tunaitegemea sana kuingiza mapato katika Serikali yetu, lakini Idara ya Usafiri na Leseni nayo kuna mapungufu, kuna mapungufu mengi pale wanayo, kwanza ufinyu wa ofisi.

Pili unafika wakati vitabu vya ukaguzi vinakuwa haviko pale, inafika wakati vitabu vya risiti vinakuwa haviko, unakwenda unaambiwa vitabu hakuna. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri, aliangalie na hilo ili kuwaepushia wananchi usumbufu.

Mhe. Mwenyekiti, halafu pia naomba niende katika Mamlaka ya Uwanja wa Ndege. Wenzangu walishatangulia, wamemsifu sana Meneja, Meneja ni mtu mzuri sana, ni hodari, ameweza na anaweza.

Uwanja wa Ndege kila mtu shahidi, tunakwenda pale, ameiboresha, neno ambalo Mhe. Haroun halipendi lakini amefanya Uwanja wa Ndege sasa hivi kuwa bora.

Kwa hiyo Mhe. Mwenyekiti, naomba apewe ushirikiano Meneja huyu wa Uwanja wa Ndege, apewe ushirikiano wa dhati ili kuendeleza uwanja ule na pia Uwanja wa *Terminal II* Mhe. Waziri naomba ifanywe juhudi ya makusudi ili uweze kumalizika uwanja ule ili ile sifa ya uwanja wa kimataifa iweze kupatikana.

Mhe.Mwenyekiti, suala la Bandari limeshazungumzwa sana, Waheshimiwa wengi wameshalizungumza, suala la Makontena isipokuwa Mhe. Waziri, naomba hii bandari ya Mpiga Duri iweze kuchukuliwa hatua, na hatua zimeshaanza, hatua ziendelezwe ili iweze kupatikana hii bandari ya Mpiga Duri ili kupunguza usumbufu wa makontena na mambo mengine katika bandari ile.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilisema kwamba sitachangia mengi, na sitachangia kwa sababu mengi yameshazungumzwa, kwa hiyo sitaki kurudia hayo kwa hayo.

Kwa hiyo naomba sana, naomba sana Mhe. Waziri, hayo niliyokwishayazungumza ayafanyie kazi kwa kiasi, na mimi sipunguzi hata *point* moja, nitaiunga mkono mia kwa mia kwa sababu kazi ya Wizara hii nimeiona na kila mwananchi anaiona, kwa hiyo mimi sipunguzi kitu.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hotuba hii asilimia mia kwa mia kwa niaba ya wananchi wangu wa Mkoa wa Kusini Unguja. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Salma kwa michangio yako na kuokoa muda, sasa anafuata Mhe. Masoud Abrahman na baadaye afuatie Mhe. Maryam Thani Juma.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze moja kwa moja na suala zima la ununuzi wa meli ya M.V Mapinduzi. Nimpongeze Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kufanya maamuzi pamoja na Baraza la Mapinduzi na Baraza hili tukufu la Wawakilishi pamoja na wananchi kwa kuamua kununua meli mpya ya Mapinduzi, nipongeze sana kwa hilo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini nina masikitiko. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar baada ya Mapinduzi mwaka 1964 iliamua kununua meli mbali mbali,

imenunuliwa meli ya M.V. Mapinduzi I, ikanunuliwa meli ya M.V. Maendeleo, M.V. Jamhuri, M.V. sijui Afrika na meli nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, la kusikitisha meli hizi tokea kipindi hicho mpaka leo zimeshindwa angalau kuzaa mtoto mmoja, yaani kupata faida katika meli hizo, na meli hizo kila zinaposafiri zikienda Pemba zimejaa zikirudi zimejaa, zikienda Bara zimejaa zikirudi zimejaa, lakini mpaka leo tumeshindwa angalau kuzalisha meli moja iliyokuwa ni faida ya meli hizi ambazo zinafanyiwa kazi kila siku na ndio maana mpaka ukaja ukatokezea mtihani wa kuzama meli. Serikali kwa kukata ruzuku kwa kila Wizara ya Serikali ikaweza kwenda kununuliwa meli hii ya M.V. Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo ninaloliomba kama Serikali itakuwa inapata faida basi iendelee kudumu na hizi meli ambazo zinaagizishiwa na Serikali, kama haipati iwape wafanyabiashara binafsi ili waendeleze, kufanya biashara iliyokuwa hupati faida sio vizuri, ukifanya biashara iwe ile ambayo unapata faida.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niwaunge mkono wale waliozungumzia suala zima la barabara ya Miwani - Kiboje.

Barabara hii kwa kweli ni ya muda mrefu na tokea Waziri Mhe. Mwakanjuki aliahidi, lakini kwa bahati mbaya mpaka leo haijajengwa barabara ile.

Katika bajeti hii imeonekana kwenye vipaumbele haipo, lakini kwenye jaduweli imeoneshwa kama barabara hii itajengwa.
Mhe. Mwenyekiti, nimepata wasi wasi isijekuwa zile ahadi ambazo zinaenda tokea miaka hiyo mpaka leo na hii mara hii itaendelea kuwa hazitekelezwi, barabara hii ina wakulima wa eneo la kati ambao wanatoka Miwani, Kiboje, Ndagaa wanapita barabara hii; sasa hivi gari ambazo zinabeba mizigo zinalazimika zitoke Miwani zizunguke Bumbwi Sudi zipite Kitundu zije mjini, ni usumbufu mkubwa ambao wakulima wanapata. Kwa hiyo niiombe tu Serikali, mara hii kwa sababu imeandikwa kwenye kitabu cha Ilani ya uchaguzi ya mwaka 2015-2020 ni vizuri barabara hii ikajengwa ili wananchi walio katika eneo hili wapate imani na Serikali yao.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo niende kwenye eneo hili la usimamizi wa barabara. Kwa kweli tuna tatizo la muda mrefu kwenye eneo letu la Kwanyanya. Kwanyanya ni eneo la *stand* ambayo gari zinazotoka Fuoni kuja zake Bububu, eneo lile lina gari nyingi ambazo zinatoka sehemu za Mkokotoni,

Mahonda, Kiwengwa na maeneo mengine, eneo lile mara nyingi haitimizi ndani ya wiki moja utasikia imetokezea ajali.

Mhe. Mwenyekiti, Halmashauri ilikwenda kwa watu wa Mipango Miji, kutaka eneo lile angalau wapewe kwa muda wajenge *stand* ya muda mpaka pale Serikali itakapoamua kufanya lolote wao Halmashauri watatoa, lakini kwa bahati mbaya huwa wanakataa wanasema wao wana mipango yao miji na pale pana mpango maalum, lakini kila baada ya muda pale panakuwa panatokezea ajali. Sasa nimuombe Waziri atakapokuja aseme eneo lile watu wa Mipango Miji lini wataanza kulifanyia kazi, na kama bado hawajaanza kulifanyia kazi.

Kituo cha Mwenge Dar es Salaam kilikuwa ni kituo cha muda, lakini kimefanya kazi kwa muda mrefu sana mpaka pale Serikali ilipotaka kukitumia kituo kile basi wakachukua kituo wamefanya shughuli zao. Kwa hiyo naomba na hapa Kwanyanya kama Serikali haijawa tayari kupatumia eneo lile, basi wapewe Halmashauri ili waweze kuweka kituo pale cha daladala, itakuwa Serikali ya Mitaa inakusanya lakini pia tutapunguza ajali zinazotokea mara kwa mara.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye Idara ya Usafiri na Leseni. Sasa hivi Zanzibar kumekuwa na magari mengi na ukiweza kupata ajali dakika tano tu ukisimama kwenye barabara msururu wa magari unakuwa mkubwa sana, lakini hili linatokana na uzembe, lakini wenzangu wamesema pia waendesha magari waliokuwa hawana leseni, lakini pia kuna vijana wadogo wale wenye uwezo wanaendesha gari wakiwa hawajatimia umri wa miaka kumi na nane.

Ninalomuomba Mhe. Waziri, akija hapa, mimi kwa sababu sielewi ni nani au mtu mwenye sifa gani ana uwezo wa kupewa leseni ya gari kama ni yule mwenye umri zaidi ya miaka 18 au ukiwa na ukiwa wa miaka 13 ukiwa una uwezo wa kupewa gari uendeshe barabarani kama tunavyoona sasa hivi, basi Mhe. Waziri, atakapokuja hapa aweze kutueleza.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapa na mimi niseme suala zima la usimamizi wa barabara wakati wa kujengwa. Kwa kweli ni suala la kusikitisha, kwa sababu barabara zote zilizojengwa Zanzibar ukiondosha zile barabara ambazo wanajenga *UUB* zote baada ya mwaka mmoja utazikuta zimechanika. Na ushahidi wa hayo Mhe. Waziri, hapa kila tukizungumza Mhe. Naibu Waziri, huwa anasema barabara hii nimeshaitembelea na barabara hii nimeshaitembelea. Sasa nataka nipate maelezo mazuri, Serikali imejipanga

vipi kuhakikisha barabara hizi hazipewi wakandarasi waliokuwa hawana uwezo wa kujenga hizi barabara.

Mhe. Mwenyekiti, ukipita kwenye barabara ya Bumbwi Sudi hivi sasa hivi ni aibu, barabara zina mashimo na Serikali yetu kwa bahati mbaya au *UUB* mpaka pahala patokezee ajali ndiyo wanakwenda kuziba lile shimo, kwa hiyo niiombe sana zaidi wanaangalia maeneo ya mjini, lakini maeneo ya vijijini si aghalabu kwenda kuziba.

Kwa hiyo niwaombe sana Idara hii kwa sababu wanafanya kazi nzuri ya kutujengea barabara pamoja na kuwa wanawapa wakandarasi waliokuwa hawana sifa, lakini niipongeze tu Serikali, niwapongeze na hawa Waziri na Katibu Mkuu wote wazee wao wana majina makubwa kwenye nchi hii, kwa hiyo niwaombe sana wasimamie Wizara hii ili ifanye kazi bila ya woga, na pale panapoonekana mkandarasi mbovu, basi Mhe. Magufuli alikuwa anawaondoa wale hawafanyi kazi, lakini pia na posho zao zilizobakia hawalipwi ili mwengine atakayekuja kuomba kazi pale ahakikishe kajiandaa vizuri na ana wakandarasi wazuri.

Mhe. Mwenyekiti, lakini bado niombe Serikali inapotoa barabara kujengwa, Serikali inakuwa na mkandarasi kusimamia, huyu anakuwepo wapi mpaka tukajengewa mabarabara mabovu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo mimi naunga mkono hotuba hii kwa asilimia 99 mpaka pale nitakapoambiwa barabara ya Kiboje - Mndo itajengwa lini.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Masoud, sasa anafuata Mhe. Maryam Thani na baadaye atafutia Mhe. Mohammed Said Dimwa ajitayarishe.

Mhe. Maryam Thani Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa nafasi hii kuweza kuchangia Wizara hii ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

Kwanza kabisa naishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuweza kufanya juhudi zake za kuleta maendeleo katika Zanzibar.

Vile vile naishukuru Wizara hii kwa kuweza kututengenezea barabara mbali mbali, na pia namshukuru Afisa Mdhamini Pemba kwa juhudi yake ya kuweza kushirikiana na watendaji wao kuweza kututengenezea barabara nzuri kabisa ya Wete - Gando na Wete - Konde.

Mhe. Mwenyekiti, barabara zetu hizi ni nzuri sana tena za sifa hata Mhe. Hamza ameziona. Mhe.Mwenyekiti, barabara zetu nzuri sana lakini kuna mapungufu madogo ambayo yamechangia wananchi wetu kulalamika kuhusu upitishwaji wa barabara zetu hizi.

Mhe. Mwenyekiti, wananchi wangu wa Jimbo la Gando wanalalamika sana kulipwa fidia zao katika upitishwaji wa barabara hizi. Wananchi wangu wanalalamika mpaka sasa bado baadhi yao hawajalipwa fidia hizi kutokana na upitishwaji wa barabara ya Gando - Wete.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alikuja kututembelea Gando akaenda Ukunjwi na humo alifanya mikutano yake na aliahidi wananchi hawa waliokuwa hawajalipwa fidia zao muda mfupi sana watalipwa fidia zao. Lakini cha kusikitisha Mhe. Mwenyekiti, mpaka sasa wananchi hawa baadhi yao hawajalipwa fidia zao.

Kwa hiyo naiomba wizara hii ifuatilie kwa kina jambo hili ili wananchi hawa waliobakia waliokuwa hawajalipwa fidia zao waweze kulipwa fidia kama ahadi ya Mhe. Rais alivyoiahidi.Nimuulize Mhe. Waziri, ni lini ahadi hii ya Mhe. Rais wa Zanzibar itatekelezwa.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na barabara zetu za Gando ni nzuri lakini kuna baadhi ya barabara na barabara yenyewe ni kutoka Gando kwenda Chaoni, na barabara ya Wete kwenda katika kijiji kinachoitwa Chozi.

Mhe. Mwenyekiti, barabara hizo ni mbaya sana na wananchi wanasumbuka katika kusafirisha mazao yao kupeleka mjini ili kuweza kujipatia mahitaji yao ya kila siku.

Mhe.Mwenyekiti, wananchi hawa katika kijiji hichi cha Chaoni walimu wetu wa maskuli ndio wanaotokea wengi huko na wakati wa mvua wanapata tabu sana ya kufika maskulini ili kuweza kuwasomesha watoto wetu; hivyo naiomba sana Wizara hii iwaangalie wananchi hawa kuweza kuwatengenezea barabara zao hizi.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika Shirika hili la Bandari. Tunashukuru sana kuona kwamba kwenye kitabu hiki imeeleza kwamba bandari ya Wete itafanyiwa matengenezo.

Naiomba Wizara hii ijitahidi kufanya matengenezo hayo kwa haraka ili wananchi wengi wa Mkoa wa Kaskazini ambao wanapata tabu sana ya usafiri

kwenda Unguja kufanya biashara zao. Itengenezwe kwa haraka ili waweze kufanya biashara zao vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, Gati hii ya Wete ni muhimu sana kwa wananchi wetu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, kwa sababu wananchi wa Mkoa wa Kaskazini Pemba ndio wengi wafanyabiashara, kwa hiyo itakapoimarishwa Gati hii ya Wete wananchi hawa watafaidika sana kutokana na biashara zao na vile vile wananchi hawa ndio ambao watakaosababisha Serikali yetu kupata mapato kwa wingi, kutokana na wafanya biashara hawa ni wengi, na mpaka sasa bandari hii haijatengenezwa, kwa hiyo wanapata shida sana. Naiomba sana serikali ijitahidi kutengeneza Gati yetu ya Wete.

Mhe. Mwenyekiti, naipongeza tena Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kututengenezea meli yetu ya *MV* Mapinduzi II, meli yetu hii ni nzuri, na meli yetu hii ina sifa kubwa. Kwa sababu wananchi kutoka Pemba kuja Unguja na kutoka Unguja kuja Pemba sasa hivi hawapati tena usumbufu mkubwa kwa kweli.

Kwa hivyo naiomba Serikali ijitahidi sana kama inavyojitahidi meli hii kufanya kazi zake vizuri, ijitahidi kuokoa muda wa kukaa sana kwenye bahari, kwa sababu wananchi huwa wanachoka sana kukaa masaa mengi, lakini naishukuru meli hii ya MV Mapinduzi muda wake si mkubwa sana kuliko meli nyengine.

Kwa hivyo nasema na hizo meli nyengine zijitahidi kuokoa muda, angalau ule muda wa kukaa sana kwenye meli uwe mdogo, kwa sababu watoto huwa wanalizana kwenye meli, huwa washachoka sana, kwa hivyo hata hizo meli nyengine naziomba muda wautumie mfupi.

Mhe. Mwenyekiti, naipongeza tena serikali kwa kutaka kututengenezea kiwanja chetu cha Uwanja wa Ndege uliopo Chake Chake. Naishukuru kwa jitihada zake hizo iendelee kututengenezea uwanja wetu mzuri huo uwe uwanja wa kimataifa, na ndege kubwa ziweze kutua katika uwanja wetu uliopo Chake Chake.

Mhe. Mwenyekiti, naliomba Shirika hili ama Wizara ijitahidi kusema na wamiliki wa vyombo hivi waweze kupunguza gharama za usafiri kutokana na wananchi wengine hali zao ni duni na wengine huwa hawawezi kusafiria maboti kutokana na hali zao. Kwa hivyo naiomba sana wizara hii ijitahidi kushirikiana na wenye vyombo hivi ili wananchi wetu wapunguziwe gharama za usafiri.

Mhe. Mwenyekiti, mchango wangu ndio huu lakini ninamwambia tena waziri ajitahidi na anieleze ni sababu zipi mpaka leo ahadi ya Rais haijaweza kutekelezwa kuwalipa fidia wananchi wangu wa Jimbo la Gando.

Kwa hayo machache naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia 95 kutokana na wananchi hawa hawajalipwa fidia zao mpaka hivi sasa. Baada hayo machache naiunga mkono asilimia 95 hotuba hii. Ahsante.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa imani yako kwa kuweza kuniruhusu na mimi kidogo angalau nichangie kwa maneno mawili matatu japo muda ni mdogo sana.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Waziri, Naibu Waziri lakini nimpongeze sana Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote lakini tusimsahau sana Afisa Mdhamini Pemba ambaye jitihada tumeziona kwa kazi zake.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza niende tu kwenye karakana kuu ya magari iliyopo Chumbuni. Nilikuwa nataka niiulize wizara karakana hii ipo haipo. Lakini kama ipo karakana hii inafanya kazi gani, kwa sababu gari nyingi za serikali zinapelekwa kwenye magereji binafsi na pesa za malipo yale yanakuwa makubwa zaidi. Kwa nini sasa serikali tusihamie kwenye karakana ile tukapeleka miundombinu iliyokuwa mizuri ili gari zote za serikali zihamie pale ili tuweze kupata basi bei angalau iliyokuwa rahisi kwa kutengeneza vyombo vya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, ushauri ni huo naiomba sana serikali ifikirie kuimarisha karakana ile, na kwa sababu hiyo tuweze basi vyombo vyote vya serikali kuelekezwa pale, mafundi wote wa serikali wapelekwe pale kuanzia rangi mpaka utengenezaji wa magari yenyewe hata kufanya *service*. Kwa sababu gari ya serikali moja inafanyiwa *service* shilingi laki tano, wakati tukifanyia pale tutaokoa pesa nyingi sana. Kwa hivyo ningeomba sana Mhe. Waziri asikie kilio chetu hiki ahamie karakana pale.

Mhe. Mwenyekiti nije kwenye Shirika la Bandari. Kwanza nichukue fursa hii kumpongeza sana Mkurugenzi kwa kazi kubwa anayoifanya. Na nataka kusema hapa Mkurugenzi yule kesho tukianza kumuangalia ataanza kuota mvi katika kichwa chake chote, kazi ngumu sana anaanza kupata. Lakini nimshukuru sana Mkurugenzi na nimpongeze tena kwa kuchagua majembe mengi katika kitengo chake cha *operation*.

Nasema hivi kwa sababu makontena pale yamejaa lakini watu wa *operation* wanafanya kazi *time* zote. Niiombe sana serikali kuweza kuwatumia watu wale saa zote lakini wasiwasahau pale wanapofanya kazi. Mtu anapofanya kazi basi angalau huwa anatizamwa.

Mhe. Mwenyekiti, lakini la kukera zaidi katika serikali hii, moja tumeondoa bandari kavu katika sehemu ile ya Bwawani hili linaleta shida sana. Baadhi ya wenzangu wamezungumza lakini mimi ninazungumza leo, hata jana nilikuwa bandarini kwa yale makontena yalipofungamana wale watu wa *operation* wanashindwa hata kufanya kazi zao, watu wanashindwa hata kutoa biashara zao. Lakini kubwa zaidi ongezeko la bei za bidhaa zinaongezeka kutokana na vitu kuchelewa kutoka bandarini, aidha kuna meli nyingi zimekaa nje kule.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye Baraza lako Tukufu hapo nyuma ukikaa utaona meli mbili zimekaa kwa upande huu sijui kwa upande ule kule wa kwendea Pemba meli ngapi, inaleta shida, serikali inaanza kutu-*beep* fedha zinaongezeka. Tunaomba sana serikali iweze kutafuta kiwanja cha kuweka bandari kavu ili basi tuone makontena yale yanatoka vizuri, biashara zinaenda vizuri, hatimaye basi waweze kufaidika wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye viwanja vya ndege. Nichukue fursa kubwa sana kumpongeza Mkurugenzi lakini na timu yake yote.

Nichukue fursa hii kuwapongeza hasa ndugu zangu wafanyakazi wa *VIP Lounge* wanafanya kazi kubwa sana. Hapa nataka niseme kitu tu Wawakilishi wenzangu katika vikao mbali mbali vya nyuma vilivyopita walikuwa wakipiga kelele sana juu ya utendaji mbovu, juu ya utendaji uliokuwa sio wa viwanja vya ndege. Lakini hatua inaanza moja ndio tufikie elfu moja, hatua moja tumeanza elfu moja tutaipitia, tumpongeze Mkurugenzi kwa hatua yake kubwa aliyofikia. Na sio siri kila mtu kaona utendaji wa pale, kila mtu ana sifa na kuona kitu gani kinafanyika.

Mhe. Mwenyekiti, pale pana walinzi wetu wa vikosi wakati mwengine wanawanyanyasa wananchi na wakati mwengine wanawanyanyasa wazee. Kuna vijana pale pembeni wanayo *show room* yao, pia wanawaingilia weshawavunja mpaka mikono. Sasa hiki kitu kinasikitisha, mimi ni shahidi mkubwa sana, nimepita mzee ikasimamishwa gari apakiwe kwa dakika isiozidi moja. Sasa nataka Shirika hili linambie kusimamishwa gari pale ku-*park* vipi na kuweza kusimamishwa gari.

Chengine kinachonisikitisha kuwa Mamlaka katika sheria yake namba 8 ya mwaka 2011 iliunda sheria ya kuleta ripoti, sijawahi kumuona Mhe. Waziri hata siku moja kuleta ripoti na nina nia ya kuchukua shilingi yangu ikiwa sikupata maelezo ya kutosha juu ya suala hili.

Nimejaribu kutizama vitabu vyote, nimejaribu kupekuwa sheria hizi lakini hakuna hata moja nilipoona kuwa wanaitendea haki.

Mwenyekiti, huwa nashangaa sana na hili Baraza lako litakosa meno ya kuisimamia serikali. Kama taasisi hizi zote hazitaleta ripoti zake hapa halafu matumizi na mapato zinapitishwa na Baraza lako tukufu, nataka uiangalie sana Mhe. Mwenyekiti, Baraza litakosa meno na nguvu ya kuisimamia serikali.

Mhe. Mwenyekiti nije sasa sehemu hizi nyengine za Pemba, nimetembea sehemu za Junguni Pemba, baada ya kutembea sehemu za Junguni Pemba nilikuta sehemu nyingi sana ambazo watu pale baada ya njia kupita nyumba zao zimeharibikiwa. Lakini nataka kusema wamesikitika muda mwingi, mimi mwenyewe nimeshamuona Afisa Mdhamini nishazungumza naye, ningeomba sana wawafanyie utaratibu wapate kuwalipa watu wale kama pana fidia yoyote imetengwa kwa ajili yao basi waweze kupata.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye barabara hizi za ndani. Kwenye Jimbo la Mpendae lina barabara nyingi sana za ndani lakini kati ya hizo Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, wakati ananadi Ilani yake ya Chama cha Mapinduzi wakati anasema na akatoa ahadi kuwa barabara zile moja kutoka Mchina mwisho kuelekea Hospitali ya Mpendae, ambayo imetajwa humu kwenye kitabu chao, lakini vile vile moja kutoka Mchina Soko la mboga mboga kupitia Kaburi kikombe mpaka Jang'ombe, skuli zimejengwa na wananchi wenyewe na viongozi wao wa Jimbo la Mpendae.

Mhe. Rais yeye alitoa kauli kuwa atazimaliza kwa lami. Sasa ningeomba sana barabara hii niliyoambiwa kilomita 1.5 imalizwe haraka iwezekanavyo, ili wananchi wajenge imani basi na kauli ambazo wanatoa viongozi wao wakuu.

Jengine hii barabara iliyotoka Mchina mwisho tungeomba sana, ni barabara ambayo inaweza ikaondosha usumbufu mkubwa wa msongamano wa magari ambao unapitia Mwanakwerekwe, unapitia Mpendae, lakini ikipita hivi ni rahisi sana kuondoa msongamano, tungeomba sana wizara ijitahidi kuona inamaliza barabara zile haraka ili tuone basi usumbufu mkubwa unaweza ukatoweka.

Mhe. Mwenyekiti, niseme tu nilikuwa na mchango huu mdogo, niwapongeze, lakini nasema nina nia ya kuchukua shilingi yangu ikiwa majibu sitopata mazuri katika hayo madogo tu niliyoyasema, na ninaunga mkono hoja kwa asilimia 99.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofi*).

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi awali ya yote nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataala*, ambaye ametujaalia uzima tukaweza kukutana hapa katika Baraza lako Tukufu.

Pia nichukue fursa hii kukushuru wewe kwa kunipatia nafasi hii na mimi nikaongea machache katika wizara hii.

Tatu nichukue fursa hii kumshukuru Waziri, kumpongeza Waziri na Naibu Waziri wake kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya katika wizara yao hii, lakini na watendaji wao mahiri kabisa nawapongeza wote kwa ujumla wao.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi nianze mchango wangu katika ukurasa wa 4 ambapo kuna programu ile inaonesha ujenzi na matengenezo ya barabara.

Kwanza nichukue fursa hii kuipongeza sana Wizara kwa juhudi zake hizo za kujenga barabara kuu zote katika nchi yetu lakini na zile barabara wanazozifanyia matengenezo ninashukuru na napongeza sana kwa hatua hiyo. Lakini mimi nataka nizungumzie au niiombe wizara kuangalia kwa makini wakati ule wa ujenzi wa zile barabara zetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa nini nasema hilo, nasema kwa sababu Serikali naiona inapoteza pesa nyingi sana kwa ujenzi wa barabara halafu tunakuwa hatufiki mwisho tunaanza tena kutia kifusi barabara hiyo inapobomoka tunarudi tena tunatia, yaani kuliko mara 4 au tano utakuta tunajenga barabara moja.

Mimi niishauri serikali ingeaangalia uwezo wake kwa wakati ule ina uwezo wa kujenga barabara ngapi, moja au mbili, lakini zikaenda katika kiwango cha lami ili mwisho wa mwaka ukifika basi tunaweza tukajigamba kama ndani ya mwaka huu tumeweza kujenga barabara hii. Kuliko tunapoteza fedha nyingi lakini tunarudia barabara hizo kwa hizo.

Pia niiombe serikali kuangalia ule uwekaji wa *road reserve* ambao ni jambo muhimu sana katika ujenzi wa barabara. Mhe. Mwenyekiti, tumeona hivi sasa maendeleo ya wananchi wetu wanahisi inapojengwa ile barabara basi wao ni

kusogea karibu na ile barabara yenyewe. Hali ambayo serikali saa nyengine inakuwa inao uwezo wa kujenga barabara lakini inafikiria gharama kubwa za kulipa fidia juu ya majengo wakayoyabomoa kwa wananchi ambao wamejenga pale.
Kwa hivyo ni suala muhimu kabisa kuwekwa alama ambazo zitaonesha mtu katika ujenzi wake wote lakini asije akaifikia alama hii, kwa sababu ndio tumejiwekea akiba itakapotokea ongezeko la kuongeza barabara basi nafasi tuweze kuwanayo ambayo haileti usumbufu wala itakuwa haina gharama.

Mhe. Mwenyekiti, pia niende kwenye mchango wangu katika miundombinu ya Bandari na Viwanja vya Ndege. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii kwa dhati kabisa kuyapongeza mashirika haya kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanaifanya.

Mhe. Mwenyekiti, napenda nipongeze na mjumbe aliyemaliza kuzungumza punde tu alisema, kama kwa kweli kiwanja chetu cha ndege kimepiga hatua au viwanja vyetu vya ndege ambapo kwanza Pemba tulikuwa na kilio cha uwekaji wa taa, taa zimewekwa tunashukuru.

Lakini katika kiwanja cha Pemba mimi nataka kusema bado tulikuwa na kilio cha uzio ambao unalizunguka eneo lile la uwanja wa ndege, hili ni jambo muhimu ambalo linaweza kuzuia wanyama wasiingie na kusababisha hatari katika kiwanja cha ndege. Mheshimiwa bado kilio hicho tunacho, wizara iendelee kuliangalia jambo hilo kwa umuhimu wake na uweze kujengwa uzio.

Mhe. Mwenyekiti, pia ndani ya uwanja wa ndege kulikuwa kuna mapungufu yale ya kuwa na vituo vile vya afya, watu wa kilimo kwa sababu pale panapitishwa saa nyengine mbegu mbali mbali lazima kuwe na ukaguzi wa watu wale ili kusiingizwe tu vitu kiholela katika bandari zetu na viwanja vyetu vya ndege. Kwa hivyo bado ninasisitiza vile vitengo viendelee kuwepo, kwa sababu mwahala mule ni muhimu, inaweza kutokea *emergency* saa yoyote lakini kikawepo kitengo kile cha afya kikaweza ku-*save* yale yatakayojitokeza.

Mhe. Mwenyekiti, pia katika uwanja wa ndege wa Pemba kulikuwa na *tower* ile ambayo kwa wakati huo tulotembelea ilionekana kulikuwa kunavuja na wafanyakazi walikuwa wakishindwa kufanya kazi zao kiukamilifu na ile ni sehemu muhimu. Nilitaka kujua imefikia wapi, imeshatengezwa au bado.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, katika Bandari niwashukuru na niwapongeze kwa dhati kwa kuiona bandari yetu ya Mkokotoni na kuweza kuishughulikia hata katika kisiwa chetu kile cha Tumbatu kuanza hali ambayo inaleta usalama

zaidi katika bandari ile. Lakini bado niendelee na kusisitiza pia katika bandari hii vitengo hivyo ambavyo nimevitaja navyo havipo vinavyoshughulika na afya na mambo mengine. Na pale kunaingizwa bidhaa mbali mbali, kuna wanyama wanaosafirishwa kutoka Tanga wanaingia katika bandari yetu ili kujiepusha haya na yale ambayo yanaweza kusababisha kuja kupata matatizo basi na pale vitengo hivyo lazima viwepo.

Pia kuangalia bandari ile kwa umakini kwa sababu ndio vyanzo vyetu vya mapato ambavyo vinaweza kutuingizia mapato. Pale bandari ile inaonekana kukua kwa kasi sasa lazima tuwe makini juu ya kuyachunga mapato hayo.

Mhe. Mwenyekiti, pia niendelee na mchango niende katika programu ya ujenzi na usimamizi wa nyumba zile za maendeleo. Mhe. Mwenyekiti tulikuwa na kilio kikubwa katika majumba yetu haya ya maendeleo katika jengo lile la Kengeja. Nilitaka kujua ujenzi ule umefikia wapi na vipi tumeweza kuhakikisha wakaazi wa jumba lile basi linajengwa vizuri na wanaendelea kuwa katika usalama. Kwa sababu lile jumba lilikuwa bovu na watu walikuwa wanaendelea kuishi. Nilikuwa nataka kujua Mhe. Waziri akija atueleze ni hatua gani zimechukuliwa, na kwamba jengo lile limefanyiwa ukarabati au bado, na kwa nini ikawa bado wakati tangu bajeti zilizopita nyuma tulikuwa tunasisitiza kuhusu jambo hili.

Mhe. Mwenyekiti, pia jengo la treni la Zanzibar, jengo lile ilikuwa maisha ya watu hayako vizuri, kwani lile jengo ni bovu, kwa hiyo tulitaka nalo kujua ni hatua gani ambazo zinachukuliwa ili kuhakikisha wananchi wa pale wanaendelea kuishi kwa usalama.

Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana muasisi wetu hayati Abeid Amani Karume, ambaye kwa kweli aliamua kujenga majengo yale ya Michenzani na aliyajenga kila pahala. Hii ilionesha ni kujali maisha ya wananchi wote wa nchi yake. Kwa hiyo, mimi niishauri serikali, zile sera ambazo zinakuwa nzuri basi ni vizuri hata zikaja awamu ngapi, lakini jambo ambalo zuri ni wajibu wetu tuliendeleze. Sera ile ambayo aliileta Mhe. Karume ya kujenga majengo yale na akaweza kutumia eneo dogo kwa kuweka watu wengi, tungeliiendeleza bado, ingelikuwa tuna ardhi ya kutosha ya kujenga viwanda, ardhi ya kutosha ya kilimo, lakini kwa kuwa ile sera tuliiacha njia panda, kwa hiyo imeweza kubeba tatizo la ardhi limekuwa linatukabili. Kwa hiyo, mimi naomba sera ambayo iko vizuri basi ni vizuri tukaiendeleza kwa maslahi ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli wenzangu wamesema mengi, mimi nilikuwa na mchango mdogo, na hasa nilitaka kuiunga mkono wizara hii kwa sababu ni

wizara ambayo ina majukumu makubwa, na ina kazi kubwa ambayo inawaunganisha wananchi katika mahitaji yao mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, samahani kuna jambo moja nimelisahau.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimuombe Mhe. Waziri kuweka matuta au alama zitakazowafanya madereva kupunguza mwendo kasi hasa katika maeneo ya skuli. Tuna skuli ya Mahonda, tuna skuli ya Pale, magari yanakwenda mbio sana na wanafunzi wanapata ajali mara kwa mara. Kwa hiyo, naomba sana Mhe. Waziri hili uliangalie, na pia mufanye baadhi ya siku kuwaita madereva na kuzungumza nao, kwa kweli inaonekana wenzetu hawaelewi hata yale maeneo wao wenyewe wanapeleka watoto wao humo kusoma, lakini hawaelewi wakifika maeneo yale kama wapunguze mwendo kwa usalama wa vizazi vyetu vijavyo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja, na naomba wenzangu waiunge mkono hotuba hii ili Mhe. Waziri aweze kutujengea barabara na mambo mengine yanayomuhusu katika wizara yake, ili wananchi wetu waweze kufaidika na matunda yao ya Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Tatu Mohammed Ussi: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi hii ili nami niweze kuungana na wenzangu kuichangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

Pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia kusimama wakati huu ili kuweza kuichangia hotuba hii.

Mhe. Mwenyekiti, mchango wangu moja kwa moja utalenga kwenye Shirika la Bandari na Usafirishaji. Pamoja na kwamba Wajumbe wengi wamezungumzia lakini na mimi naomba nitoe machache niliyonayo ndani ya moyo wangu kwa lengo la kulichangia Shirika hili la Bandari.

Mhe. Mwenyekiti, niipongeze Wizara hii ya Mawasiliano na Usafirishaji kwa kuimarisha usafirishaji wa nchi kavu pamoja na usafirishaji wa baharini. Mhe. Mwenyekiti, katika suala la usafiri wa baharini, siku za nyuma tulikuwa tuna kilio kikubwa kwa suala la usafiri, lakini namshukuru Rais wa Zanzibar pamoja na serikali yetu kwa kuimarisha usafiri wa baharini zikiwemo meli zetu za

mashirika binafsi kama vile Bakhressa pamoja na meli ile ya Serengeti, lakini pia na meli zetu za serikali ikiwemo Mapinduzi II na Maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, pia nilishukuru Shirika hili zamani kule Pemba katika Bandari ya Mkoani kulikuwa na kilio cha kituo wanachokaa wasafiri, lakini nashukuru Shirika hili limeweza kuwajengea abiria, na sasa hivi kusema kweli hawana tatizo, wakifika pale kuhangaika huku na kule, isipokuwa wanakaa pale kusubiri usafiri wakati wowote. Hii ni faraja kubwa kwa wasafiri wa visiwa hivi vya Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, abiria wanaokwenda Unguja na Pemba sasa hivi hatuna tatizo, lakini Mhe. Mwenyekiti sasa nawasemea ndugu zangu za Kisiwa Panza na Makoongwe.

Mhe. Mwenyekiti, kama tunavyojua kadhia iliyotukuta watu wa Pemba kutokana na mambo ya kisiasa, naomba Shirika hili liangalie kwa kina kurudisha ule mfumo wa zamani uliokuwepo wa kuwapelekea boti wananchi wetu wa visiwa hivi viwili vya Makoongwe na Kisiwa Panza kwa sababu ya kupunguza ile kadhia ya usafiri. Kwani wananchi hawa tokea kumalizika kwa uchaguzi, ingawaje wanasafiri lakini wanasafiri kwa shida kubwa sana, kwa sababu ya ubaguzi uliopo wa kisiasa.

Kwa hivyo, naishauri serikali kutafuta boti kuweka katika visiwa vile viwili au hata na visiwa vyengine vyenye kadhia kama hii.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo nije kwenye suala la wafanyakazi wa mawasiliano sehemu ya barabara. Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Mawasiliano imeajiri wafanyakazi sehemu ya barabara kwa lengo la kusafisha mule barabarani, palipoharibika kuweka vizuri lakini wafanyakazi hawa inaonekana uadilifu wao ni mdogo katika kutenda kazi zao.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu wafanyakazi hawa sijui kama wana wasimamizi mule vituoni au hawana, lakini wanapokwenda kazini wanakwenda muda wanaotaka na kuondoka muda wanaotaka, kwa sababu hawana usimamizi mzuri.

Mhe. Mwenyekiti, hii inatuletea hasara, kwa sababu wafanyakazi hawa wanalipwa lakini utendaji wao wa kazi hauridhishi, na hauridhishi kwa sababu wanakwenda muda wanaotaka na kuondoka muda wanaotaka. Kazi ya kufanywa siku moja, pahali pa kukata majani siku moja panakatwa siku tatu, na wafanyakazi hawa wanakaa kitako na kuzungumza lakini hatimaye wakiona

gari, na hiyo gari waone gari za viongozi ndio utaona wanajidai kusimama kukata majani.

Kwa hiyo, namuomba yule anayehusika na mambo ya usafishaji wa barabara awasimamie wafanyakazi hawa, kwa sababu wanakula pesa zetu lakini utendaji haupo.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ingawa wenzangu wengi wameshalizungumza suala la bandari ya Unguja kuhusu makontena.
Mhe. Mwenyekiti, yale makontena kwa kweli ni kero na ni hatari kwa abiria.

Mhe. Mwenyekiti, tunapofika kutoka Pemba utaona pale abiria wamesimama chini ya makontena wanasubiri mizigo yao, makontena yale hatujui yalivyokaa na makontena utaona meli imefunga gati karibu na pale. Kwa hivyo, hili nalishauri Shirika liangalie sehemu ya kuweka makontena ili ile gati iwe ni sehemu ya abiria tu na mizigo yao, kwa sababu ni jambo la hatari.

Mhe. Mwenyekiti, pia mwenzangu aliyekaa kitako Mhe. Panya amezungumzia suala la usafiri. Nije kwenye kituo cha daladala cha gari za Bububu pamoja na kuwa hili linaingia kwenye Wizara ya Mawasiliano kwa sababu ni usafirishaji wa abiria, lakini linaingia katika Serikali za Mitaa.

Hili Mhe. Mwenyekiti, abiria wanaotoka Bububu kuja upande wa pili wanapata shida, na wanapata shida kwa sababu madereva wanawachukua abiria wanawaweka pale Malindi, kuna abiria wengine wana miguu yao wanaweza kutembea, lakini kuna abiria wengine hawawezi Mhe. Mwenyekiti. Lakini kero zaidi kwa sisi tunaotoka Pemba, unatoka na mzigo wako kutoka kule bandarini mpaka huku Kisiwandui, jamani hatuoni hili ni tatizo kwa mwananchi.

Kwa hivyo, naiomba wizara inayohusika ya Mawasiliano pamoja na Serikali za Mitaa kuliangalia tena suala hili, kwani wazee wetu pengine mtu ana mgonjwa wake lakini anashindwa kuja kutokana na gari ya Bububu iliyomchukua anakwambia mimi sifiki hospitali. Wakati dereva yule alipopewa kibali na kuchukua leseni amesema atatembea mjini kote, na sijui kuna sababu gani ya kuwa dereva huyu asifike hospitali akamteremsha yule abiria ambaye alimchukua. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, kutokana na hayo mimi namalizia mchango wangu kwa hapo kwa sababu mengi wenzangu wameshayazungumza.

Baada ya maelezo hayo naunga mkono hoja asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mhe. Said Soud Said: (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia bajeti ya Wizara hii ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

Kiukweli ni kwamba bajeti ya wizara hii imepangika vizuri na imejieleza vizuri, na sidhani kwamba kuna upigaji wa buti, kwa sababu mawaziri wote waliojieleza basi mahitaji yao yanaihitajia wizara hii. Anayejenga skuli lazima apite kwenye barabara, anayekwenda kulima lazima apite kwenye barabara, anayekwenda kutibu lazima apite kwenye barabara. Sasa kimsingi wizara hii ndio ime-*hold* na ndio roho ya serikali. Kwa maana hiyo hata hawa Wawakilishi kuja kwao huku kwa ndege, kwa meli, kwa gari wametumia usafiri chini ya wizara hii. Kwa misingi hiyo, kwanza nachukua nafasi ya kumpongeza Rais wa Kwanza wa Zanzibar kwa kazi kubwa aliyoifanya, hayati Abeid Amani Karume, kazi ya kuifanya nchi hii iwe na barabara kila pembe na *Alhamdulillah* pamoja na kwamba nyingi zimekuwa katika hali mbaya lakini tunaahidi kwamba serikali itakuwa tayari kuzifufua.

Vile vile nachukua nafasi hii kumpongeza Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuamini kwamba Balozi Ali Karume na Mhe. Katibu Mkuu wa Wizara hii Mustafa Aboud Jumbe wana uwezo mkubwa wa kuweza kuzisimamia njia hizi, wana uwezo mkubwa wa kuweza kuifanya wizara hii ikarudi tena pale kama zamani, ambapo lengo la Mapinduzi ya Zanzibar ni kuwafanya Wazanzibari waondokane na shida za usafiri, shida za ujenzi na shida za mawasiliano.

Kiukweli ni kwamba serikali inajipanga vizuri katika kuondoa shida hizi, na nataka ieleweke wazi kwamba wizara hii kwa muda wa miaka mitano ilikuwa imekamatwa na watu waliokuwa wanasema hawajapata serikali. Kwa hiyo, hakuna lolote lilokuwa limefanywa katika kipindi kile, isipokuwa walikuwa na nia ya ku-*demote* yale maendeleo ya Mapinduzi na hatimaye Mwenyezi Mungu amewajaalia wamekaa upande kwa hiari zao.

Mhe. Mwenyekiti, kimsingi sasa wizara hii imekamatwa na wazalendo, na tunaamini kwamba serikali iliyopo madarakani ina uwezo mkubwa wa kuharakisha maendeleo yale yote yaliyokuwa hayapatikani yatapatikana kwa muda mfupi sana.

Tunaamini kwamba watendaji wa wizara hii watakuwa tayari kutoa mashirikiano, kutoa maelekezo, ilimradi tuweze kufikia lengo la serikali pale inapotakiwa.

Wito wangu kwa watendaji wote wa serikali, kwa sababu tumekubali kufanya kazi ya kumsaidia Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, nawahakikishia tena watendaji wa serikali wa wizara hii na wizara nyengine, sitokuwa tayari kuiliachia jipu. Nitapasua jipu popote litakapokuwa, kwa vile wasije wakaona kwamba Ali Karume atakuwa haoni labda na Said Soud atakuwa haoni. Mimi nikiona nitapasua jipu, na si wizara hii tu, wizara zote nikiona kuna uharibifu wa utendaji kwa nia ya kuidumaza serikali sitokuwa tayari.

Kwa hiyo, wale waliokuwa bado hawajakubali kuona kwamba serikali hii ndio serikali halali wakajirekebishe, maana mimi nawajua, na wengi wako katika wizara hii, wakajirekebishe, wawe tayari kufanya kazi chini ya serikali hii, hawako tayari basi wakae upande watuachie nafasi tuendeleze serikali. Kwa maana hiyo, napenda kuchukua nafasi hii kusema kwamba ni wajibu wetu Wawakilishi kupitisha bajeti hii kwa nderemo, kwa maana ya kwamba tumpe nafasi Mhe. Ali Karume afanye kazi yake vizuri pamoja na Naibu Waziri wake, pamoja na watendaji wake ni wajibu wetu kusimamia yale yote yalikuwa yamekuwa na kasoro katika majimbo yetu, kutoa taarifa ili wizara iweze kufanya kazi yake vile inavyotakiwa.

Pia ni wajibu wetu kulinda rasilimali ambazo tunazo, wenzetu wameanza *operation* ya kuharibu migomba, mikarafuu na minazi watakuwa tayari kuharibu hata madaraja hawa. Kwa hiyo, tuwe tayari kuhakikisha kwamba tunalinda njia zetu kwa namna yoyote ile, ili tufikishe nia ya serikali pale inapotakiwa.

Mhe. Mwenyekiti, tunaamini chini ya uongozi wa Dkt. Ali Mohamed Shein tutapiga hatua kubwa, yale yote ambayo yanaelezwa kuhusiana na meli kwamba labda ina matatizo, watu hawapati kupitisha magari, hawapati kupitisha mizigo hayo yote yataboreshwa.

Nia ya serikali hii ni kununua meli nyengine itakayowezesha kutoa huduma vile ambavyo tumezoea.

Nia ya serikali hii ni kuharakisha maendeleo yale yaliyokusudiwa na Mapinduzi ya 1964 ili kuondoa dhila na shida ya Wazanzibari.

Sisi ndio Wazanzibari, sisi ndio wazalendo wa nchi hii, wajibu wetu ni kulinda Mapinduzi ya 1964, kwani ndio kigezo cha mafanikio yetu sisi.

Waheshimiwa Wawakilishi, muondokane na ile dhana ya kusema kwamba labda sisi hatuwezi, ni kwamba tunaweza, na tuwaache wale watu sasa waliokuwa wameanzisha kimbembe wao wenyewe wanavutana kama gari mbovu.

Tutapiga hatua ya maendeleo, tutapiga hatua ya kuondoa shida za watu na mabarabara yote tunaamini chini ya uongozi wa Dkt. Ali Mohamed Shein, chini ya waziri wake Ali Karume basi nina uhakika kabisa kwamba mambo haya yatafanikiwa.

Kwa hiyo, nawaomba mabuti na mateke yapungue wakati tukipitisha bajeti hii.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Said Soud, tumemsikia anasema mabuti yapungue, sasa anafuata Mhe. Chum Kombo Khamis, Naibu Waziri wa Afya, ahsante karibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, samahani mimi ni Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo na si Naibu Waziri wa Afya.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante, endelea.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia kuwepo hapa katika Baraza lako tukufu leo hii. Pia nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika hotuba hii ya Mawasiliano na Miundombinu.

Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru pia Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na nimpongeze kwa kuchaguliwa kwake kwa kupata kura nyingi sana. Lakini Mhe. Mwenyekiti, nataka nisichukue muda mkubwa sana, niende moja kwa moja katika mchangio wangu.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rais wa Zanzibar anawapenda wananchi wake sana sana sana. Katika hotuba yake Mhe. Rais katika Wizara hii aliiboresha sana katika kuwapa kipaumbele wananchi wake katika miundombinu ya barabara na mawasiliano. Lakini Mhe. Mwenyekiti niseme kwamba imezoeleka kwa wananchi wetu kuonekana kwamba uharibifu wa miundombinu ni hali ya kawaida.

Mhe. Rais amejitahidi kuboresha miundombinu, lakini wananchi wetu wanaonekana kwamba wakati mwengine hawaipi umuhimu sana miundombinu hii, na wanapokwishatengenezewa kwa mfano kama barabara miundombinu hii wanaifanyia hujuma kiasi ambacho hawathamini mchango wa Rais wetu na Taifa letu kwa jumla na wananchi wake.

Mhe. Mwenyekiti, miundombinu hii wananchi wetu wanaifanyia hujuma kwa mfano zikishakujengwa barabara hizi kuna zile alama ambazo wananchi wetu wanawekewa kwa kuoneshwa madereva wetu hapa pana wanafunzi yaani pana skuli, hapa pana *cross* au pana mpindo mkali na kadhalika.

Hii wananchi wetu alama hizi hasa hasa kisiwani Pemba imeonekana kwamba ukifuatilia miundombinu ile yote au alama zile wamezikata ama kwa njia ya misumeno au sijui wanatumia vifaa gani, lakini hizi alama wanaziondoa kiasi ambacho mara nyingi wananchi wanakuwa wanapiga kelele suala hili wanaomba kwamba kama sehemu za maskuli tujengewe matuta, lakini mna viashiria ambavyo vimewekwa kwa barabara hii kuonesha kwamba hapa pana wanafunzi au zipo skuli, kwa hiyo hii ilikuwa inahitajika waitunze hata ya kujengewa haya matuta ilikuwa inaonesha kwamba hapa pana skuli, hapa pana *cross*.

Mhe. Mwenyekiti, hii niwaombe sana wenzangu Wawakilishi kupitia Baraza hili tukufu tuisaidie Serikali sana, tuwaelimishe wananchi wetu kwamba Mhe. Rais, ameiboresha miundombinu hii basi kwa hiyo na yeye tumpe *support* Mhe. Rais hii miundombinu isiharibiwe.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa nichangie katika kipengele hiki kwa sababu nimeona wenzangu wengi wamesimama na kutetea wananchi, kulipwa fidia zao na kadhalika, hii najua kwamba ni haki yao au ni haki yetu, kwa sababu sote tumeingia humu kwa ajili ya kuwawakilisha wananchi wetu kwa kuwatetea wananchi wetu, lakini hili sisi kama Serikali tunatakiwa tulitetee na tulisimamie ili wananchi hii miundombinu waiheshimu sana sana sana.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho niseme naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na niwaombe Waheshimiwa wenzangu kwa kuwa hili ni kumi la maghfira, kwa hiyo na sisi tuwaghufirie Wizara tuwapitishie bajeti yao ili wafanye kazi zaidi.

Ahsante sana Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Chum. Sasa anafuata Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri, Mhe. Naibu Waziri wa Elimu, tafadhali.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu: Ahsante Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii na mimi kueleza machache ingawa nitayoyaeleza mengi ameshayataja hapa Mheshimiwa, lakini nitajaribu kueleza kwa namna nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba Serikali imekuwa ikiweka miundombinu mbali mbali na katika muktadha huu miundombinu yanahusiana na masuala ya Wizara hii. Imekuwa ikitumia fedha nyingi sana kugharamia masuala hayo, na sisi Wawakilishi tumekuwa tukitetea wananchi wetu ambao ndio wajibu wetu, lakini kuna suala moja ambalo tumekuwa tukilisahau siku zote, nalo ni suala la kueleza wajibu wa wananchi wetu katika kutunza mali za umma.

Mhe. Mwenyekiti, kumezuka tabia hatua kwa hatua za watu kuchukia miundombinu inayoletwa na shughuli za kimaendeleo, labda tunaweza tukaita kama tutatohoa maneno tunaweza tukasema *development phobia,* yaani kila kitu cha maendeleo baadhi ya watu wanakichukia na kama alivyosema mwenzangu wanakihujumu.

Kwa hivyo tabia hii ya kuharibu na kudhoofisha *activities* na miradi inayohusiana na maendeleo haipaswi kuachwa hivi hivi tu, kwa hiyo sisi Wawakilishi wa wananchi Mhe. Mwenyekiti, tuna wajibu sambamba wa kutetea haki zao lakini pia na kuwaeleza wananchi wajibu wao, lazima mambo haya yaende sambamba, ikiwa yatakwenda upande mmoja tu Serikali itafanya wajibu wake sawa, lakini siku ya pili baadhi ya wananchi wanahujumu, kwa hivyo inakuwa washa zima washa zima hatuwezi kwenda pahali. Kwa hiyo lazima sisi Wawakilishi tuendelee kuwaelimisha wananchi wetu katika shughuli zetu, katika mikutano yetu na kila kitu chetu, lakini kama hatujafanya hivyo kwamba tunakuwa tunatetea tu, kwa kweli tutakuwa tunadhoofisha juhudi za Serikali katika kuleta maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, tabia hizi ambazo tunaweza kuzinasibisha na kumomonyoka kwa maadili ya watu wetu, inawezekana ikaelezwa kwa namna mbali mbali wanasaikolojia wana namna yao ya kueleza tabia hii, wanasiasa tuna namna zetu ya kuelezea tabia hii na wanafalsafa wana namna zao za kuelezea falsafa hiyo, lakini kwa vyovyote vile lazima tabia hii ikomeshwe katika jamii yetu.

Serikali haiwezi tu kuendelea kujenga miundombinu baadhi ya watu wakahujumu, nafikiri suala hili tuna wajibu sote Serikali na sisi Wawakilishi

wa wananchi kuwaelimisha watu wetu kujua umuhimu wa miundombinu hii ambayo inayoletwa na Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, wakati mwengine kwa bahati mbaya mtu inaweza kuwa ni jambo linamhusu yeye mwenyewe maadam linatokana na Serikali basi akalihujumu tu, kama hizo barabara inatuhusu sote lakini siku ya pili unaihujumu, kama hiyo hospitali inatuhusu sote labda siku ya pili unaihujumu, kama ni skuli inatuhusu sote unahujumu, kama ni meli inatuhusu sote, hizi ni tabia za kibinadamu, kwa hiyo nafikiri lazima tuzirekebishe.

Mhe. Mwenyekiti, na tunaweza kurekebisha tabia hizi kwa kuelimishana tu kidogo kidogo hatua kwa hatua. Kwa hiyo hapa naiomba pia Wizara hii inahusiana na miundombinu na wasisite kuendelea kuwaelimisha wananchi kupitia vyombo mbali mbali vya habari, hii inaweza kusaidia hatua kwa hatua watu wanaweza wakaelewa, lakini hatuwezi kukaa kimya tu kwamba mali inahujumiwa, miundombinu inahujumiwa sisi tunakaa kimya, hii itakuwa si busara, kwamba sisi Wawakilishi wa wananchi tuna wajibu wa kufanya hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, tokea hapo tunaelewa kwamba rasilimali tuliyonayo ni chache mno. Juzi moja nilisema *is like "watering an elephant in the desert,* halafu tunaacha wananchi wetu wanahujumu. Kwa hivyo ndugu Mwenyekiti ni wajibu wetu Wawakilishi kuwaelimisha. Na tunaweza kuwaelimisha kwa njia mbali mbali, tunaweza kuwaelimisha hatua kwa hatua, elimu hii ya kuthamini na kuheshimu mali ya Serikali, tunaweza kuianzisha katika madarasa ya msingi, sekondari na kadhalika, lakini pia na kupitia elimu nyengine ambazo watu wanazielewa, tukifanya hivyo nadhani tunaweza kutunza hii miundombinu yetu katika muda muafaka unaotakiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa una dakika moja.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana labda kabla sijamaliza niseme kwamba wananchi wetu wana jukumu kubwa la kuhakikisha kwamba wanaheshimu na wanatunza miundombinu ya maendeleo.

Naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja, ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Mchangiaji wetu wa mwisho kwa leo itakuwa ni Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo, na yeye ana dakika tano Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwanza nichukukue fursa hii kumshukuru *Allah Subhana Wataalla* Muumba vyote kwa kutujaalia alasiri hii na sisi kupata nafasi hii ya kuchangia hotuba hii.

Niendelee kumshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein kwa imani kubwa aliyokuwa nayo ya kumteua Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji Mhe. Ali Abeid Amani Karume, hii inathibitisha wazi tu kwamba umakini alioufanya kwenye uteuzi ndio umakini aliokuwa nao Mhe. Waziri wa Ujenzi.

Mhe. Mwenyekiti, nichukue dakika chache tu kuchangia machache. Kwanza kabisa nichangie suala zima la mawasiliano.

Mhe. Mwenyekiti, suala la mawasiliano ndio suala pekee ambalo linawafanya binadamu kukamilisha mambo yao, bila ya mawasiliano masuala yote yanakuwa magumu. Kwa hiyo umuhimu wa mawasiliano napenda Waheshimiwa wenzangu wauone katika bajeti hii. Mawasiliano yaliyokuwepo hapa kwenye miundombinu baina ya jamii na jamii, baina ya chombo na chombo ndio pekee ambayo yatakuza uchumi wa nchi yetu na maendeleo ambayo Zanzibar tunataka kuyafikia katika kipindi hiki ambacho awamu hii ya pili ya Serikali ya Dkt. Shein imeyakusudia.

Mhe. Mwenyekiti, lakini tunapozungumzia mawasiliano ya miundombinu nataka sana kuyalinganisha na ujenzi wa miundombinu. Unapokuwa na ujenzi mzuri wa miundombinu ndio mawasiliano yanapokuwa yanakuwa mazuri zaidi.

Mimi nataka niwaambie tu Waheshimiwa wenzangu kama ulivyoonekana umuhimu wa kuwa na habari katika taifa letu ndio kunapo umuhimu wa kuwa na mawasiliano katika utendaji wa kazi zetu hizi. Na nasema hili kwamba nchi yetu inategemea uchumi mkubwa sana wa utalii, lakini utalii hauwezi kuwa na tija bila ya kuwa na mawasiliano mazuri, bila ya kuwa na ujenzi wa miundombinu mizuri.

Tutizame mwanzo kabisa utalii ulivyoanzishwa miaka ya 1992 ulionekana kwamba una udumazi wa aina yake, lakini baada ya kurekebisha mawasiliano na miundombinu hususan hii ya barabara basi utalii wetu ndio umetapakaa kutoka pembe ya Kaskazi mpaka pembe ya mwisho ya Kusini katika visiwa vyetu.

Mhe. Mwenyekiti, hivyo ningeomba sana Wizara hii kwa kushirikiana pamoja na sisi kumuunga mkono Mhe. Waziri, basi miundombinu itiliwe mkazo hususan katika kuleta mawasiliano kwenye vijiji. Tutizame vijiji vyote ambavyo vinatoa utalii kwa wingi zikiwemo zile sehemu zenye fukwe, zikiwemo sehemu zenye vivutio, sehemu za magofu, basi miundombinu yetu tuhakikishe umejengwa katika uimara mkubwa na mle ambapo mnaonekana sasa hivi mna uharibifu basi tuhakikishe kwamba miundo mbinu ile tunairekebisha ili kukuza utalii wetu.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na dakika chache nilizokuwa nazo za kuchangia na pamoja na kwamba unanitizama sana nataka kwanza niunge mkono hoja iliyowasilishwa na Mhe. Waziri, naunga mkono hoja kwa asilimia mia, na nataka niwaombe basi Waheshimiwa Wawakilishi kwa nia moja, mmoja hapa tumepata msimamizi wa kuweza kusimamia Wizara yetu hii. Tumepata mtu ambaye yuko *linear* anaposema hapa panatakiwa pafanywe yeye hufanya, anaposimamia hapa patekelezwe utekelezaji wake haurudi nyuma, kwa maana hiyo basi nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi sote kwa pamoja mapema tu kesho kutwa tukifika tuunge mkono hoja hii kwa asilimia mia bila ya vikwazo, bila ya vikwamizi vya aina yoyote, sitarajii kwamba kutakuwa kuna mambo mengi ya kusitisha Wizara hii, mambo yote tuyaone kwamba yanatoka mstari mpya na yanaingia mstari mpya.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Waheshimiwa Wajumbe, hadi hapo ndio mwisho wa uchangiaji kwa siku ya leo.

Kwanza kuna tangazo kabla sijaahirisha ni kuwa Waheshimiwa Wajumbe wote mnatakiwa kufika katika ukumbi wa juu mara baada ya kuahirishwa kikao hiki, kuna maelekezo muhimu kutoka kwa Mkurugenzi wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii *ZSSF* Zanzibar, mnaombwa muhudhurie mara baada ya kuahirishwa kikao hichi.

Baada ya hapo kwa sababu muda umeshafika naomba niwashukuru sana Wajumbe wote waliochangia kwa maandishi, waliochangia moja kwa moja na wale ambao waliokuwa hawakupata kwa bahati mbaya kwa muda basi wanaweza kupeleka michangio yao kwa Mhe. Waziri kwa maandishi. Baada ya hapo niseme naliakhirisha Baraza hili hadi siku ya Jumatatu saa tatu asubuhi.

(Saa 8.57 mchana Baraza liliahirishwa hadi tarehe 20/06/2016 saa 3.00 za asubuhi)